# NAFASI NA MAHALI KATIKA HADITHI FUPI TEULE ZA DIWANI YA *KURUDI NYUMBANI NA HADITHI NYINGINE*

**SPACE AND PLACE IN SELECTED SHORT STORIES IN *KURUDI NYUMBANI NA HADITHI NYINGINE* ANTHOLOGY**

**NJOROGE FLORENCE WAHU**

**C50/CE/29153/2015**

**IDARA YA KISWAHILI CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**NOVEMBA, 2024**

## IKIRARI

**MTAHINIWA**

Kazi hii ni tokeo la utafiti wangu binafsi na haijapata kuwasilishwa katika chuo kikuu kingine kwa kusudi lolote lile.

Sahihi:……………………………… Tarehe: 19/11/2024……………

**Njoroge Florence Wahu**

C50/CE/29153/2015

**MSIMAMIZI**

Tasnifu hii imetolewa kwa ufahamu na kibali changu kama msimamizi aliyeteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi:……………………………… Tarehe: 20/11/2024

**Dkt. Jesse Murithi**

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu Cha Kenyatta

## TABARUKU

Kwa mume wangu mpendwa Ndugi na wanangu Macharia, Njeri na Njoroge.

## SHUKRANI

Namshukuru Maulana kwa fadhila zake tele katika kipindi kizima cha utafiti wetu. Namshukuru kwa afya njema amani na kunipatanisha na waja wenye moyo safi walionisaidia katika shughuli nzima ya utafiti. Shukrani za dhati zimwendee mwelekezi na msimamizi wangu Dkt. Jessee Murithi kwa kunielekeza ipasavyo katika utafiti hadi kufikia kilele chake. Aidha namshukuru Dkt. Arege kwa mchango wake wa kunielekeza katika hatua za mwanzo za utafiti huu. Nawashukuru pia wahadhiri wangu wa Chuo Kikuu cha Kenyatta walionifunza na kunipa mwelekeo wa utafiti pamoja na wahadhiri wa vyuo vingine wakiwemo Mhadhiri Ester, Mhadhiri Gikonyo na Prof. Kineene wa Mutiso. Mungu awabariki. Kwa namna ya pekee, namshukuru mamangu kwa kunihimiza kila wakati kulenga juu katika maisha. Ahsante kwa kauli yako, “Mwanangu, yote yawezekana.” Aidha nawashukuru wanangu na mume wangu kwa uvumilivu na mchango wao wa namna mbalimbali katika utafiti huu. Singependa kumsahau rafiki yangu Ruth kwa kunipa ari ya kwendeleza masomo yangu. Isitoshe, nawashukuru wanafunzi tuliosoma nao kwa ushirikiano wao katika utafiti huu pamoja na walimu wenzangu walionifaa sana wakati wa utafiti.

## FASILI YA ISTILAHI

**Fremu** – Maeneo ambayo hutokea katika mawazo, ndoto na kumbukumbu za wahusika katika hadithi ambayo si mandhari ya hadithi husika.

**Mahali** – Sehemu fulani katika nafasi yenye maana inayotokana na tajriba za watu na ambayo huwawezesha wanajamii kutimiza mahitaji yao ya kila siku.

**Kivuli –** Mwasilishi mtazamaji wa nafasi asiye msimulizi wala mhusika katika hadithi.

**Mapinduzi –** Mtazamo mpya wa kuliangazia jambo, tofauti na ule ilivyozoeleka.

**Mtazamo wa kipanorama-** Mtazamo ambao mwasilishaji wa jambo au kitu husimama mahali ambapo anakiona kikamilifu kwa uwazi bila kizuizi.

**Nafasi –** Jumla ya mandhari ya matukio pamoja na vielezo na fremu katika hadithi.

**Nafasi ya kijamii -** Maana zinazohusishwa na nafasi fulani iliyozalishwa na jamii kutokana na vigezo mbalimbali vya jamii hiyo.

**Vielezo** – Ufafanuzi wa kina wa mahali, kitu, mtu na tukio.

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| BBC | British Broadcasting Corporation |
| Uk. | Ukurasa |

## YALIYOMO

**IKIRARI** .......... **ii**

**TABARUKU** .......... **iii**

**SHUKRANI** .......... **iv**

**FASILI YA ISTILAHI** .......... **v**

**YALIYOMO** .......... **vii**

**IKISIRI** .......... **xv**

**ABSTRACT** .......... **xvi**

**SURA YA KWANZA** .......... **1**

**USULI WA UTAFITI** .......... **1**

1.1 Usuli wa Mada .......... 1

1.2 Suala la Utafiti .......... 8

1.3 Malengo ya Utafiti .......... 9

1.4 Maswali ya Utafiti .......... 10

1.5 Sababu za Kuchagua Mada .......... 10

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti .......... 14

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada .......... 15

1.8 Msingi wa Nadharia .......... 22

1.8.1 Nadharia ya Naratolojia .......... 22

1.8.2 Vipengele vya Nafasi na Mahali .......... 25

1.8.2.1 Nafasi ya msimulizi .......... 25

1.8.2.2 Nafasi ya simulizi/hadithi .......... 25

1.8.2.2.1 Mandhari .......... 26

1.8.2.2.2 Fremu .......... 26

1.8.2.3 Vielezo ........ 27

1.9 Mbinu za Utafiti ........ 27

1.9.1 Muundo wa Utafiti ........ 27

1.9.2 Mahali pa Utafiti ........ 28

1.9.3 Uteuzi wa Sampuli ........ 28

1.9.4 Ukusanyaji wa Data ........ 30

1.9.5 Uchanganuzi wa Data ........ 30

1.9.6 Uwasilishaji wa Data ........ 30

1.9.7 Uzingativu wa Maadili ........ 31

1.10 Hitimisho ........ 31

**SURA YA PILI ........ 33**

**VIPENGELE VYA NAFASI NA MAHALI KATIKA DIWANI YA *KURUDI NYUMBANI* NA *HADITHI NYINGINE* ........ 33**

2.0 Utangulizi ........ 33

2.1 Nafasi ya Hadithi ........ 33

2.2 Nafasi ya Msimulizi ........ 45

2.3 Fremu ........ 47

2.4 Vielezo ........ 51

2.5 Hitimisho ........ 62

**SURA YA TATU ........ 64**

**UWASILISHAJI WA NAFASI NA MAHALI KATIKA DIWANI YA *KURUDI NYUMBANI NA HADITHI NYINGINE* ........ 64**

3.0 Utangulizi ........ 64

3.1 Uhusishaji ........ 64

3.1.1 Uhusishaji Kupitia kwa Jicho la Msimulizi............................................65

3.1.2 Uhusishaji Kupitia kwa Jicho la Mhusika ..............................................66

3.1.2.1 Mhusika kuangalia kupitia dirishani....................................................66

3.1.2.2 Mhusika akiingia mahali fulani kama vile nyumba.............................67

3.1.2.3 Mhusika akitembea mahali fulani kwa mfano mjini. ...........................67

3.1.2.4 Mhusika kutazama kifaa au chombo huku akimwelezea mhusika mwingine kukihusu..........................................................................................68

3.1.2.5 Mhusika anapotengeneza kitu husika ..................................................69

3.2 Mtazamo / Mahali pa Msimamo.................................................................70

3.2.1 Mtazamo wa Kipanorama.........................................................................70

3.2.1.1 Mtazamo wa kipanorama kando..........................................................70

3.2.1.2 Mtazamo wa kipanorama igizi.............................................................72

3.2.2 Mtazamo wa Kimandhari ........................................................................72

3.2.2.1 Mtazamo wa kimandhari hamaji .........................................................73

3.2.2.2 Mtazamo wa kimandhari tuli................................................................73

3.2.3 Mtazamo Karibu .........................................................................................74

3.3 Sifa za Ufafanuzi katika Vielezo ...............................................................75

3.3.1 Sifa za mwonekano/ kuangazwa.............................................................76

3.3.2 Sifa za sauti..................................................................................................77

3.3.3 Sifa za harufu...............................................................................................78

3.3.4 Sifa za mguso...............................................................................................79

3.4 Maumbo ya Vielezo.......................................................................................80

3.4.1 Vielezo virefu ..............................................................................................80

3.4.2 Vielezo vifupi ..............................................................................................81

3.4.3 Vielezo vya kimhutasari ....................................................................83

3.4.4 Ufundi ....................................................................................................84

3.4.5 Historia ya kielezo ....................................................................................85

3.5 Hitimisho ....................................................................................................86

**SURA YA NNE ..........................................................................................87**

**DHIMA YA NAFASI NA MAHALI KATIKA SIMULIZI.......................87**

4.0 Utangulizi ....................................................................................................87

4.1 Nafasi na Mahali katika Ujenzi wa Maudhui ..........................................88

4.1.1 Nafasi na Mahali kama Maudhui.............................................................88

4.1.1.1 Vinyago vya Watalii ..............................................................................88

4.1.1.1.1 Utalii ....................................................................................................88

4.1.1.1.2 Biashara ................................................................................................89

4.1.1.1.3 Mashindano...........................................................................................90

4.1.1.1.4 Bidii .......................................................................................................90

4.1.1.1.5 Ubunifu ..................................................................................................91

4.1.1.1.6 Ukengeushi ............................................................................................91

4.1.1.2 Njozi ya Mtu Mweupe ...............................................................................92

4.1.1.2.1 Ubabe .....................................................................................................92

4.1.1.2.2 Ubinafsi...................................................................................................93

4.1.1.2.3 Kujitegemea ............................................................................................93

4.1.1.2.4 Mabadiliko...............................................................................................94

4.1.1.2.5 Safari .......................................................................................................94

4.1.1.2.6 Subira ......................................................................................................94

4.1.1.2.7 Ujirani mwema .........................................................................................95

4.1.1.2.8 Siri ....................................................................................95
4.1.1.2.9 Sheria ................................................................................96
4.1.1.3 Mioyo ya Chuma .................................................................96
4.1.1.3.1 Utengano............................................................................96
4.1.1.3.2 Bidii ...................................................................................97
4.1.1.3.3 Uwajibikaji ........................................................................97
4.1.1.4 Kurudi Nyumbani ...............................................................97
4.1.1.4.1 Uwajibikaji ........................................................................97
4.1.1.4.2 Mazingira...........................................................................98
4.1.1.4.3 Utabaka..............................................................................98
4.1.1.4.4 Malezi ................................................................................99
4.1.1.4.5 Utamaduni..........................................................................99
4.1.1.4.6 Maamuzi ..........................................................................100
4.1.1.5 Mihuri ya Majanga ...........................................................100
4.1.1.5.1 Kiangazi...........................................................................100
4.1.1.5.2 Dini ..................................................................................101
4.1.1.5.3 Nafasi ya mwanamke.......................................................101
4.1.1.5.4 Mawasiliano.....................................................................102
4.1.1.5.5 Ushirikina ........................................................................102
4.1.1.6 Safari ya Maangamizi.......................................................103
4.1.1.6.1 Utamaduni........................................................................103
4.1.1.6.2 Mazingira.........................................................................103
4.1.2 Nafasi na Mahali katika Kumulika Maudhui ya Hadithi.......................104
4.1.2.1 Vinyago vya Watalii .........................................................104

4.1.2.1.1 Madhara ya kutokuwa makini ........................................................104
4.1.2.1.2 Mapenzi ........................................................................................105
4.1.2.2 Njozi ya Mtu Mweupe .........................................................................106
4.1.2.2.1 Utabaka ........................................................................................106
4.1.2.2.2 Uhamaji.........................................................................................107
4.1.2.2.3 Ukoloni .........................................................................................108
4.1.2.3 Mioyo ya Chuma ...............................................................................109
4.1.2.3.1 Mapenzi ........................................................................................109
4.1.2.3.2 Ushirikiano ...................................................................................110
4.1.2.4 Safari ya Maangamizi ........................................................................111
4.1.2.4.1 Elimu............................................................................................111
4.2 Umuhimu wa Nafasi na Mahali katika Kujenga Wahusika......................111
4.2.1 Hulka za Wahusika ...............................................................................112
4.2.1.1 Vinyago vya Watalii ...........................................................................112
4.2.1.1.1 Chombo ........................................................................................112
4.2.1.1.1.1Msanii ..........................................................................................112
4.2.1.1.1.2 Mwenye tamaa.............................................................................113
4.2.1.3 Mioyo ya Chuma ...............................................................................113
4.2.1.3.1 Watoto wa Kaikai .........................................................................113
4.2.1.3.1.1 Wenye bidii..................................................................................113
4.2.1.3.1.2 Wenye ushirikiano .......................................................................114
4.2.1.4 Kurudi Nyumbani ..............................................................................114
4.2.1.4.1 Cathy............................................................................................114
4.2.1.4.1.1 Mwajibikaji..................................................................................114

4.2.1.4.1.2 Mwenye mapenzi ya dhati ....... 115
4.2.1.4.2 Gatobu ....... 115
4.2.1.4.2.1 Mwenye mapuuza ....... 115
4.2.1.4 Safari ya Maangamizi ....... 116
4.2.1.4.1 Wanakijiji ....... 116
4.2.1.4.1.1 Wasiowajibika ....... 116
4.2.1.4.2 Vijana ....... 116
4.2.1.4.2.1 Wenye ushirikiano ....... 116
4.2.1.4.3 Wanafunzi wa Chuo Kikuu ....... 117
4.2.1.4.3.1 Watovu wa nidhamu ....... 117
4.2.2 Hali za Kisaikolojia za Wahusika ....... 117
4.2.2.1 Vinyago vya Watalii ....... 118
4.2.2.1.1 Chombo ....... 118
4.2.2.1.1.1 Mwenye wivu ....... 118
4.2.2.1.2 Sally ....... 118
4.2.2.1.2.1 Mwenye majivuno ....... 118
4.2.2.1.2.2 Mwepesi wa kushawishika ....... 119
4.2.2.2 Mioyo ya Chuma ....... 119
4.2.2.2.1 Kaikai ....... 119
4.2.2.2.1.1 Mwenye wasiwasi ....... 119
4.2.2.3 Kurudi Nyumbani ....... 120
4.2.2.3.1 Gatobu ....... 120
4.2.2.3.1.1 Mwenye mapenzi ....... 120
4.2.2.3.1.2 Mwenye uchungu ....... 120

4.2.2.3.1.3 Mwenye msimamo........121

4.2.2.3.2 Cathy........121

4.2.2.3.2.1 Mwenye masikitiko........121

4.2.2.4 Mihuri ya Majanga........122

4.2.2.4.1 Obando........122

4.2.2.4.1.1 Mwoga........122

4.2.2.4.1.2 Jasiri........122

4.3 Hitimisho........122

**SURA YA TANO........124**

**MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI NA MAPENDEKEZO........124**

5.0 Utangulizi........124

5.1 Muhtasari wa matokeo ya utafiti........124

5.2 Changamoto katika utafiti........126

5.3 Mchango wa utafiti........127

5.4 Mapendekezo........128

5.5 Hitimisho........128

**MAREJELEO........129**

**VIAMBATISHO........134**

Kiambatisho I: Idhini ya Kufanya Utafiti........134

Kiambatisho II: Cheti Cha NACOSTI........135

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza kipengele cha nafasi na mahali katika hadithi fupi ya Kiswahili kwa kurejelea diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingin*e (2007) iliyoharirirwa na Mwenda Mbatia. Vipengele tofauti vya fasihi kama vile, wahusika na uhusika, mandhari, mtindo na matumizi ya lugha vimetafitiwa na watafiti mbalimbali. Hata hivyo, kadri ya ufahamu wa mtafiti, utafiti kuhusu nafasi na mahali kama kipengele cha fasihi haujafanywa kwa kina katika fasihi ya Kiswahili. Vilevile, diwani teule haijachambuliwa kwa kutumia mtazamo wa nafasi na mahali. Utafiti huu ulinuia kuchunguza: Vipengele vya nafasi na mahali kama vinavyojitokeza katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine,* kuonyesha namna kipengele cha nafasi na mahali kilivyowasilishwa katika hadithi teule, na kuonyesha umuhimu wa nafasi na mahali katika kujenga maudhui na wahusika katika hadithi fupi teule za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Utafiti uliongozwa na nadharia ya naratolojia mkondo wa De Jong (2012) wa nafasi katika usimulizi. Mihimili ya nadharia iliyotumika ni; nafasi ya hadithi, nafasi ya msimulizi, fremu na vielezo. Utafiti ulifanywa maktabani na mtandaoni ili kupata data ya kuufaa utafiti wetu. Mtafiti aliisoma diwani teule, tasnifu na makala mengine muhimu. Uteuze wa sampuli ulifanywa kimakusudi ambapo mtafiti aliteua hadithi sita za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Data ilikusanywa, kuchanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya kimaelezo. Matokeo ya utafiti wetu yaliafiki matarajio yetu kwa kuthibitisha kuwa nafasi na mahali ni kipengele cha kimsingi katika ujenzi wa hadithi. Utafiti ulibainisha vipengele tofauti vya nafasi na mahali ambavyo vinapatikana katika hadithi teule za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Isitoshe, mtafiti alionyesha mbinu mbalimbali zilizotumika kuwasilisha nafasi na mahali katika hadithi teule na hatimaye akaonyesha dhima ya nafasi na mahali katika ujenzi wa maudhui na wahusika wa hadithi teule katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine.* Matokeo ya utafiti huu yatakuwa ya manufaa kwa waandishi wa fasihi ya Kiswahili hususan wa hadithi fupi, wasomi na watafiti wa baadaye wa fasihi ya Kiswahili.

## ABSTRACT

This research sought to study space and place in the Swahili short story with particular reference to a Swahili anthology entitled *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007) which was edited by Mwenda Mbatiah. Different aspects of literature such as character and characterization, setting, themes and style have been researched over time by various reseachers. However, according to the researcher's knowledge, space and place in Swahili literature had not been researched on. Moreover, the selected text has not been subjected to research on space and place. Our research, therefore, focused on identifying the different aspects of space and place found in *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, demonstrating how space and place are presented in various short stories and establishing the importance of space and place in the development of themes and characterization of selected stories in the selected anthology. Our research was guided by the theory of narratology as espoused by De Jong (2012). The tenets of the theory that were used include: story space, space of the narrator, frames and description. Data collection was done in the library and in the internet, through reading selected stories in *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* anthology. We also studied books, dissertations and other relevant literature from the internet. Our study applied purposeful sampling whereby six short stories from the selected text were selected for analysis. Descriptive method of data analysis was used in our research. The research findings were presented by descriptive method. From our analysis, it is evident that space and place takes a central place in the construction of stories. Our research identified the different aspects of space and place found in selected stories of *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* anthology. It also, demonstrated different ways in which the aspects of space and place are presented in the selected text. Finally, our research demonstrated the importance of space and place in the development of themes and characterization in the selected stories of the selected text. In this regard therefore, our research will be of substance to authors of Swahili anthologies, Swahili literature scholars as well as future researchers of Swahili literature.

# SURA YA KWANZA

# USULI WA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia usuli wa utafiti kwa kufafanua vipengee vya kimsingi vya uchunguzi wetu. Ilijadili usuli wa mada ambao ulieleza historia ya hadithi fupi pamoja na kuifafanua dhana ya nafasi na mahali. Isitoshe, suala la utafiti liliwekwa wazi pamoja na malengo na maswali ya utafiti. Sura hii pia ilipambanua sababu za kuchagua mada ya utafiti. Aidha, upeo na mipaka ya utafiti ilibainishwa pamoja na kuonyesha baadhi ya tafiti za awali zilizohusiana na mada yetu ya utafiti. Nadharia iliyoongoza utafiti ilibainishwa na mihimili ya nadharia hiyo iliyofanikisha utafiti huu kufafanuliwa. Hatimaye sura hii ilifafanua mbinu za utafiti zilizojumuisha: muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa data na uzingativu wa maadili.

## 1.1 Usuli wa Mada

Wamitila (2002) anasema kuwa chimbuko la utunzi wa hadithi fupi linanasibishwa na Edgar Allan Poe ambaye ni mtunzi na mhakiki wa kimarekani. Anaendelea kusema kuwa katika karne ya kumi na tisa mtunzi huyu alitoa maelezo yake kuhusu hadithi fupi. Hata hivyo, asili ya hadithi fupi ya Kiswahili inahusishwa na Brander Mathews kwa kuwa ndiye aliyetumia istilahi ya Kiingereza "short story" kumaanisha hadithi fupi, kwa mara ya kwanza. Vilevile, anasema kuwa uandishi wa hadithi fupi kwa lugha ya

Kiswahili ulianza mnamo karne ya ishirini na maendeleo makubwa ya uchapishaji yakashuhudiwa katika miaka ya sabini.

Kwa mujibu wa Mc Onyango (2006), katika ukanda wa Afrika Mashariki, hadithi fupi ya Kiswahili ni ya karne ya ishirini. Anasema kuwa mtafiti mtajika Albert Gerard alifanya kazi nyingi za fasihi za Kiafrika zikiwemo hadithi fupi za Kiswahili ambazo anazipa tarehe ya kati ya karne ya ishirini. Mtafiti huyu anasema kuwa hadithi fupi za Kichina na Kirusi zilitafsiriwa kwa Kiswahili tangu miaka ya elfu moja mia tisa na hamsini. Katika kipindi hicho, kulikuwa na ngano za kiafrika ambazo zilikaribiana na tafsiri za hadithi za Kichina na Kirusi, hivyo, kuwachochea waafrika kuzikubali kwa urahisi na matokeo yake yakawa kutunga hadithi zao wenyewe.

Rollins (1983) anafafanua vipera kadha vya fasihi ya Kiswahili ambavyo vilitangulia kuzaliwa kwa utanzu wa hadithi fupi ya Kiswahili. Anaeleza vipera vya kisa, hadithi, hekaya, kioja na habari. Katika ufafanuzi wake, kisa ni hadithi ambayo inaonyesha mwanzo na matokeo yanayoonyesha adhabu iliyo wazi. Anatoa mfano wa kisa kinachoelezea chanzo cha uadui kati ya kuku na mwewe. Pia anatoa mfano wa *Kisa cha Punda wa Dobi* katika mkusanyiko wa *Swahili Tales* wa Steere (1896).

Akifafanua dhana ya hadithi, anasema kuwa sifa bainifu ya hadithi ni kutamatishwa kwa kutaja adhabu au kisasi kama tokeo la kitendo fulani. Anasema kwamba hadithi ilikuwa kisa cha kweli au cha kubuni. Anaendelea

kusema kuwa, kule Uarabuni, hadithi ilikuwa kisa cha kweli kuhusu nabii na washirika wake lakini baadaye maana hiyo ilibadilika kwa sababu ya tamaduni nyingi danganyifu ambazo zilifanya hadithi kuwa na maana ya uhalisi au uongo yaani ya kubuni. Anatoa mifano ya *Hadithi ya Liongo* pamoja na *Hadithi ya Chewa.*

Dhana nyingine ambayo anaifafanua ni hekaya. Kulingana na maelezo yake, hekaya zina chanzo katika hikaya za waarabu ambazo maana yake ni kuiga. Anasema kuwa miongoni mwa waswahili, hekaya zilimaanisha kitu cha ajabu au cha kushangaza. Mwanzoni, hekaya za Kiswahili zilikuwa kazi ndefu za kubuni zenye maudhui ya kustaajabisha na vifumba macho. Wahusika wa hekaya walikuwa wanyama walioiga tabia za binadamu na kuficha sifa zao. Anatoa mfano wa *Hekaya za Abunuwasi.*

Utanzu wa hekaya ulikuwa na kitanzu tegemezi kilichoitwa kioja. Kitanzu hiki pia kilirejelewa kwa jina maarufu 'ajabu'. Dhana nyingine ambayo aliifafanua ni habari. Anasema kuwa habari ni neno lililotumika kumaanisha ripoti, ujumbe au simulizi ambayo haikuwa na mpangilio maalum wa kimawazo na wa kisanaa. Neno hili pia lilimaanisha historia.

Alieleza dhana nyingine ambayo ni simo na kusema kuwa simo ni masimulizi ya kufananisha au ya kulinganisha. Simo zilikuwa masimulizi ya kitashbiha.
Neno masimulizi lilikuwa la kijumla lililojumuisha vipera vingi vya masimulizi ya kinathari. Masimulizi yalijengwa kwa vipera mbalimbali vya hadithi. Neno hili masimulizi liliibua mjadala mkubwa kwa kuwa asili yake ni

mazungumzo yaliyofanyika jikoni. Anatoa mfano wa *Masimulizi na Mafundisho* kutoka Uarabuni ambayo ni mkusanyiko wa hadithi zenye maudhui changamano.

Ohly (1977) anafafanua vipera vinane vilivyotangulia utanzu wa hadithi fupi ya Kiswahili. Anasema ya kwamba vipera hivi vina sifa zinazofanana, hivyo, vina maana zinazokaribiana sana. Kwa sababu hii, vipera hivi vinastahili kubainishwa ili kuondoa utata wa kimaana. Vipera anavyoshughulikia ni pamoja na: mabuniko anayoeleza kuwa ni hadithi za kubuni, ngano, ambazo ni hadithi fupi za mapenzi, masimulizi, ambacho ni kitendo cha kusimulia, na hadithi, kumaanisha mfululizo wa matukio. Aidha, alishughulikia kipera cha ngano na kusema kuwa hizi ni hadithi zisizo na uhalisia. Dhana nyingine ni kioja. Anasema kuwa kioja ni hadithi zinazoibua taharuki. Pia, anatoa maelezo ya habari na kusema kuwa habari ni ripoti iliyoandikwa kuhusu tukio fulani kama vile, kwenye magazeti au maandishi ya kitawasifu. Hatimaye, anatoa maelezo ya hekaya na kudai kwamba hekaya ni kisa cha kuvutia chenye sifa ya uhalisia au uwezekano wa kuweko.

Bertoncini (1989) anasema kuwa hadithi fupi ya Kiswahili ya kisasa ilizaliwa kisiwani Zanzibar. Anasema kuwa awali, hadithi fupi zilikuwa na sifa tangulizi ambazo hazikuzingatia suala la mtindo. Sifa hizi ziliondolewa baadaye. Kwa mujibu wa mtaalam huyu, Shirika la BBC ndilo lililochangia pakubwa katika kuukuza utanzu wa hadithi fupi ya Kiswahili ya kisasa kwa kuwahimiza wasikilizaji wake kutunga, kuandika na kuwasilisha hadithi fupi za Kiswahili

kwa ajili ya upeperushaji. Mradi huu ulipokelewa kwa dhati na katika miaka miwili ya kwanza mafanikio makubwa yalishuhudiwa ambapo hadithi fupi mia sita ziliwasilishwa. Miongoni mwa hadithi hizi, zilizoonekana bora zaidi zilichapishwa katika mkusanyiko wa *Hekaya za Kuburudisha* ambapo hadi sasa vitabu vinne; *Mapenzi ni Kikohozi (1970), Vituko Duniani (1970), Pavumapo Palilie (1972) na Kinywa Jumba la Maneno (1977)* vinapatikana.

Mbuthia (2003) anasema kuwa ni dhahiri kuwa hadithi fupi ya Kiswahili ya kisasa ina asili yenye msingi katika vipera vingi vilivyoitangulia. Hata hivyo, kati ya vipera hivi vyote hakuna kilicho na sifa zote kuu zinazoibainisha hadithi fupi ya Kiswahili ya kisasa.

Mbuthia na Iribemwangi (2014) wanasema kuwa utanzu wa hadithi fupi ya Kiswahili umekomaa. Utanzu huu umefumwa kwa kutumia mitindo mbalimbali inayoufanya kuwa wa kuvutia, kufahamisha na kuelimisha. Mitindo hii huupa utanzu wa hadithi fupi ya Kiswahili upekee utokanao na mchanganyiko wa mbinu za kigeni na mbinu asilia za Kiafrika.

Tafiti nyingi kuhusu utanzu wa hadithi fupi za Kiswahili zimefanywa na watafiti wafuatao: Mbuthia (2003), Mukopi (2005), Ntiba (2011), Kaui (2011), Kyalo (2012), na Onchangu (2013). Hata hivyo kadri ya ufahamu wetu, ilibainika kuwa mandhari, sehemu mojawapo ya nafasi na mahali, ndicho tu kipengele cha nafasi na mahali kilichofanyiwa utafiti katika fasihi ya Kiswahili. Kulikuwa na haja ya kufanya utafiti wa kina kuhusu nafasi na

mahali kama kipengele cha usimulizi kwa sababu kipengele hiki ni muhimu katika kukuza simulizi. Utafiti wetu basi ulinuia kukibainisha kipenge hiki kikamilifu.

Diwani teule katika utafiti wetu ilikuwa *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* ambayo ilichapishwa na shirika la uchapishaji la Focus kwa mara ya kwanza mnamo mwaka wa 2007. Diwani hii ina mkusanyiko wa hadithi fupi kumi na mbili zilizoandikwa na waandishi tofauti. Hadithi zinazoiunda diwani hii ni pamoja na: "Vinyago vya Watalii" (Sospeter Shake), "Njozi ya Mtu Mweupe" (Mwenda Mbatia), "Mioyo ya Chuma" (Macharia Mwangi), "Usaliti" (Prisca Jerono), "Shetani Hana Hatia" (Bitugi Matundura), "Kurudi Nyumbani" (Mwenda Mbatia), "Peremende" (Hanah Mwaliwa), "Mihuri ya Majanga" (J.W. Nyonje), "Kaburi la Siri" (Mari-Djata Amadi), "Tumbombele Mla Misitu" (John Kobia) "Safari ya Maangamizi" (Julius Gichamba) na "Njia ya Mwongo" (Prisca Jerono).

Hadithi fupi za diwani teule zinatofautiana katika kiwango cha ufupi. Kwa kutumia kigezo cha idadi ya kurasa zilizotumika katika kila hadithi, diwani hii ina makundi matatu ya hadithi. Kuna haditi fupi, za urefu wa wastani na hadithi ndefu. Hadithi zilizo fupi ni: "Mioyo ya Chuma" (Macharia Mwangi) yenye kurasa nne, "Usaliti" (Prisca Jerono) yenye kurasa tisa na "Peremende" (Hanah Mwaliwa) yenye kurasa tisa. Hadithi za urefu wa wastani ni: "Vinyago vya Watalii" (Sospeter Shake) yenye kurasa kumi na nne, "Njia ya Mwongo" (Prisca Jerono) yenye kurasa kumi na tano. "Njozi ya Mtu Mweupe" (Mwenda

Mbatia) yenye kurasa kumi na mmoja, “Shetani Hana Hatia” (Bitugi Matundura) yenye kurasa kumi na mmoja, na “Mihuri ya Majanga” (J.W. Nyonje) yenye kurasa kumi na mmoja.

Vilevile kuna kundi la hadithi ambazo ni ndefu zikilingashwa na zile za awali. Hadithi hizi ni: “Kaburi la Siri” (Mari-Djata A.K.A.) yenye kurasa kumi na saba, “Tumbombele Mla Misitu” (John Kobia) yenye kurasa kumi na saba na “Safari ya Maangamizi” (Julias Gichamba) yenye kurasa kumi na saba. Hatimaye kuna hadithi moja ambayo ni ndefu zaidi kwa kuwa ina kurasa thelathini na nne. Hadithi hii inaitwa “Kurudi Nyumbani” ya Mwenda Mbatia.

Hadithi fupi kama zilivyo tanzu nyingine za fasihi, hushughulikia masuala yanayohusu maisha ya wanajamii. Diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* imeyashughulikia masuala haya na kuyabainisha kupitia kwa maudhui mbalimbali. Masuala yanayomulikwa ni kama vile mgongano baina ya uhifadhina na msukumo wa mabadiliko, manufaa ya urafiki wa kweli, mvutano baina ya uadilifu na uhitaji na mengineyo.

Buchholz na Jahn (2005) wanaeleza dhana ya nafasi kama mazingira wanamoishi wahusika wa hadithi na yale yanayowazunguka. Kwa mujibu wa wataalamu hawa, nafasi ni mazingira halisi ambamo wahusika huishi na kutendea matendo yao.

Ronen (1986) anasema kuwa mazingira ya wahusika yanaweza kuelezewa zaidi kama mandhari, dhana ambayo ikipanuliwa zaidi hutofautisha kati ya

eneo halisi la matukio na ulimwengu mzima wa wahusika. Katika masimulizi pana mpaka kati ya eneo mahususi ambamo matukio hutukia na nafasi nzima inayoweza kuhusishwa na matukio hayo.

De Jong (2012) anasema kuwa nafasi ya hadithi hujumuisha mandhari ya matukio ya hadithi, nyanda zilizotajwa kupitia kwa kumbukumbu au ndoto na vifaa au vyombo vyote vinavyopatikana katika hadithi.

Mahali ni nafasi iliyopewa maana na wanajamii kutokana na ufahamu wao na uzoefu wao kuhusiana na nafasi hiyo. Mahali hufafanuliwa kwa kiwango ambacho wanajamii hupatia eneo fulani maana. Maana hizi hutolewa kufuatia vigezo viwili ambavyo kwa upande mmoja kuna njia ya moja kwa moja kama vile, kupitia hisia za kuona, kunusa, kuhisi na kusikia. Kwa upande mwingine, kuna njia isiyo ya moja kwa moja inayohusiana na maana zinazotokana na ishara au sanaa. (Tuan, 1977).

Monster (2009) anasema kwamba mahali ni dhana badilifu ambayo hujengwa na kujengwa upya mara kwa mara. Mahali pana uwezo mkubwa katika fasihi hasa katika ulimwengu wa kisasa wa utandawazi. Ni kitu tunachotangamana nacho na kukipa maana.

## 1.2 Suala la Utafiti

Watafiti wa awali katika hadithi fupi ya Kiswahili wameshughulikia vipengele mbalimbali vya simulizi vikiwemo; lugha, maudhui, msuko na wahusika. Hata

hivyo, kando na vipengele vilivyotafitiwa awali, hadithi huundwa kwa kipengele cha nafasi na mahali ambacho kwa mujibu wa Fludernik (1996), ni muhimu sana kwani huwasitiri wahusika wa hadithi na kuwapa uwanja wa kutendea matendo yao. Kwa mujibu wa De jong (2012), kipengele hiki kinaweza kuwa kimekuzwa kikamilifu katika hadithi ama kikashughulikiwa kwa ufinyu tu. Hata hivyo, kipengele cha nafasi kina dhima kuu katika kuijenga simulizi yeyote. Kulingana na ufahamu wa mtafiti, ilibainika kuwa kipengele hiki hakijatafitiwa. Utafiti huu basi ulilenga kutafiti kipengele cha nafasi na mahali katika hadithi fupi ya Kiswahili kwa kuchunguza aina za nafasi na mahali katika hadithi teule, jinsi kipengele cha nafasi na mahali kilivyowasilishwa katika hadithi na kubainsha umuhimu wa nafasi na mahali katika ujenzi wa hadithi fupi ya Kiswahili kwa kuchambua hadithi fupi sita za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti wetu yalikuwa:

1. Kubainisha vipengele vya nafasi na mahali ambavyo vinapatikana katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*.
2. Kuonyesha jinsi kipengele cha nafasi na mahali kilivyowasilishwa katika hadithi fupi mbalimbali za diwani teule.
3. Kubainisha umuhimu wa nafasi na mahali katika ujenzi wa maudhui na wahusika wa hadithi fupi katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi nyingine*.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

1. Je, ni vipengele gani vya nafasi na mahali ambavyo vinapatikana katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*?

2. Je, kipengele cha nafasi na mahali kimewasilishwa vipi katika hadithi za diwani teule?

3. Je, kipengele cha nafasi na mahali kina umuhimu gani katika ujenzi wa maudhui na wahusika kwenye hadithi fupi zilizoteuliwa katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*?

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Ari ya kushughulikia utafiti kuhusu nafasi na mahali katika hadithi fupi ilichochewa na sababu mbalimbali. Sababu ya kwanza ya kuchagua mada yetu ni kutambua kuwa nafasi na mahali ni kipengele kikuu cha usimulizi katika ujenzi wa simulizi yoyote ile.

Carteau (1984) anasema kwamba hadithi huundwa kwa ukinzani wa mitagusano katika nafasi. Nafasi ni viungo katika shughuli ya ujenzi wa hadithi ambayo hufanyika kila siku. Anaendelea kusema kuwa hadithi yoyote ina motifu ya safari ambayo hufanyika katika nafasi, hivyo hadithi ina muundo wenye njia za nafasi ambazo huunganisha sehemu moja na nyingine na kuzalisha simulizi.

Moretti (1998) anaeleza kuwa nafasi sio chombo ajizi cha kuendesha matukio ya kitamaduni ila ni nguvu inayoenea katika uwanja mzima wa usimulizi na

kuunda uwanja huo kwa kina. Kwa mujibu wa mtaalam huyu, nafasi sio zao la usimuliaji bali ni chanzo au kiini cha usimuliaji.

Grossberg (1996) anaeleza kuwa kipengele cha nafasi kina hadhi sawa na cha wakati kwa sababu kina jukumu la kuzalisha simulizi. Anaendelea kueleza kuwa nafasi ni suala la mwelekeo wala sio la kihistoria na kwa mtazamo huu basi, nafasi huchukua sehemu yake kama kipengele kikuu cha ujenzi wa hadithi sawa na wakati ila sio kipengele kinachotawaliwa na wakati katika simulizi. Kulingana naye, nafasi sio uwanja tuli, batili na tupu wa kutukia kwa matukio na kuaathiriwa na mpito wa wakati, bali ni kipengele hai, tendi na kamili kinachojenga simulizi. Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, ni bayana kuwa kipengele cha nafasi na mahali kina sehemu kubwa katika ujenzi wa hadithi. Mawazo haya basi yalimpa mtafiti motisha wa kukibainisha na kukifafanua kipengele hiki ili kieleweke vyema na waandishi, wasomi na watafiti wa fasihi ya Kiswahili.

Sababu ya pili ni kuwa, kwa mujibu wa De Jong (2012), kipengele cha nafasi na mahali hakijapewa uzito kinadharia japo ni kipengele muhimu katika ujenzi wa hadithi. Anaendelea kusema kuwa wananaratolojia wanakubaliana kuwa kipengele hiki kimepuuzwa kwa sababu ya kauli ya Buchholz na Jahn (2005) kuwa simulizi ni sanaa ya wakati wala sio ya mahali, hivyo, wanadai kuwa nafasi ni kipengele wazi au bayana sana ambacho hakina haja ya kuchunguzwa. Katika uchunguzi wetu wa kimsingi, ilibainika kuwa utafiti kuhusu nafasi na mahali katika fasihi ya Kiswahili pia ulikuwa umepuuzwa. Hata hivyo, ilibainika kuwa kipengele hiki kina dhima kuu katika simulizi

hivyo ni muhimu kufanyiwa utafiti. Kwa msingi huu basi, mtafiti alitaka kukifanyia utafiti na kukiweka wazi kitaaluma ili kieleweke bayana na kuchangia kukitilia mkazo katika fasihi ya Kiswahili.

Sababu ya tatu ni kutokana na madai ya Zoran (1984). Anasema kuwa nafasi ni mfumo changamano katika hadithi, ila ni sehemu ndogo tu ambayo hufafanuliwa katika hadithi. Maoni haya yanaafikiana na ya De Jong (2012), anayesema kuwa kipengele cha nafasi hakiwezi kuwasilishwa kikamilifu hata kikishughulikiwa katika upana au ufinyu wake. Kwa sababu hii pana umuhimu ya kukichanganua kipengele kwa kunyesha vijenzi vyake ili kieleweke vyema na wasomi na watafiti wa fasihi ya Kiswahili. Mtafiti basi alivutiwa na madai haya na kuona haja ya kukifanyia kipengele hiki utafiti ile kieleweke na hatimaye kuwafaa waandishi, wasomi na watafiti wa fasihi ya Kiswahili.

Mtafiti pia alivutiwa na utambuzi kuwa fafanuzi au vielezo vipatikanavyo katika hadithi ni sehemu ya nafasi. Hata hivyo, aligundua kuwa sehemu hii ya nafasi haikuwa imetafitiwa na kufafanuliwa na watafiti wa awali. Fludernik (2009) anasema kuwa fafanuzi ni njia mojawapo ya kuyapa sifa mandhari ya hadithi na kurutubisha mahali katika hadithi. Mtafiti alitaka kuthibitisha madai haya kupitia utafiti wake.

Diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* ilichaguliwa kwa sababu ni mojawapo ya kazi za hadithi fupi za awali tangu utanzu wa hadithi fupi ulipoanza kushughulikiwa kwa kina. Diwani hii pia imevutia makini ya

watafiti tofauti ambao wameifanyia utafiti ila haijachambuliwa kwa mtazamo wetu. Mtafit alitaka kuendeleza utafiti wa hadithi za diwani hii kwa kuchunguza vipengele ambavyo havikuwa vimeshughulikiwa. Hii ni kwa sababu diwani hii ilikuwa miongoni mwa diwani za kwanza zilizochangia pakubwa katika kuukuza utanzu wa hadithi fupi ya Kiswahili.

Mbatia (2007) anasema kuwa diwani hii imekusanya kazi za waandishi waliokomaa na waandishi chipukizi lakini walio na kipawa cha uandishi. Mtafiti basi alikuwa na mshawasha wa kufanyia utafiti hadithi za waandishi tofauti kitajriba na kuchunguza jinsi walivyokishughulikia kipengele cha nafasi katika kazi zao.

Isitoshe, utanzu wa hadithi fupi haujafanyiwa tafiti za kutosha katika fasihi ya Kiswahili kama anavyosema Nzong'a (2020), akimnukuu McOnyango (2006). Kwa sababu hii, mtafiti alipata ari ya kuchangia katika kuuendeleza utanzu huu kwa kuufanyia utafiti.

Mwisho, kulikuwa na haja ya kuthibitisha madai ya De Jong (2012) anayesema kwamba nafasi imechukua mtazamo wa kimapinduzi unaopanua dhima zaidi za nafasi katika simulizi, tofauti na ule mtazamo finyu wa awali uliochukulia nafasi kama uwanja wa matukio tu. Mtafiti alitaka kuyabainisha maendeleo haya kwa kubainisha aina za nafasi na mahali, jinsi kipengele cha nafasi na mahali kilivyowasilishwa katika hadithi fupi pamoja na kuonyesha majukumu zaidi yanayotekelezwa na nafasi katika hadithi fupi ya Kiswahili kwa kutumia

kielelezo cha diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Kwa njia hii, mtafiti angeweza kubainisha uhusiano na mwingiliano uliopo kati ya kipengele cha nafasi na mahali na vipengele vinginevyo vya fasihi vikiwemo wahusika, maudhui na mandhari katika hadithi fupi ya Kiswahili.

**1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti wetu ulichunguza kipengee cha nafasi na mahali katika hadithi fupi ya Kiswahili kwa kuichambua diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Mtafiti alichanganua maneno na kauli za msimulizi na wahusika katika hadithi husika. Aidha tulichunguza maudhui ya waandishi mbalimbali wa hadithi sita za diwani hii. Diwani hii ina mkusanyiko wa hadithi fupi kumi na mbili zilizoandikwa na waandishi tofauti. Hadithi zinazoiunda diwani hii ni pamoja na: "Vinyago vya Watalii" (Sospeter Shake), "Njozi ya Mtu Mweupe" (Mwenda Mbatia), "Mioyo ya Chuma" (Macharia Mwangi), "Usaliti" (Prisca Jerono), "Shetani Hana Hatia" (Bitugi Matundura), "Kurudi Nyumbani" (Mwenda Mbatia), "Peremende" (Hanah Mwaliwa), "Mihuri ya Majanga" (J.W. Nyonje), "Kaburi la Siri" (Mari-Djata Amadi), "Tumbombele Mla Misitu" (John Kobia) "Safari ya Maangamizi" (Julius Gichamba) na "Njia ya Mwongo" (Prisca Jerono). Hadithi sita zilizochambuliwa ni: *Vinyago vya Watalii, Mioyo ya Chuma, Usaliti, Kurudi Nyumbani, Mihuri ya Majanga* na *Safari ya Maangamizi.*

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya naratolojia, mkondo wa De Jong (2012). Mihimili ya nadharia iliyotumika katika utafiti wetu ni: Nafasi ya

hadithi, nafasi ya msimulizi, mandhari na fremu na vielezo. Utafiti ulichunguza aina za nafasi na mahali zinazopatikana katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, jinsi kipengele cha nafasi na mahali kinavyowasilishwa na waandishi wa hadithi fupi sita za diwani teule na umuhimu wa nafasi na mahali katika ujenzi wa maudhui na wahusika wa hadithi zilizoteuliwa kwenye mkusanyiko wa hadithi za *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Ingawa mkondo wa De Jong (2012) ndio uliotumika kuchanganua data ya utafiti wetu, mawazo ya wananadharia wengine yalitumika katika ufafanuzi wa nadharia.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Kuna kazi mbalimbali za kiusomi zilizoandikwa kuhusiana na mada yetu ya utafiti. Baadhi ya kazi hizi ni za wataalamu katika uwanja wa nafasi na mahali na nyingine ni za watafiti katika fasihi ya Kiswahili.

Mbuthia (2003) alifanya utafiti kuhusu jinsi hadithi fupi za Kiswahili zilivyoshughulikia kipengele cha mtindo na maudhui. Katika utafiti wake alieleza kuwa utanzu wa hadithi fupi una uwezo wa kushughulikia maswala yote ya jamii. Aidha utafiti wake ulidhihirisha kuwa utanzu wa hadithi fupi una sifa za kipekee zinazotokana na tanzu zake tangulizi, hivyo kuupa utanzu huu sifa za kiusimulizi na za kiuandishi. Anaendelea kusema kuwa maadili ya hadithi fupi yanaibuka kuwa muhimu kuliko uhalisia utokanao na mtazamo wa msomaji. Kazi hii ni tofauti na yetu kwa vile ilichunguza mtindo na maudhui katika hadithi fupi ilhali utafiti wetu ulichunguza nafasi na mahali katika

hadithi fupi ya Kiswahili. Hata hivyo utafiti huu ulitufaa katika sehemu ya kuelezea historia ya hadithi fupi ya Kiswahili.

Ntiba (2011) alifanya utafiti kuhusu namna uteuzi wa mtindo katika hadithi fupi ya Kiswahili unavyoathiriwa na dhamira. Uchunguzi wake ulihusisha diwani za *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, *Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine* na *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, diwani zote zikiwa za mwaka wa 2007. Utafiti wake ulionyesha jinsi uteuzi wa mitindo ya waandishi wa vitabu teule ulivyoathiriwa na dhamira za kazi zao. Utafiti huu uliainisha masuala muhimu yaliyoangaziwa na wandishi wa mwaka wa elfu mbili na mia saba. Aidha alichunguza athari ya mazingira kwa utunzi wa watunzi hao. Utafiti wake uliongozwa na nadharia iliyounganisha mihimili kadha ya nadharia ya uchanganuzi saikolojia na kadha ya nadharia ya mtindo. Utafiti wake unatofautiana na wetu kwa maana yeye ulichunguza masuala mahususi yaliyoshughulikiwa na waandishi mbalimbali wa hadithi fupi katika diwani teule ilhali utafiti wetu ulishughulikia nafasi na mahali kama kipengele muhimu cha ujenzi wa hadithi. Utafiti huu ulitufaa kwa kueleza maudhui yaliyoshughulikiwa na waandishi wa hadithi mbalimbali za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* hivyo kutuwezesha kuonyesha jinsi maudhui hayo yanaathiriwa na nafasi na mahali.

Kaui (2015) alitathmini namna riwaya na hadithi fupi za Kiswahili zinavyosimilishwa kwa ajili ya wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya. Ali ifafanua dhana ya usimilishaji, akaeleza historia ya usimilishaji, akaonyesha

mbinu za kusimilisha na matatizo ya usimilishaji. Aidha, utafiti wake ulidokeza njia mbalimbali za kutatua matatizo ya usimilishaji. Utafiti wake ulijumuisha mihimili ya nadharia ya usimilisho na ile ya nadharia ya uigizaji. Kazi hii inatofautiana na yetu kwa kuwa ilichunguza suala la usimilisho ilhali utafiti wetu ulichunguza kipengele cha nafasi na mahali katika hadithi fupi ya Kiswahili. Utafiti huu haukutumika katika utafiti wetu.

Arege (2012) alishughulikia Utenzi wa Rasi’l Ghuli na kufanya utafiti kuhusu usimulizi kwa kuongozwa na nadharia ya usimulizi. Utafiti huu ulichunguza vipengele vya daraja na sauti za usimulizi, wahusika na wakati. Uchunguzi huu ulibainisha kwamba mfuatano wa matukio katika utenzi wa Rasi’lGhuli sio wa moja kwa moja, bali mtindo wa urudiaji ulitumika kwa wingi. Isitoshe, ulieleza kuwa misimamo ya kiitikadi inaathiri tabia za wahusika. Aidha, ilibainika kuwa utenzi wa Rasi’lGhuli una daraja nyingi za usimulizi na sauti za wasimulizi kadhaa. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwa sababu ulichunguza vipengele tofauti vya usimulizi bali sio kipengele cha nafasi na mahali katika simulizi. Pia, utafiti wake haukutumia mkondo wa De Jong wa nadharia ya naratolojia. Isitoshe, utafiti huu ulitafiti utanzu wa ushairi lakini utafiti wetu ulichunguza utanzu wa hadithi fupi ya Kiswahili. Utafiti huu ulitumika katika utafiti wetu kueleza mikondo na maendeleo ya nadharia ya naratolojia.

Kyalo (2012) alichambua diwani ya *Pendo la Heba na Hadithi Nyingine* na diwani ya *Mizungu ya Manabii na Hadithi Nyingine* huku akingozwa na nadharia ya Finominolojia. Utafiti huu ulichunguza kipengee cha mandhari

kwa kutumia mtazamo linganishi. Utafiti huu ulibainisha kuwa waandishi mbalimbali wa hadithi fupi husawiri mandhari yaliyojikita katika eneo moja, hivyo, mandhari hayabadiliki. Mandhari yaliyopatikana katika utafiti huu ni ya kihistoria, kijiografia, kihisia na kisaikolojia. Utafiti wake pia ulionyesha mbinu mbalimbali za lugha zinazotumiwa kuwasilisha mandhari. Isitoshe, alionyesha kuwa matumizi ya lugha katika kusawiri mandhari yanatofautiana kutoka mwandishi mmoja hadi mwingine. Katika kazi yake pia amedokeza vipengele vingine vya hadithi fupi kama vile; muundo na umbo, dhamira na mtindo. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa kuwa ulitumia nadharia ya finominolojia ilhali utafiti wetu ulitumia nadharia ya naratolojia. Isitoshe, utafiti huu ulichunguza mandhari kwa kutumia mtindo linganishi ambao haukutumika katika utafiti wetu. Aidha mtafiti alichunguza jinsi waandishi wanavyosawiri mandhari kwa kutumia mbinu za lugha na kutumia mtazamo wa kale uliochukulia mandhari kama uwanja wa matukio tu. Kwa upande wa utafiti wetu, tulichunguza mandhari kama kiungo kijenzi cha nafasi na mahali na kuonyesha majukumu zaidi yanayotekelezwa na kipengele cha nafasi na mahali. Aidha, tulitumia mtindo wa kimapinduzi kulishughulikia suala la nafasi na mahali. Kazi hii ilikuwa ya manufaa kwetu kwani ilichangia kutoa maelezo ya mandhari kama kipengele cha nafasi na mahali.

Chemtai (2016) alichunguza kipengele cha mtindo katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili. Aliangazia dhamira, maudhui, mandhari, mtindo, wahusika na muundo, kama vijenzi vya hadithi fupi za Kiswahili za kisasa. Katika ufafanuzi wake, anasema kuwa mandhari ni mazingira ambayo hadithi inaandikiwa.

Anasema kuwa, chanzo cha umuhimu wa kudadisi mazingira katika uchambuzi wa fasihi ni kutambua kwamba, kila jambo hufanyikia mahali maalum. Kwa msingi huu, kipengee hiki hukamilishana na vipengee vingine katika hadithi fupi. Anatambua dhima ya mandhari katika fasihi na kupendekeza kuwa mandhari yaelezwe kwa kina zaidi. Anakiri kuwa tunapoeleza mandhari hatuna budi kuchunguza mtindo kwa maana unatumika kuyachora.

Fauka ya hayo, anasema kuwa mandhari huathiri jinsi mwandishi anavyoandika kazi yake, kwa maana mandhari huchorwa kwa kutumia lugha yenye mvuto. Utafiti huu ulitufaa kwa kuwa unaeleza kipengele mojawapo cha nafasi na mahali ambacho ni mandhari, hivyo kazi hii iliuwekea utafiti wetu msingi kwa kufafanua dhana ya mandhari na kuonyesha jinsi mandhari yanavyoziathiri hadithi fupi. Tofauti kati ya utafiti huu na wetu ni kuwa, utafiti wake ulichunguza mandhari kama kipengele cha mtindo katika hadithi fupi ila utafiti wetu ulikishughulikia kipengee cha nafasi na mahali huku mandhari yakisawiriwa kama sehemu ndogo ya kipengele hiki cha usimulizi.

Hussein (2018) alifanya uchanganuzi wa maudhui ya siasa na jinsi yanavyodhihirika katika hadithi fupi ya *Kikaza* iliyoandikwa na Oduori na *Uteuzi wa Moyoni* iliyoandikwa na Timammy. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Katika utafiti wake, alichanganua mbinu za sanaa zilizotumiwa na watunzi wa hadithi hizi ili kujenga maudhui ya siasa. Utafiti wake pia ulibainisha namna siasa zinavyoathiri maendeleo ya jamii. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwa kuwa ulitumia nadharia ya uhalisia ilhali wetu

ulitumia nadharia ya naratolojia. Pia, utafiti wake ulichunguza maudhui ya siasa na mbinu za sanaa zinazotumiwa kuwasilisha maudhui hayo katika hadithi fupi tuele ambazo ni tofauti na zetu. Isitoshe, utafiti wetu ulichunguza kipengele cha nafasi na mahali katika diwani tofauti na yake. Uchunguzi huu haukuchangia katika utafiti wetu.

Nzong'a (2020) alichunguza namna wanaume wanavyopewa majukumu mapya katika hadithi fupi ya Kiswahili. Nadharia ya upembuzi na nadharia ya uana ziliongoza utafiti huu ambao ulichambua diwani tatu tofauti. Utafiti huu ulibainisha namna jinsia ya kiume inavyogawiwa majukumu upya, sifa za wanaume zinazotokana na mgao huo na jinsi wanaume wanavyoathirika kwa kupokea majukumu mapya. Utafiti huu unahitilafiana na wetu kwa kuwa uchunguzi wetu ulihusu kipengele cha nafasi na mahali katika hadithi fupi ya Kiswahili. Utafiti huu ulitufaa katika usuli wa hadithi fupi ya Kiswahili.

Misoi (2022) alitafiti kuhusu dhima ya usimulizi katika nyimbo za taarab zenye asili katika pwani ya Afrika Mashariki. Utafiti huu ulibainisha kuwa usimulizi umekuza mbinu za uandishi, wahusika na ploti katika uwasilishaji wa nyimbo za taarab zilizofanyiwa utafiti. Mbinu ya urudiaji imekuzwa na kipengele cha wakati kupitia kwa aina ya idadi marudio, ambapo tukio lililotendeka mara moja, linasimuliwa zaidi ya mara moja. Kupitia kwa aina ya mpangilio, kipengele cha wakati kimekuza mbinu ya kisengere mbele, kisengere nyuma, dayalojia na majazi. Utafiti huu ulitofautiana na wetu kwa vile alitafiti kuhusu nyimbo za taarab na ingawa ulitumia nadharia ya

naratolojia, mkondo na mihili iliyotumiwa ni tofauti na tuliyoitumia. Aidha utafiti wake ulihusu dhima ya usimulizi katika nyimbo za taarabu ilhali wetu ulihusu kipengele cha nafasi na mahali katika hadithi fupi ya Kiswahili. Utafiti huu ulitusaidia kufafanua nadharia ya naratolojia.

De Jong (2012) anasema kuwa, kipengele cha nafasi na mahali kina dhima kuu katika usimuliaji wa hadithi. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, kuna tofauti kubwa katika jinsi waandishi tofauti wa hadithi huangazia kipengele cha nafasi. Baadhi yao hutunga au hubuni hadithi zenye wingi wa nafasi au zenye nafasi tele huku wengine wakibuni hadithi zenye nafasi haba au finyu. Hata hivyo, anaendelea kusema kuwa, wananaratolojia wanakubaliana kwamba kipengele cha nafasi hakiwezi kushugulikiwa kikamilifu ila wasimuliwa hupewa maelezo yaliyochujwa na kuteuliwa kwa makini na mwandishi.

Kulingana na utafiti wetu, hali iliyokuwepo ni kuwa tafiti zilizofanywa awali hazikushughulikia kipengele cha nafasi na mahali kwa undani. Kipengele cha mandhari, ambacho ni mojawapo ya viambajengo vya nafasi na mahali ndicho tu kilichotafitiwa. Kwa sababu hii, ilibainika kuwa kulikuwa na haja ya kufanya uchunguzi wa kina kuhusu nafasi na mahali kama kipengele muhimu cha usimulizi katika fasihi ya Kiswahili. Utafiti wetu ulinuia kukichanganua kipengele cha nafasi na mahali kwa kuonyesha vipengele vyake na uwasilishaji wake katika hadithi fupi teule za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* na kuonyesha dhima yake katika ujenzi wa maudhui na wahusika wa hadithi zilizoteuliwa za *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine.*

## 1.8 Msingi wa Nadharia

Bryman (2016), nadharia ni namna ya kuangazia jambo kitaaluma. Ni kompasi ya kumpa mchunguzi maelekezo ya kulizingatia suala la utafiti wake. Sawa na jinsi kompasi inavyomwelekeza msafiri kupata njia, ndivyo nadharia inavyomwongoza mtafiti kuelewa na kueleza anachofanyia utafiti.

TUKI (2004), nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani.

Wafula na Njogu (2007) wanaeleza kuwa nadharia ni maelekezo yote yanayomwezesha msomaji au mhakiki kuielewa kazi ya fasihi kwa kuzingatia utaratibu maalum. Wanaendelea kusema kwamba istilahi hii ni ya kijumla na hutumika kurejelea mwongozo unaompa msomaji wa kazi ya fasihi mwelekeo ili kupata ufahamu bora wa kazi hiyo katika vipengee tofauti tofauti vya kazi ya fasihi, ambavyo hujumuika na kuleta wiano kwenye kazi hiyo. Kwa misingi ya maoni ya wataalamu hawa basi, utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya naratolojia ili kumpa mtafiti maelekezo na kuongoza utafiti wake.

### 1.8.1 Nadharia ya Naratolojia

Gholami (2013) anasema kwamba Plato ndiye anayehusishwa na chanzo cha wazo la naratorojia. Mwanafalsafa huyu wa kiyunani aliibua wazo hili katika andiko lake la tatu liitwalo "The Republic" la mwaka wa 1930. Plato alitumia istilahi digesia na mimesia kurejelea dhana ya tendo la kusimulia na tendo la kudhihirisha mtawalia. Mwanafalsafa huyu alieleza kuwa digesia ina maana ya usimulizi unaowasilishwa kwa hadhira kupitia kwa msimulizi ilhali mimesia ni

uonyeshaji usiomhusisha msimulizi, hivyo, msimulizi hajitokezi wazi bali huwa amefichika.

Misoi (2022, akimnukuu Prince 1982) anasema kuwa nadharia ya naratolojia inashughulikia jinsi ya kusimulia hadithi. Kwa vile nadharia ya usimulizi inahusika na shughuli ya kusimulia, mwananaratolojia hana budi kuzingatia kwa kina kile kinachosimuliwa na kile ambacho hakikusimuliwa. Aidha, anapaswa kuchunguza jinsi matukio yalivyosimuliwa na mafanikio ya mbinu zilizotumika kusimulia.

Gholami (2013) anasema kuwa Todorov ndiye aliyebuni neno “narratology” linalotafsiriwa kuwa usimulizi. Alilitumia kwa mara ya kwanza katika kitabu chake cha *The Grammar of Decameron*. (1969). Todorov na waasisi wenzake Barthes wa awali na Greimas walikuwa katika mchakato wa kubuni kanuni ambazo zingetumiwa kuainisha simulizi katika aina mbalimbali kwa kuwa walishughulikia uainishaji wa hadithi pekee. Kipindi hiki kilikuwa cha urasimi mkongwe ambapo nadharia ya naratolojia ilichukuliwa kuwa utanzu wa nadharia ya umuundo. Mtazamo wa waasisi hawa ulitiliwa shaka na kuchochea kuibuka kwa kikundi kiingine cha wananaratolojia wa urasimi mkongwe ambao ni Stanzel, Genette na Chatman. Wananaratolojia hawa hawakuweka kanuni za kijumla kwa simulizi zote ila walibuni aina mbalimbali za simulizi ambazo zilifafanuliwa na kutolewa mifano mahususi.

Baadaye nadharia ya naratolojia iliingia kipindi cha urasimi ambacho kilihusishwa na Bal na Rimmon-Kenan. Arege (2012, akimnukuu Rimmon-Kenan 2003) anasema kuwa nadharia ya naratolojia imeimalika na kujitegemea na hata kutumika katika uchanganuzi wa tafiti nyingi za aina mbalimbali za simulizi zikiwemo hadithi fupi, riwaya na ushairi.

Gholami (2013) anaendelea kusema kuwa katika kipindi cha usasa nadharia ya naratolojia ilihusishwa na Gibson, Currie na O'Neill. Katika kipindi hiki nadharia ya naratolojia ilichukua mikondo tofauti kama vile mkondo wa naratolojia tambuzi unaohusishwa na Herman na kuendelezwa na wataalamu kama Palmer na Zunshine. Hata hivyo, baadhi ya watalamu kama Phelan walitumia mihimili ya naratolojia ya urasimi na kuongezea mihimili mingine ya mwandishi halisi, msomaji halisi na maadili ya uandishi na usomaji.

Mkondo wa nadharia ya naratolojia uliotumiwa katika utafiti wetu ni wa De Jong (2012), ambaye anasema kuwa, kipengele cha nafasi na mahali kina dhima kuu katika usimuliaji wa hadithi.  Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, kuna tofauti kubwa katika jinsi waandishi tofauti wa hadithi huangazia kipengele cha nafasi. Baadhi yao hutunga au hubuni hadithi zilizojaa mandhari au zenye wingi wa mandhari huku wengine wakibuni hadithi zenye uchache wa mandhari. Hata hivyo, anaendelea kusema kuwa, wananaratolojia wanakubaliana kwamba kipengele cha nafasi hakiwezi kushugulikiwa kikamilifu ila wasimuliwa hupewa maelezo yaliyochaguliwa na kuteuliwa kwa makini na mwandishi.

### 1.8.2 Vipengele vya Nafasi na Mahali

De Jong (2012) anapendekeza mihimili ifuatayo itumike katika chambuzi wa nafasi na mahali kama kipengele cha usimulizi:

1. Nafasi ya msimulizi
2. Nafasi ya hadithi / simulizi ambayo ina mandhari na fremu
3. Vielezo

#### 1.8.2.1 Nafasi ya msimulizi

De jong (2012) anasema kuwa msimulizi husimulia nafasi yake mwenyewe. Nafasi ya msimulizi inaweza kuwa sawa na nafasi ya hadithi au ikawa tofauti kabisa. Msimulizi anaweza kubainisha aliko anapotanguliza usimulizi wake au adhihirishe kuwa nafasi ya hadithi inapatikana katika wakati sawa na ule wa msimulizi.

Utafiti wetu ulijikita kwenye mtazamo huu. Mhimili huu ulitumika kubainisha vipengele vya nafasi na mahali vinavyopatikana katika hadithi fupi za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*.

#### 1.8.2.2 Nafasi ya simulizi/hadithi

Kwa mujibu wa De jong (2012), nafasi ya hadithi ni jumla ya mandhari ya matukio, maeneo yanayotokea mawazoni, ndotoni na katika kumbukumbu pamoja na vifaa katika hadithi. Nafasi ya hadithi humhitaji msomaji/msimuliwa tendi ambaye anaweza kuhusisha mahali na nafasi fulani na maana ama dhana fulani. Anasema kwamba tunaweza kupambanua kati ya nafasi ya fabula na nafasi ya hadithi. Kulingana naye, nafasi ya fabula ni nafasi

kamili ambayo inaizungukia hadithi husika, ilhali nafasi ya hadithi ni nafasi mahususi kama inavyowasilishwa na msimulizi katika hadithi yake. Anaendelea kusema kuwa, mijadala kuhusu nafasi katika hadithi mara nyingi hujikita katika nafasi ya hadithi.  Aidha, anasema kuwa katika uchunguzi wa nafasi ya hadithi pana haja ya kutofautisha kati ya mandhari na fremu. Vipengee hivi vya nafasi ya hadithi vinafafanuliwa ifuatavyo.

**1.8.2.2.1 Mandhari**

Buchholz na Jahn (2005) wanasema kuwa mandhari ni jumla ya mazingira ya kijamii, kihistoria na kijografia, ambamo matendo hutendeka katika hadithi. Mazingira haya huhusishwa na hadithi nzima.

Kwa mujibu wa De jong (2012) mandhari ni mahali mahususi ambapo matukio ya hadithi hutukia. Madhari hubadilikabadilika katika hadithi hivi kwamba matukio ya hadithi hayafanyiki katika sehemu moja bali katika sehemu au mahali mbalimbali.

**1.8.2.2.2 Fremu**

Ronen (1986) anasema kuwa fremu ni mahali pa kufikirika ambapo hutokea kwenye mawazo, ndoto na kumbukumbu.

De jong anaeleza kuwa fremu ni maeneo ambayo hutokea katika mawazo, ndoto na kumbukumbu. Anasema kwamba fremu huibua mawanda ya mbali yasiyofikika au kueleweka, tena yasiyo halisi na ambayo hupanua nafasi ya hadithi kwa njia mbalimbali.

Mhimili huu ulitumika kuonyesha namna kipengele cha nafasi na mahali kilivyowasilishwa katika hadithi fupi teule za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Pia ulitumika kuonyesha umuhimu wa nafasi katika kujenga maudhui na wahusika wa hadithi teule.

#### 1.8.2.3 Vielezo

De jong (2012) anaeleza kuwa vielezo ni maelezo ya kina kuhusu mahali, vitu, watu na matukio. Maelezo haya hutokea katika hali tulivu ambayo haina mpito wa wakati, tofauti na ilivyo katika hadithi. Maelezo haya huwa na mpangilio kimuundo ambao hutofautiana na mpangilio wa hadithi ambao ni wa kimantiki. Kipengele hiki kilitumika kuonyesha jinsi nafasi na mahali huwasilishwa katika hadithi na kubainisha umuhimu wa nafasi na mahali katika ujenzi wa maudhui na wahusika wa hadithi fupi zilizoteuliwa.

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Kothari (2014) anaeleza kuwa ili kupata matokeo ya kuaminika, uchunguzi wa kitaaluma sharti uongozwe na mbinu kadhaa za utafiti. Kwa sababu hii, utafiti wetu ulizingatia mbinu mbalimbali za uchunguzi.

### 1.9.1 Muundo wa Utafiti

Mugenda na Mugenda (2003) wanasema kuwa muundo wa utafiti ni mpango unaobainisha vipengele muhimu vya kazi inayotarajiwa kufanywa katika utafiti mzima.

Utafiti wa kimaelezo ndio muundo tulioutumia katika utafiti wetu. Creswell (2012) anasema kuwa, muundo wa kimaelezo ni ule unaotoa ripoti ya jinsi

mambo yalivyo katika mazingira fulani. Mtafiti hukusanya data, huichunguza kuichanganua na kutoa maelezo na fafanuzi mwafaka kulingana na matokeo aliyoyapata. Mtafiti alikusanya data kwa kuchambua maneno, vishazi na sentensi katika hadithi teule za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine.* Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kisha data hiyo ikawasilishwa kwa njia ya kimaelezo.

### 1.9.2 Mahali pa Utafiti

Uchunguzi wetu ulifanyika kwenye maktaba ya idara ya Kiswahili chuoni Kenyatta, maktaba kuu ya chuo na maktaba ya umma mjini Murang'a. Mtafiti alisoma diwani teule, vitabu na tasnifu mbalimbali kwa makini pamoja na makala mengine muhimu kwenye mtandao.

### 1.9.3 Uteuzi wa Sampuli

Hadithi sita za waandishi tofauti katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* zilichambuliwa. Sampuli hii iliteuliwa kimakusudi kwa kuwa hadithi hizi zina data muhimu zilizohitajika katika utafiti huu. Hadithi zilizoteuliwa kufanyiwa utafiti zilidhihirisha vipengele vya nafasi vikiwemo, nafasi ya hadithi, nafasi ya msimulizi, fremu na vielezo. Waandishi wa hadithi teule pia walionyesha mbinu mbalimbali za kuwasilisha nafasi na mahali na wakaonyesha umuhimu wa nafasi na mahali katika ujenzi wa maudhui na wahusika wa hadithi. Hadithi zifuatazo za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* zilichambuliwa:

1. Vinyago vya Watalii- (Sospeter Shake)

2. Mioyo ya Chuma- (Macharia Mwangi)
3. Njozi ya Mtu Mweupe- (Mwenda Mbatia)
4. Kurudi Nyumbani- (Mwenda Mbatia)
5. Mihuri ya Majanga- (J.W. Nyonje)
6. Safari ya Maangamizi- (Julius Gichamba)

Wamitila (2002) anasema kuwa hadithi fupi ni hadithi ambayo husimulia kwa ufupi na ambayo dhamira yake, mtindo, wahusika, maudhui na mandhari yake ni finyu. Pia anasema kuwa hadithi fupi zina maudhui finyu na hutumia muundo sahili wa uwasilishaji. Kwa sababu ya sifa hii ya ubanifu, hadithi sita za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* zilikosa data muhimu iliyohitajika katika utafiti wetu, hivyo, hazikuchambuliwa. Hadithi hizi zilitumia mandhari kama uwanja wa matukio tu na zilikosa nafasi ya msimulizi, fremu na vielezo. Kwa kukosa vipengele vilivyotajwa vya nafasi na mahali, hadithi hizi zilikosa mbinu mbalimbali za kuwasilisha nafasi na uhusiano kati ya nafasi na mahali na maudhui na wahusika wa hadithi.

Hadithi zifuatazo za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* hazikuchambuliwa.

1. Usaliti- (Prisca Jerono)
2. Shetani Hana Hatia- (Bitugi Matundura)
3. Peremende- (Hanah Mwalia)
4. Kaburi la Siri- (Mari-Djata Amadi Kwaa Atsiaya)
5. Tumbombele Mla Misitu- (John Kobia)
6. Njia ya Mwongo- (Prisca Jerono)

### 1.9.4 Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data ulifanyika kwa kusoma kwa kina hadithi sita teule katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Mtafiti alichunguza maneno, vishazi, sentensi na vifungu katika hadithi fupi sita katika diwani teule. Alisoma kwa undani na kuzihakiki kwa kuzingatia vipengele vya nafasi na mahali vinavyopatikana katika hadithi fupi teule, kuchunguza namna kipengele cha nafasi na mahali kilivyowailishwa na kuchunguza umuhimu wa nafasi na mahali katika ujenzi wa maudhui na wahusika mbalimbali wa hadithi teule za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya naratolojia inayohusiana na nafasi. Mtafiti alihakiki maneno, sentensi na kauli za wasimulizi, waandishi na wahusika katika hadithi teule kulingana na malengo ya utafiti. Mtafiti alichanganua maneno, kauli, vishazi na sentensi ili kubainisha jinsi waandishi mbalimbali walivyowasilisha nafasi na mahali katika kazi zao, vipengele vya nafasi na mahali vinavyobainika katika hadithi teule na mchango wa nafasi na mahali katika ujenzi wa wahusika na maudhui ya hadithi.

### 1.9.6 Uwasilishaji wa Data

Njia ya maelezo ilitumika kuwasilisha matokeo ya uchunguzi wetu. Maelezo yalitolewa kwa maandishi yaliyopangwa katika sura tano, huku mtafiti akiongozwa na malengo ya utafiti. Sura ya kwanza ilijumuisha sehemu za kimsingi za utafiti. Sura hii ilionyesha suala la utafiti, maswali ya utafiti,

malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti. Mbinu za utafiti zilijumuisha muundo, mahali, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data. Sura pili na ilijumuisha vipengele vya nafasi na mahali vinavyopatikana katika hadithi teule za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Sura ya tatu ilishughulikia jinsi kipengele cha nafasi na mahali kilivyowasilishwa katika diwani teule na sura ya nne ikaonyesha umuhimu wa nafasi na mahali katika ujenzi wa maudhui na wahusika wa hadithi fupi sita katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi nyingine.* Sura ya mwisho ilieleza matokeo ya uchunguzi, mchango wa utafiti, na kutoa mapendekezo na hitimisho.

### 1.9.7 Uzingativu wa Maadili

Mtafiti aliomba idhini ya kufanya uchunguzi kutoka kwa Chuo kikuu cha Kenyatta kabla ya utafiti kuanza, ili kuzingatia maadili ya utafiti. Aidha mtafiti aliomba kibali cha kufanya utafiti katika shirika la NACOSTI. Utafiti ulifanywa kwa kuongozwa na maadili ya uaminifu na uwazi. Mtafiti aliepuka wizi wa mawazo ya kazi za watafiti wengine kwa kuwanukuu katika utafiti wake.

## 1.10 Hitimisho

Sura hii ilishughulikia usuli wa mada, suala la utafiti malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti na yaliyoandikwa kuhusu mada. Aidha mtafiti alishughulikia msingi wa nadharia pamoja na mihimili ya nadharia iliyotumika katika utafiti. Mbinu za utafiti zilishughulikiwa zikijumuisha, muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, uteuzi wa sampuli,

ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data. Mtafiti pia alishughulikia kipengele cha uzingatifu wa maadili kuhitimisha sura ya kwanza.

Sura ifuatayo itashughulikia vipengele vya nafasi na mahali kama vinavyobainika katika hadithi fupi sita za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine.*

# SURA YA PILI

# VIPENGELE VYA NAFASI NA MAHALI KATIKA DIWANI YA *KURUDI NYUMBANI NA HADITHI NYINGINE*

## 2.0 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia vipengele vya nafasi na mahali vinavyopatikana katika hadithi fupi sita za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* kwa kuongozwa na mtazamo wa De jong (2012).

Soja (1990) anasema kuwa kando na wakati, wahusika na ploti, nafasi ni kiungo kikuu cha hadithi. Piatti na wengine (2009), umuhimu wa nafasi ni kuibua mandhari ya hadithi ambayo hubadilikabadilika kutegemea wahusika wanaoiunda nafasi hiyo kupitia kwa matendo yao. Nafasi basi hutegemea kwa kiasi kikubwa wahusika wanaotendea matendo katika nafasi fulani, kutembelea nafasi na kuitazama nafasi hiyo.

De Jong (2012) anasema kuwa uchambuzi wowote kuhusu nafasi na mahali katika simulizi unapaswa kuzingatia vipengele vifuatavyo:

1. Nafasi ya hadithi
2. Nafasi ya msimulizi
3. Fremu
4. Vielezo

Mtazamo huu ndio tulioutumia katika utafiti wetu.

## 2.1 Nafasi ya Hadithi

Chatman (1978) anasema kuwa nafasi ya simulizi haibainiki kwa uhalisi ila hujengwa mawazoni ambapo maneno hutumiwa kuchora taswira. Taswira hizi

hudokezwa kwa kutumia vivumishi vya sifa, kutaja vitu halisi au kutumia vilinganishi vya vitu halisi. Nafasi ya hadithi ni sehemu ambayo hadhira ya hadithi hiyo inaelekezwa kuangazia kwa makini na msimulizi.

Kwa upande mwingine anayafafanua mandhari na kusema kuwa ni jumla ya mazingira ya kijamii, kihistoria na kijiografia ambamo matendo hutendeka katika hadithi. Mazingira haya yanahusishwa na hadithi nzima. Aidha kuna kipengele cha nafasi inayohusishwa na ploti, ambamo matendo na mawazo ya wahusika hutawala. Nafasi hii hujumuisha maeneo yote yaliyotajwa katika hadithi, ambamo matendo ya kufikirika hutendeka katika mawazo ya wahusika. Matendo haya sio halisi bali ni ya kufikirika tu.

Prince (1987) anasema kuwa nafasi ya hadithi ni mahali ambapo hali na matukio yanayosimuliwa katika hadithi hutukia.

Vermette (1987) anaeleza nafasi kuwa mandhari ambayo ni mazingira ya kubuni, yanayotumiwa na msimulizi kufunua ploti ya hadithi na ambapo mhusika mkuu wa hadithi hupatikana.

Ryan (1991) anasema kuwa kinyume cha nafasi ya hadithi ni dunia ya hadithi. Anaieleza dunia ya hadithi kuwa ni jumla ya mawanda yote yanayokamilishwa na mawazo ya msomaji kwa kutegemea tajriba yake kitamaduni na tajriba ya ulimwengu halisi. Dunia ya hadithi hupokelewa na kuchorwa na mawazo kama dunia nzima yenye maumbile halisi na kamili ya kijiografia, huku yakijumuisha kwa mfano, maziwa yanayotenganisha maeneo, hata kama dunia ni ya kubuni ambayo haina maumbile kama haya. Katika hadithi yenye

mchanganyiko wa mazingira halisi na mazingira ya kubuni, dunia ya hadithi hutamalaki.

Kwa mjibu wa Ryan (1991), kando na dunia ya hadithi, kuna ulimwengu wa hadithi. Huu ni ulimwengu halisi unaowasilishwa kwenye hadithi pamoja na malimwengu dhahania yanayoundwa fikrani mwa wahusika. Ulimwengu wa hadithi hutokana na imani, matamanio, hofu, matarajio, haipothesia, ndoto na fantasia za wahusika hao.

Buchholz na Jahn (2005) wanaeleza nafasi ya hadithi kuwa ni mazingira halisi ambamo wahusika wa hadithi hutembelea na kuishi. Mazingira haya pia wanayaita mandhari. Wanaendelea kusema kuwa nafasi ya hadithi ina vipengele vya mazingira funge ambayo yanahusishwa moja kwa moja na matukio. Zoran (1984) anayaita mazingira funge eneo lionekanalo. Anasema kuwa mazingira funge ni mazingira ya matendo yanayohamahama na yanayoweza kufululiza na kuingiliana. Kwa mfano; mazingira ya chumba cha kunyolewa yanaweza kubadilika na kuwa chumba cha malazi kadri mhusika anavyohama katika chumba kile. Mazingira haya yana ngazi za nafasi ndogo na nafasi kuu. Kwa mfano, chumba ni nafasi ndogo ya nafasi kuu ambayo ni nyumba nzima. Bal (1985) anabainisha aina mbili za nafasi ya simulizi na kusema kuwa kuna nafasi inayomzingira mhusika na nafasi kama kipengele cha usimulizi.

De jong (2012) anasema kuwa waandishi mbalimbali huyapa mazingira uzito tofauti katika kazi zao. Baadhi ya waandishi huyapa mazingira umakini zaidi

huku wengine wakiyapa nafasi ndogo sana katika kazi zao. Kulingana naye, nafasi ya hadithi ni jumla ya mazingira ambamo matukio ya hadithi hutukia ambayo hayawezi kuwashilishwa kikamilifu katika hadithi. Anatofautisha katika ya nafasi ya fabula na nafasi ya hadithi na kusema kuwa nafasi ya fabula ni jumla ya nafasi inayoweza kuhusishwa na hadithi inayosimuliwa ilhali nafasi ya hadithi ni nafasi mahususi inayohusishwa na hadithi kama ilivyowasilishwa na mwandishi. Msomaji wa hadithi hupewa maelezo machache kuhusu nafasi na kuachiwa wajibu wa kukamilisha maelezo yasiyotolewa katika nafasi ya hadithi kutegemea tajriba yake. Mawazo haya yanaunga mkono kauli ya Stanzel (1984) anayesema kuwa sio rahisi kutoa maelezo ya nafasi katika hadithi kikamilifu.

Utafiti wetu ulitumia mtazamo wa De jong na kubainisha nafasi za hadithi zilizowasilishwa na waandishi wa hadithi zifuatazo zilizoteuliwa.

**Vinyago vya Watalii**

UK. 9: Aya 2

> *…. Chombo alitambua mara moja kwamba Chris alikuwa Mwamerika pindi tu alipoingia kibandani mwake…*

Uk. 11

> *Kabla Chris hajatoka katika kibanda cha Chombo, msichana mrembo wa Kiafrika alikuja mbio mbio na kujitoma humo. Alimkumbatia Chris na kumbusu midomoni. Chris alimgeukia Chombo na kusema kwa kicheko: "Sally -mpenzi wangu."*

Uk. 17

> *... Kabla hajainuka na kutoka kibandani, kiroja kikazuka kama mzuka kutoka kuzimu. Macho yake yalinasa kitu kama mfanano wa Sally mita ishirini kutoka kibandani…*

Mazingira ya matukio ni katika kibanda cha Chombo. Msimuliwa anapewa maelezo mafupi kuhusu kibanda kile kwamba kina kuta na kuachiwa kuijaza nafasi nzima ya kibanda hicho kutegemea tajriba yake ya vibanda vya biashara kama hii ya kuuza vinyago vya watalii.

Uk. 11

> *"Mimi niko likizoni hapa Mombasa kwa juma zima. Nitakachofanya ni kulipa nusu ya gharama yake ili isichukuliwe na mtu mwingine…*

Mazungumzo haya kati ya Chombo na Chris yanadhihirisha kwamba matukio ya hadithi yanafanyika katika mazingira ya Mombasa. Msimuliwa wa hadithi anatajiwa tu jiji la Mombasa na kuachiwa jukumu la kuchora picha ya mawazoni kuhusu jiji hili. Msimulizi hajajitwika wajibu wa kutoa maelezo kamili au kuchora mji wa Mombasa kimaandishi katika hadithi yake.

Uk. 14: Aya 8

> *Pindi alipopokea dola mia mbili kutoka kwa Chris, alikimbia benki na kubadilisha dola kwa sarafu ya Kenya…*

Tukio la kubadilisha dola kwa sarafu ya Kenya linafanyika katika benki. Hata hivyo, msimuliwa hajapewa habari kamili kuhusu benki yenyewe. Ameachiwa jukumu la kuchora picha ya mawazoni kuhusu benki na kujijazia maelezo ambayo hajapewa. Maswali mengi yanaweza kuibuka kuhusu nafasi hii kama vile: Benki ni gani? Iko wapi? Imejengwa vipi? Imejengwa kwa kutumia nini? Maswali haya yanapaswa kujibiwa na msimuliwa kutegemea tajriba yake.

Tukio la kulipa karo ya shule linatukia katika shule ya upili alikosomea Rukia. Vilevile mazingira haya yametajwa tu na hayajafafanuliwa zaidi. Msimuliwa pia ana jukumu la kujijazia habari ambazo hakupewa kuhusu shule ya upili alikosomea Rukia.

Uk. 19-20: Aya 10

> *…Njiani hawakuzungumza mengi. Chombo alijaribu kumdadisi Sally ili amfahamu zaidi. Lakini hakufika popote katika jitihada zake…. Wakawa wanatembea kimyakimya kando ya barabara, chini ya kivuli cha minazi…*

Mazingira ya matukio ni njiani kando ya barabara. Msimulizi anatoa maelezo machache kwamba njia waliyotumia Sally na Chombo wakielekea nyumbani kwa Chombo ilikua kando ya barabara chini ya kivuli cha minazi.

Uk. 20: Aya 2

> *… Walishakula sasa wamejilaza kitandani kulipisha jua la adhuhuri lililowaka moto…*

Mazingira ya matukio ni kitandani chumbani mwa Chombo majira ya adhuhuri baada ya chamcha. Wahusika Sally na Chombo wanasawiriwa wakipumzika baada ya kupata chamcha. Mwandishi hajatoa maelezo mengi kuhusu mazingira haya ila anamwachia msomaji ayajaze kwa ujumbe ambao hakupewa na mwandishi.

**Njozi ya Mtu Mweupe**

Uk 23: Aya 2

> *… Nchini Uingereza kwenyewe, na kwingineko katika makoloni yake, ndoto hii ilikuwa na mashabiki wengi. Babangu marehemu Robert Stoneheart, alikuwa mmoja wa mashabiki wake wakubwa…*

Njozi ya mtu mweupe ilishabikiwa nchini Uingereza ambako msimuliwa hajapewa maelezo kamili kuhusu nchi hiyo. Aidha ushabiki huu uliendelezwa katika makoloni ya Uingereza. Msimuliwa ana jukumu la kuvuta makini yake na kuyatambua makoloni ya Uingereza kutegemea tajriba yake katika historia.

Uk. 24: Aya 2

> *Robert Stoneheart alizaliwa na kulelewa Uingereza, katika Kijiji kidogo karibu na mji wa Manchester, mwaka wa 1895…*

Mahali alikozaliwa Robert Stoneheart ni katika Kijiji kidogo karibu na mji wa Manchester nchini Uingereza. Maelezo yanayotolewa ni kuhusu mahali ambapo jina lake halikutajwa, kwa hivyo, msimuliwa ana jukumu la kuchunguza vijiji vinavyozunguka mji wa Manchester nchini Uingereza. Vilevile, mandhari kiwakati yametajwa kwamba alizaliwa mwaka wa 1895 ila msimuliwa hajapewa habari za mwezi, tarehe, siku na saa.

Uk. 25: Aya 2

> *…Niliamka na kulivuta pazia. Kulikuwa asubuhi. Nilishangaa kuona kundi la watu nje ya nyumba yetu. Nilipotoka chumbani mwangu, niliona polisi wakishughulika nje na ndani ya nyumba…*

Matukio yanatukia nyumbani kwa kina Allan jijini Mombasa. Maelezo yanayotolewa hapa si kamili kwani yanataja tu chumba cha kulala cha wazazi wa Allan na chumba cha kulala cha Allan ambacho tunaelezwa kuwa kilikuwa na kitanda na pazia. Maelezo mengine yamebanwa hivyo msimuliwa anastahili kujaza pengo la sehemu ambazo hazikuelezwa za nyumba hii kutegemea tajriba yake.

**Mioyo ya Chuma**

Uk. 34: Aya 1

> *…Haya yalipotokea, Milka aliondoka kwenda Nairobi kuishi na Watoto wake waliofanya kazi huko. Kaikai akaachwa pweke nyumbani kumenyana na majuto na machungu.*

Aya 2

> *…Alipofika nyumbani, Milka alikwenda moja kwa moja na kuingia chumbani. Alijikaza kuutawala wahaka uliomtawala moyoni. Alijiambia kwamba kilichomrudisha hapa ni wajibu ambao lazima autekeleze…*

Nafasi ya hadithi hii ni nyumbani kwa Kaikai. Msimuliwa ana jukumu la kufahamu jinsi mazingira ya nyumbani yanavyokaa ili kujaza pengo la maelezo lililoachwa na msimulizi. Msimulizi anatoa maelezo finyu ya nafasi ya hadithi, ila anaonyesha kuwa matukio yanatukia nyumbani.

Uk.38: Aya 3

> *Kana kwamba alitaka kuthibitisha kauli yake, alishuka kutoka kitandani, akavuta viatu vyake vizee kutoka mvunguni na kuisukuma humo miguu yake. Kisha akasimama katikati ya chumba. Kwa wasiwasi mkubwa, Milka aliinuka…*

*Aya 4*

> *Kaikai alisogea karibu na mlango. Milka alikwenda karibu na dirisha akifikiria kwamba ingekuwa njia ya kutorokea kukitokea hatari yoyote. Lakini alikuwa amesahau kwamba dirisha lilikuwa na nondo. Kuweza kupitia hapo kulihitaji muujiza wa kujigeuza ndege au kipepeo…*

Matukio yanatukia katika chumba cha kulala cha Kaikai ambacho tunaambiwa kuwa mna kitanda alimolala Kaikai.Chumba hiki ndicho walicholala Kaikai na Milka kabla ya Milka kuondoka na kwenda Nairobi. Msimulizi anaeleza kuwa chumba hiki pia kilikuwa na mlango na dirisha lenye nondo.

Uk.38: Aya 5

> *…Ghafla, aliporomoka na kuanguka sakafuni. Kaikai alimwinamia akamshikashika na kujaribu kumpa huduma ya kwanza. Kisha akamchukua mikononi kama mtoto mchanga na kumlaza kitandani…*

Matukio ya kuanguka kwa Milka, Kaikai kumwinamia Milka na kujaribu kumpa huduma ya kwanza yanatokea sakafuni kwenye chumba cha kulala cha Kaikai. Maelezo kamili kuhusu mandhari haya hayatolewa isipokuwa kuyataja tu.

Uk. 39: Aya 2

> *Baada ya saa moja hivi, Milka alirudi katika hali yake ya kawaida. Kaikai alimwongoza hadi sebuleni. Alitayarisha chai wakanywa huku wakizungumza. Kaikai aliungua pazia la moyo wake…*

Matukio yanatukia sebuleni wanakokaa Kaikai na Milka. Katika mazingira haya chai inaandaliwa, mazungumzo yanaendelea kati ya Kaikai na Milka huku wakinywa chai.

Uk.41: Aya 1

> *Alizikwa nyuma ya nyumba kwenye kiwanja kizuri alichotayarisha kufanyia sherehe ya kuwakaribisha nyumbani mke na watoto wake…*

Mazishi ya Kaikai yalifanyika kwenye kiwanja kichokuwa nyuma ya nyumba yake. Mazingira haya hayajafafanuliwa kikamilifu ila yametajwa tu.

Katika hadithi hii, inabainika kuwa matukio mbalimbali yanatukia katika nafasi tofauti tofauti. Kuna yale yanayotukia Nairobi, nyumbani kwa Kaikai, kitandani, sakafuni na kiwanjani.

**Kurudi Nyumbani**

Uk. 64: Aya 1

> *Cathy alikuja kuniona hospitalini siku ya pili. Alipoingia kwenye wadi, alikuta nikiandaliwa kupelekwa kwenye chumba cha kupasuliwa…*

Mazingira ya matukio ni ya hospitalini ambako mhusika Gatobu alikuwa amelazwa baada ya kuhusika katika ajali ya barabarani. Msimulizi ambaye ni Gatobu anasimulia akiwa katika kitanda cha hospitali. Msimuliwa anatajiwa tu kuwa matukio ni ya hospitalini bila kupewa maelezo ya hospitali hiyo kikamilifu.

Uk.66

Aya 3

> *"Haya, Gatobu sasa tumefika. Mambo yatakuwa mazuri," yule wa kwanza alitangaza, huku akiongoza kitanda kuingia chumbani. Harufu kali ya madawa ilinipiga puani.*

Aya 4

> *"Sista, malizeni kazi yenu sasa ndio tuanze yetu. Mtoeni mgonjwa kitandani mumlaze kwenye meza ya kufanyia upasuaji…*

Matukio yanatukia katika chumba cha upasuaji hospitalini. Katika mazingira haya, ndipo Gatobu anapelekwa ili kufanyiwa upasaji wa mguu wake uliovunjika. Mgonjwa anapofikishwa hapa anatolewa kwenye kitanda na kulazwa kwenye meza ya upasuaji kisha upasuaji unaendelea.

Uk. 69: Aya 4

> *"Kwanza hii wadi ya kawaida nataka utoke leo hii," aliendelea. "Nataka upelekwe Amnesty Ward…*

Matukio yanatukia katika wadi ya kawaida hospitalini alikolazwa Gatobu baada ya kufanyiwa upasuaji na kutolewa kwenye thieta.

Uk. 74: Aya 2

> *…Dakika mbili baadaye, baba alikuja akaniita. Nilimfuata mpaka kwenye ofisi ya daktari.*
>
> *"Huyu ndiye kifunguamimba wa kwangu. Anaitwa Gatobu," baba alinijulisha kwa daktari. Daktari aliinamisha kichwa, akatabasamu.*

Matukio haya yanatukia katika ofisi ya daktari ambako daktari aliwaita Gatobu na babake kuwafahamisha kuhusu matokeo ya upasuaji alioufanyia Bibi Mawera mgonjwa wao. Ofisi ya daktari inatajwa tu bila kutoa ufafanuzi wake.

Uk. 77: Aya 5

> *…Tulipofika kwenye maegesho, daktari alituaga, akaenda na hamsini zake. Baba alifungua gari, nikaingia…*

Matukio haya yanafanyika katika maegesho ya magari ambapo Gatobu na Kiambi wanamsubiri baba yao amalize shughuli za kumhamisha Bibi Mawera hadi nyumbani. Msimuliwa hajapewa maelezo yoyote kuhsu maegesho ila tu kutajiwa matukio yaliyotukia pale.

**Mihuri ya Majanga**

Uk. 109: Aya 2

> *Muda si muda umati ulikusanyika katika uga mtakatifu uliokuwa karibu na bonde la Mto Sio…*

Mazingira ya matukio ni katika uga mtakatifu karibu na bonde la Mto Sio. Hapa ndipo jamii ya Wagimbi inakusanyika ili kufanya mambo yao pamoja. Katika mazingira haya pia, shughuli za kitamaduni kama vile matambiko hufanyika.

Uk. 114: Aya 1

> *... Alipita katika njia na vijia vyote vya kijijini akitoa ilani ya kuwaita wanaume wote. Wazee kwa wavuli walihitajika kukongamana wakiwa wamejihami barabara.*

Matukio yanatukia katika njia na vijia vyote vya kijijini ambako mjumbe wa jamii ya Wagimbi alipita akiwaita wanaume wote wa kijiji kwa kongamano la kutafuta suluhisho la janga la kuharibiwa mimea yao mashambani.

Uk. 117: Aya 2

> *Wakati huu wote Obando alikuwa akiyatazama haya yote katika kijipango kilichokuwa katika mojawapo ya vichuguu…*

Matukio yanatukia pangoni katika mojawapo ya vichuguu. Pangoni palikuwa mahali salama pa kujificha ili kuepuka shambulizi la jinyama lililovamia kijiji cha Wagimbi. Kichuguu pia ni nafasi ambayo inasawiriwa kama nafasi kubwa iliyobeba nafasi ndogo ambayo ni pango. Aidha, mwandishi anasema kuwa kulikuwa na vichuguu vingine.

**Safari ya Maangamizi**

Uk. 154: Aya 1

> *Mzee Majuto ambaye daima hurauka mapema alisikika nje ya nyumba yake akisemezana na mkewe...*

Matukio yanatukia nje ya nyumba ya mzee Majuto. Mzee majuto na Mama Kimweri wana mazungumzo kuhusu ndoto ya Mzee majuto.

Uk. 156: Aya 5

> *Kabole alifuatana na mzee Majuto kwenda kuonyeshwa mahali ambapo kaburi lingechimbwa. Ilikuwa ni katika sehemu ya chini ya shamba karibu na mwembe…*

Tukio la safari linatukia njiani kutoka nyumbani hadi sehemu ya chini ya shamba la Mzee Majuto karibu na mwembe. Aidha, msimulizi anatajiwa nafasi ya sehemu ya chini ya shamba chini ya mwembe ambako matukio ya baadaye ya kumzika Pendo yangefanyika.

## 2.2 Nafasi ya Msimulizi

De jong (2012) anasema kuwa msimulizi husimulia nafasi yake mwenyewe. Kulingana naye, nafasi ya msimulizi inaweza kuwa sawa na nafasi ya hadithi au ikawa tofauti kabisa. Msimulizi anaweza kubainisha aliko mwanzoni mwa usimulizi wake. Aidha anaweza kudhihirisha kuwa nafasi ya hadithi inapatikana katika wakati sawa na ule wa msimulizi.

**Njozi ya Mtu Mweupe**

Uk. 24: Aya 1

> *Robert Stoneheart (babake msimulizi Allan) alizaliwa na kulelewa Uingereza katika kijiji kidogo karibu na mji wa Manchester, mwaka wa 1895… Mwaka wa 1930, alijiunga na wahamiaji wa kiingereza nchini Kenya, akafika Mombasa. Nilikuwa na umri wa miaka mitano wakati huo…*

Aya 2

> *…Nilianza kwenda shule wakati huu. Bado tuliishi katika umaskini lakini Maisha nchini Kenya yalikuwa mazuri ikilinganishwa na hali ilivyokuwa tulikotoka…*

Msimulizi ambaye ni Allan anaeleza kuwa babake alizaliwa Uingereza. Anaeleza pia kwamba wazazi wake ambao ni Robert Stoneheart na Betsy Stoneheart walihama kutoka Uingereza hadi Mombasa nchini Kenya akiwa na umri wa miaka mitano, kwa hivyo, anamaanisha kuwa kwao ni Uingereza. Anazidi kusema kuwa maisha nchini Kenya yalikuwa mazuri kuliko hali

ilivyokuwa walikotoka. Mwandishi anaonyesha kuwa kuna tofauti kati ya nafasi ya hadithi na nafasi ya msimulizi. Hadithi inasimuliwa katika sehemu tofauti na alikozaliwa msimulizi ingawa msimulizi anarejelea kwao ili kutufahamisha.

Uk. 27: Aya 2

> *Babangu alipotoka jela hakutaka kuendelea kukaa Mombasa. Aliniambia kuwa alitaka tuhamie mahali pengine ili aweze kusahau yaliyotokea… Alinifichulia mpango wake wa kuuza hisa zake katika biashara yao- ambayo sasa ilikuwa ishaanza kustawi tena- kisha anunue shamba katika White Highlands. Baada ya wiki mbili tu babangu alikuwa amekamilisha mipango yote na sasa tulikuwa tayari kuhama.*

Aya 3

> *Maskani yetu mapya yalikuwa na nyumba kubwa iliyokuwa katika pembe ya shamba kubwa la mibuna, ekari thelathini. Upande wa kushoto, kama mita mia mbili hivi kutoka kwenye nyumba yetu, kulikuwa na vibanda kumi na vitano…Jirani yetu alikuwa Dkt. Welch- mmishonari ambaye alikuwa na zahanati hapo kwake, nusu kilomita kutoka kwetu…*

Msimulizi anaeleza kuwa maskani yao mapya baada ya kuhama kutoka Mombasa yalikuwa Limuru. Anaeleza kuwa punde tu walipohama kutoka Uingereza waliishi Mombasa lakini baada ya babake kutoka jela walihamia katika White Highlands- Limuru- ambako walikaribishwa na Dkt. Welch jirani yao. Msimulizi anaonyesha kuwa nafasi yake ni sawa na ile ya hadithi kwani matukio yanatukia huko Limuru ambako ni nyumbani kwa msimulizi.

**Kurudi Nyumbani**

Uk.74: Aya 1

> *Kwa nini niliita safari hiyo "Kurudi Nyumbani?" Kwanza nizungumzie hii dhana ya "nyumbani". Jambo moja ambalo wazazi wangu walihakikisha kuwa limezama katika akili za watoto wao wawili- yaani mimi na Kiambi- ni kuwa nyumbani kwetu ni Meru…*
>
> Aya 2
>
> *Bila kujali mawazo ya watu wengi, nilikuwa nimeamua kwamba kwangu mimi, nyumbani ni Nairobi. Sikuwa na lengo la kumshawishi yeyote akubaliane nami…*

Msimulizi ambaye ni Gatobu anaeleza kwamba asili yake ni Meru ingawa walikuwa wakiishi Nairobi kwa sababu huko ndiko yeye na babake Inspekta Mawera walikuwa wakifanyia kazi. Anaendelea kusema kuwa babake alisisitiza sana kwamba nyumbani kwao ni Meru, ila hakuridhishwa na wazo hilo kwa kuwa yeye na ndugu yake Kiambi walizaliwa na kulelelewa Nairobi. Pia anasema kuwa hakuona unyumbani wa Meru kwani marafiki zao walikuwa Nairobi na wale majirani wa Meru hawakuelewana nao. Kutokana na hali hii, alikata kauli bila kujali mawazo ya wengine kuwa kwake yeye nyumbani ni Nairobi.

**2.3 Fremu**

Kwa mujibu wa Ronen (1986), fremu ni mazingira yanayozunguka vitu, mahali au wahusika katika hadithi. Anaendelea kusema kuwa fremu huibua mawanda ya mbali yasiyofikika au kueleweka. Anaendelea kusema kuwa, mawanda haya si halisi na hutumika kupanua nafasi ya hadithi kwa njia mbalimbali.

Buchholz na Jahn (2005) wanasema kuwa fremu ni mahali ambapo matukio dhahania hutukia katika mawazo ya wahusika na sio matukio halisi bali ni ya kufikirika.

Dennerline (2009) anaeleza kuwa fremu ni mikoa katika simulizi. Anasema kuwa mikoa ni mazingira ambamo watu hukaa na kutendea matendo na ambapo huwa wanazungukia vitu fulani au wako kando ya vitu fulani katika maisha yao ya kila siku. Anasema kwamba fremu hutazamwa kwa mielekeo mitatu ambayo ina sehemu za ndani na nje. Kulingana naye, simulizi inaweza kutengeneza mikoa katika mchakato wa kusimulia matukio. Mikoa hii ina muundo wa nafasi na huleta tofauti baina ya usimulizi wa matukio na vielezo, mahusiano, mabishano na maoni.

De jong (2012) anasema kuwa fremu ni mahali pa kufikirika ambapo hutokea kwenye mawazo, ndoto na kumbukumbu za wahusika wa hadithi. Maoni ya De Jond ndiyo yaliyumika kuchambu kipengele cha fremu. Fremu katika hadithi teule inajitokeza ifuatavyo.

**Vinyago vya Watalii**

UK 15

> *"Ndiyo. Mimi na Chris tunakwenda States kufunga ndoa," Sally alisema kwa sauti ilyojaa fahari.*
>
> *… Chris alikwepa mada ya kuondoka Kwenda Marekani na Sally. Hili liliimarisha imani ya Chombo kwamba Sally kadanganyika.*

States au Marekani ni mazingira yanayotokea tu mawazoni mwa Sally kutokana na matamanio yake ya kwenda kuishi huko na mpenzi wake mzungu Chris. Hata hivyo, ni wazi kuwa japo Sally anataja “States”, nafasi hii inatokea mawazoni tu, kwani bado ako Mombasa.

UK 19

> *Mpango wake ulikuwa waende kwake wale, kisha watoke kwenda kujistarehesha kwa vinywaji katika klabu maarufu cha Nyota ya Ufukweni…*

Mazingira ya klabu ya Nyota ya Ufukweni yanatajwa tu kama mahali ambapo Chombo alikuwa amepanga waende kujistarehesha na Sally. Mpango wake Chombo haukutimia kwani aliibiwa na Sally na akatoroka na pesa zake zote. Mazingira haya yanabakia kuwa fremu.

**Njozi ya Mtu Mweupe**

UK 24: Aya 2

> *… Babangu alikuwa na umri wa miaka 35 na mamangu, Betsy Stoneheart, alikuwa na miaka 30. Tuliselelea Mombasa badala ya kufululiza mpaka White Highlands, kama wahamiaji wengi walivyofanya.*

Msimulizi anataja tu White Highlands katika usimulizi wake. Mazingira haya yanabakia tu kuwa mahali ambapo palitokea mawazoni mwa msimulizi. Mazingira haya ni fremu kwa sababu hapajatukia matukio yoyote hapo.

Uk. 24: Aya 2

> *Babangu aliajiriwa kazi na Tajiri mmoja kutoka Italia aliyekuwa na biashara ya hoteli. Tajiri huyo alitupa nyumba nzuri yenye vyumba viwili ambamo tuliishi.*

Italia ni mahali tu ambapo mwajiri wa Stoneheart alitoka. Msimulizi alifahamu tu kwamba mwajiri wa babake alitoka mahali kuitwako Italia. Hakuna matukio halisi ambayo yanatukia pale.

Uk. 25: Aya 2

> *... Kwa muda, waliendelea vizuri katika ubia. Ghafla wakaanza kuwa na mawazo ya ajabu. Walikata shauri kwenda Afrika kusini wakisafiria baharini…*

Afrika kusini ni mazingira yanayotokea mawazoni mwa msimulizi wala sio mahali panapotokea matukio halisi ya hadithi. Japo babake msimulizi walisafiri na kumwachia mama biashara, msimuliwa hajaambiwa tukio lolote lililotukia Afrika kusini. Mahali hapa ni fremu.

**Mioyo ya Chuma**

Uk. 36: Aya 4

> *Milka alijaribu kumtuliza. Akamhakikishia kwamba yeye na watoto wake hawakumchukia. Walimpenda. Alimkumbusha kwamba watoto walikuwa wamemjengea duka na kulijaza bidhaa…*

Duka kubwa ambalo Kaikai alikuwa amejengewa na watoto wake sio mahali halisi pa matukio ya hadithi hii ila linatajwa tu Milka anapomkumbusha Kaikai kwamba Milka na watoto wake hawakumchukia Kaikai. Duka hili linatokea katika kumbukumbu za mhusika Milka hivyo ni fremu.

**Kurudi Nyumbani**

Uk.74: Aya 1

> *…Itakuwaje mtu aishi Nairobi karibu maisha yake yote na bado asipatambue kama nyumbani? Mbali na nyumba ya kazini, babangu alikuwa na nyumba yake mwenyewe katika mtaa wa Kileleweshа.*

Mtaa wa Kileleshwa ni fremu inayotokea mawazoni mwa msimulizi Gatobu anapojiuliza kuhusu unyumbani wake. Mtaa huu unatajwa tu na Gatobu anapoeleza mambo yaliyomfanya kushawishika kuwa alistahili kuita Nairobi nyumbani licha ya wazazi wake kusisitiza kwake na nduguye Kiambi kwamba nyumbani kwao ni Meru. Msimulizi haelezi matukio halisi ya hadithi ambayo yanafanyika hapa ila tu kusema kwamba babake alimiliki nyumba katika mtaa huo.

**Mihuri ya Majanga**

Uk. 113: Aya 3

> *.... waliaswa na wazee hao kuwa hizo zilikuwa sauti za mizuka ya watu waliokufa maji ambao walirudi tena katika dunia yetu kutafuta wenzi wa kuandamana nao katika dunia ya pili...*

Wanawake wanapolalamikia waume zao kuhusu milio ya ajabu waliyoisikia bondeni walipokwenda kuteka maji, wanaambiwa kuwa milio hiyo ni ya mizuka waliokuja kwenye dunia yao ili kutafuta wenzi wa kuandamana nao katika dunia ya pili. Dunia ya pili ni nafasi ambayo inatokea kwenye mawazo ya wahusika hawa kwa kuamini kuwa watu waliokufa waliishi katika dunia ya pili. Nafasi hii sio mahali mahsusi ambapo panatendeka matendo halisi ya hadithi hii.

## 2.4 Vielezo

Friedman (2005) akimnukuu Prince (1997) anasema kuwa kielezo kinaweza kuwa simulizi ingawa kina sifa finyu sana za usimulizi, kwa kuwa kinasisitiza nafasi badala ya wakati yaani mahali pa matukio badala ya mfuatano wa

matukio kiwakati katika simulizi. Anaendelea kumnukuu Ryan (1997) na kusema kwamba, kielezo kinajitegemea katika simulizi na kinaweza kuepukwa na msomaji bila kuwa na madhara yoyote katika kuielewa ploti ya hadithi.

Dennerline (2009) akimnukuu Genette (1969) anasema kuwa usimulizi ni kutoa maelezo ya wahusika na vitu katika hali ya sogezi ilhali vielezo ni maelezo ya wahusika na vitu hali hali tuli.

Kwa mujibu wa De jong (2012), vielezo ni ufafanuzi wa kina wa mahali, vitu, watu na matukio. Ufafanuzi wa vielezo hutokea katika hali tulivu ambayo haina mpito wa wakati kama ilivyo katika hadithi. Ufafanuzi huu una mpangilio wa kimuundo ambao ni tofauti na mpangilio wa hadithi ambao ni wa kimantiki. Maoni ya De Jong yalitumika kudhihirisha vielezo vifuatavyo katika diwani teule.

**Vinyago vya Watalii**

Uk.7: Aya 1

> *"STUDIO YA CHOMBO" ndiyo maneno yaliyokukaribisha kwenye kibanda kimojawapo kando ya Barabara ya Moi. Vibanda vyote katika sehemu hii ya jiji la Mombasa viliendesha biashara ya kuuza sanaa kwa watalii… Wenye mahoteli na vioski, wenye teksi, wauza michoro na vinyago, makahaba… wote walishindania watalii wa Kimarekani.*

Msimulizi anafafanua kibanda mojawapo kando ya barabara ya Moi pamoja na biashara iliyoendeshwa katika jiji la Mombasa. Aidha anatoa maelezo kuhusu jiji la Mombasa na wateja walioifanikisha biashara katika jiji hilo. Anasema kuwa, watalii kutoka pembe zote za dunia ndio waliovutiwa na biashara ya

sanaa katika jiji hilo. Vilevile, anaifafanua dola ya Kimarekani kwa kuilinganisha na sarafu nyingine za watalii waliotoka kwingineko.

Uk.8: Aya1

> *…Michoro ya mandhari ya kuvutia jijini Mombasa: Ngome ya Yesu, Bandari ya Kilindini, Mji wa Kale, Ufuo wa bahari, sura mbalimbali za Bahari ya Hindi katika misimu tofautitofauti. Michoro ya wanadamu katika hali mbalimbali. Furaha, huzuni, majuto, ujana, uzee… kila mtu aliisifu sanaa ya chombo…*

Msimulizi anatoa maelezo ya kina kuhusu mabango ya michoro yaliyokuwa katika kibanda cha Chombo maelezo haya ni tuli na hayana mpito wa wakati.

Uk. 9: Aya 2

> *…Chombo alitambua mara moja kwamba Chris alikuwa Mwamerika pindi tu alipoingia kibandani mwake. Mrefu-futi sita-na aliyesema Kiswahili akichanganya na kile Kiingereza chao. Sifa nyingine ya Chris ambayo Chombo aliitambua mara moja ni kwamba alikuwa mpenda sanaa na mwenye ujuzi mkubwa kuhusu mambo ya sanaa…*

Maelezo ya kina yanatolewa kumhusu mhusika Chris, msimuliwa anafafanuliwa sifa zake kuhusiana na urefu, jinsi alivyoongea na mapennzi na ujuzi wake kuhusu sanaa. Maelezo haya hayaonyeshi mpito wa wakati, hivyo ni kielezo.

Uk 10: Aya1

> *… Chombo alikuwa ameipa picha hii jina la "Kipusa na Adui Yake." Kama kawaida, alikuwa ametia sahihi yake pembeni chini ya picha. Ilikuwa picha ya msichana mrembo aliyevalia nguo za ndani tu. Alikuwa amejipweteka kochini huku ameshikilia kioo kwa mkono wa kulia. Alikuwa akikagua uso wake kwenye kioo. Chini ya kochi kwenye mguu wake mmojawapo, nyoka alikuwa amejiviringisha. Alikuwa*

> *karibu kumshambulia kipusa ambaye alikuwa amepumbazwa na uzuri wake mwenyewe kiasi kwamba hakujua hatari iliyomkabili. Kichaka kilichozingira mahali hapo kilitilia mkazo ujumbe wa hatari iliyofichika na ambayo ingemfikia kipusa wakati wowote…*

Msimulizi anatoa maelezo ya kina ya picha ya "Kipusa na Adui Yake" ambayo ilikuwa imechorwa na msanii Chombo kwa madhumuni ya kuipeleka mashindanoni.

Uk. 17: Aya 2

> *… Aliishi (Chombo) peke yake katika chumba alichokodisha hapo mjini. Jamaa zake waliishi huko shamba yapata kilomita ishirini kutoka mji wa Mombasa.*

Kielezo hiki kinatumika kueleza umbali uliokuwa kati ya mji wa Mombasa alikoishi Chombo na shamba walikoishi jamaa zake.

**Njozi ya Mtu Mweupe**

Uk. 24: Aya 3

> *Babangu aliajiriwa kazi na tajiri mmoja kutoka Italia aliyekuwa na biashara ya hoteli. Tajiri huyo alitupa nyumba nzuri yenye vyumba viwili ambamo tuliishi…*

Msimulizi anaifafanua nyumba waliyopewa na mwajiri wa babake kutoka Italia. Anatoa maelezo ya sifa za nyumba hiyo na sehemu zake.

Uk. 25: Aya 2

> *…Baada ya miaka kumi tuliweza kununua nyumba yetu ambayo ilikuwa kubwa na nzuri kuliko ile ya tajiri wa babangu…*

Ufafanuzi unatolewa wa jinsi nyumba aliyoinunua babake Allan ilivyokuwa. Kielezo hiki kinatumika kulinganisha nyumba ya kupewa na nyumba inayomilikiwa na mhusika binafsi.

Uk. 27 Aya 3

> *Maskani yetu mapya yalikuwa na nyumba kubwa iliyokuwa katika pembe ya shamba kubwa la mibuni, la ekari thelathini. Upande wa kushoto, kama mita mia mbili hivi kutoka kwenye nyumba yetu, kulikuwa na vibanda kumi na vitano. Humu ndimo walimoishi waafrika waliofanya kazi shambani. Jirani yetu alikuwa Dkt. Welch- mmishonari ambaye alikuwa na zahanati hapo kwake, nusu kilomita kutoka kwetu…*

Ufafanuzi unaotolewa unahusu maskani mapya ya akina Allan pamoja na ujirani wake. Anaeleza jinsi maskani hayo yalikuwa kwa kueleza yalipopatikana, ujirani wake pamoja na wakaaji wa mahali pale.

Uk. 30: Aya 2

> *…Saida alikuwa msichana mwenye urefu wa wastani, mwembamba na mwingi wa madaha ya kike. Nilihisi kwamba nilitaka kufanya urafiki wa dhati naye.*

Msimulizi anatoa ufafanuzi wa Saida bintiye Dkt. Welch kwa kutoa ufafanuzi wa urefu wake, ukubwa na tabia yake. Ufafanuzi wa wahusika pia huunda nafasi ambayo ni vielezo.

**Mioyo ya Chuma**

Uk. 36: Aya 4

> *Milka alijaribu kumtuliza. Akamhakikishia kwamba yeye na watoto wake hawakumchukia. Walimpenda. Alimkubusha kwamba watoto walikuwa wamemjengea duka na kulijaza bidhaa. Naam, duka kubwa kushinda zote kote Mung'etho. Mazuri haya yaliyotokea miaka mingi iliyopita, yalizikwa katika kaburi la sahau…*

Maelezo kuhusu duka la Mung'etho alilojengewa Kaikai na kujaziwa bidhaa na watoto wake yanatolewa. Msimulizi anaambiwa kuwa duka la Kaikai

lilijengwa na watoto wake, lilikuwa limejazwa bidhaa na ndilo lililokuwa kubwa kuliko maduka yote huko Mung'etho.

Uk. 39: Aya 1

> *... kwa nini alishtuka (Milka) na kuzirai Kaikai aliposhuka kutoka kitandani? Kwani alishakuwa zimwi? Kaikai alikuwa hayawani? Kulikuwa na meza ndogo kando ya kitanda. Juu yake kulikuwa na kioo. Kaikai alikichukua na kujiangalia. Alijikodolea macho kutafuta dalili za ukimwi.*

Msimulizi anakifafanua chumba cha kulala cha Kaikai kwa kueleza vitu vilivyokuwa mle ndani. Msimulizi anataja kuwa mna kitanda, meza na kioo. Hiki ni kielezo kwa kuwa hakina mpito wa wakati.

**Kurudi Nyumbani**

Uk. 65: Aya 4

> *…Mmoja alikishikilia kitanda chenye vigurudumu upande wa mbele, wa pili akawa anakisukuma. Mwendo wote, nilikuwa nikitoa mlio wa maumivu kila kitanda kilipotikisika. Njia ilikuwa ya changarawe, na hivyo kilisukasuka sana…*

Msimulizi anatoa ufafanuzi wa kitanda kilichotumika kumpeleka thieta anaposema kwamba kilikuwa na vigurudumu. Aidha, anaifafanua njia waliyoitumia wakielekea thieta kwamba ilikuwa ya changarawe. Maelezo haya yanajenga vielezo.

Uk. 67: Aya 1

> *…Wanawake walikuwa wauguzi wa hapo chumba cha upasuaji. Sare zao za chanikiwiti zilitofautiana na za wale wa wadini ambao walivaa sare za buluu.*

Msimuliwa amepewa maelezo ya rangi za sare za wauguzi waliotofautiana kimaeneo ya kazi hospitalini. Katika maelezo haya inabainika kwamba sare za wauguzi wa chumba cha upasuaji zilikuwa za rangi ya chanikiwiti ilhali za wauguzi wa wadini zilikuwa za rangi ya buluu.

Uk.67: Aya 2

> *Meza ya kupasulia ilikuwa ndogo kuliko kitanda. Juu yake umbali wa mita moja unusu hivi, palikuwa na kidude kikubwa cha mviringo, chenye kipenyo cha mita moja hivi, na umbo la sahani. Kidude hicho kilikuwa na "visahani" vingine vingi ndani yake, vyenye kutoa mwanga mkali. Uchunguzi wangu wa chumba cha kupasulia na vifaa vyake ulikatishwa ghafla…*

Msimulizi anatoa ufafanuzi wa chumba cha kupasulia. Anaeleza vifaa vinavyopatikana kule kama vile, meza, kitanda na kidude cha mviringo. Vilevile, anatoa ufafanuzi wa vifaa hivi kwa kueleza umbo, umbali, viungo na kazi za vifaa hivyo.

Uk. 69: Aya 4

> *… "Nataka upelekwe Amnesty Ward. Huko chakula na huduma nyingine ni afadhali. Utakaa kwenye chumba chako na utakula chochote upendacho…*

Msimulizi anatoa ufafanuzi kuhusu Amnesty Ward ambako Cathy alikusudia kumhamishia Gatobu kutoka kwa wadi ya kawaida mle hospitalini Chogwa. Maelezo haya yanaleta ulinganisho wa wadi hizi mbili na kuonyesha kuwa wadi moja ni ya hadhi kuliko nyingine.

Uk. 72: Aya1

> *… Baada ya mazungumzo mafupi baina ya Mburugo, mwenye Trooper na dereva wetu, iliamuliwa nipelekwe hospitali ya Chogwa umbali wa*

> *kilomita hamsini kutoka hapo na kilomita thelathini hivi kutoka mji wa Meru...*

Msimulizi anatoa ufafanuzi wa umbali ulioko kati ya eneo la ajali na hospitali ya Chogwa na umbali kati ya hospitali ya Chogwa na mji wa Meru.

Uk. 78: Aya 3

> *... Wosia wake haukuwa na mambo mengi. Alikuwa na hoteli moja ndogo mjini Meru aliyoirithi kutoka kwa marehemu babake. Hiyo alinirithisha mimi. Kiambi naye akarithi shilingi elfu hamsini zilizokuwa katika akaunti yake jijini Nairobi. Alimalizia wosia wake kwa kusema kuwa alimrithisha bwanake mapenzi yasiyokadirika na baraka za Mungu.*

Msimulizi anatoa ufafanuzi wa urithi ulioachwa na mamake kabla ya kufa. Urithi huu ulijumuisha hoteli, pesa taslimu, mapenzi na Baraka.

Uk. 79: Aya 2

> *... Alisita, kisha akaendelea kusema, "sasa tunataka upelekwe wadi maalum ambapo utakaa kwenye chumba chako na kupata chakula na matibabu bora ili upone haraka.*

Msimulizi anatoa maelezo kuhusu huduma za wadi maalum ambapo Cathy alitaka Gatobu alazwe ili apone haraka. Katika chumba kile kuna usiri, chakula bora na matibabu bora.

Uk. 80: Aya 1

> *...Wale wauguzi walikisukuma kikatoka nje. Cathy na daktari walitufuata. Tulipinda kulia takafuata kijia cha changarawe, mwendo wa mita kumi hivi. Tulifikia jengo kubwa, umbo la mstatili, lililoezekwa kwa matofali mekundu. Jengo hilo lilikuwa na vyumba vingi ambavyo havikuonyesha dalili kwamba vilikaa watu. Chumba nambari mbili kilifunguliwa, kitanda kikasukumwa ndani.*

Msimulizi anafafanua shughuli nzima ya kumhamisha kutoka wadi ya kawaida hadi wadi maalumu. Anatoa ufafanuzi wa njia waliyopitia, maumbo ya majengo na malighafi ya majengo hayo.

Uk. 80: Aya 3

> *"Ukitaka msaada wowote, bonyeza swichi hii. Itapiga kengele kwenye ofisi iliyo mkabala na jengo hili na wanaohusika watakuja kukusaidia", muuguzi alieleza, huku akinionyesha swichi iliyokuwa ukutani juu ya kichwa changu. Walitoka, wakaniacha nikiyakagua mazingira yangu mapya. Kulikuwa kimya kabisa, chumba kilikuwa safi na chenye nafasi ya kutosha. Kushoto, kulikuwa na mlango uliofunguliwa kiasi. Nilichungulia nikaona bafu na choo. Katikati ya chumba kulikuwa na kimeza kilichozingirwa na viti vitatu vya mkono. Kando ya kitanda, upande wa kichwani, kulikuwa na kikabati ambacho juu yake kulikuwa na jagi ya maji na glasi mbili.*

Msimulizi anatoa maelezo ya maagizo aliyopewa kuhusu chumba chake kipya. Maelezo yanayotolewa na msimulizi yanahusu mazingira yake mapya ambayo ni wadi maalum kulingana na jinsi alivyokikagua Gatobu.

Uk. 91: Aya 1

> *...Nilikuwa chumbani mwangu nikisikiliza muziki kwenye redio yangu ndogo, kwa hivyo sikupata maneno hasa ya mazungumzo yao.*

Msimulizi anatoa maelezo kuhusu redio yake ambayo ilimshughulisha usiku hata akakosa kushughulika na mazungumzo ya wazazi wake.

**Mihuri ya Majanga**

Uk. 108: Aya 1

> *... Mto wa Sio ulizidi kukonda kadili jua lilivyozidi kuwaka hata ikawa muhali kwa mbavu zake kufichika. Mwili wake ulimomonyoka kabisa. Licha ya madhila haya, mto huu ulihifadhi ile sifa yake ya uungwana*

> *wa kufa kikondoo. Kama chatu mkongwe aliyesheheni kibudu cha mbuzi aendavyo, Mto Sio ulienda taratibu, mwendo wa kinyonga ukipinda na kupenya baina ya vijiji. Maji yake yaliwasaidia sana wakazi wa eneo hili.*

Ufafanuzi unaotolewa unahusu Mto wa Sio ulivyokuwa umeathirika kutokana na kukosekana kwa mvua kwa muda mrefu.

Uk. 113: Aya 3

> *…Wanawake hawa walilalamika kuhusu sauti za ajabuajabu kama za mtu akipiga mwenzake kofi zito, au sauti inayotolewa na mtego ufyatukapo unapokamata kitu…*

Msimulizi anatoa ufafanuzi wa hali ilivyokuwa bondeni walikokwenda kuteka maji akina mama. Anaeleza kuwa kulikuwa na milio ya ajabu ambayo inafananishwa na milio ya kofi au mfyatuko wa mtego.

**Safari ya Maangamizi**

Uk. 161: Aya 2

> *… Magari manne yalionekana yameegeshwa kando ya barabara iingiayo kwa mzee Majuto. Kwa muda mrefu, barabara hii ilikuwa katika hali mbovu. Ilikuwa na mashimo makubwa ambayo yalifanya vidimbwi wakati wa masika. Hata hivyo, vijana wa Kijiji hiki wakiongozwa na Kabole walikuwa wameikarabati barabara ili kufanikisha usafiri na hususan wa magari…*

Msimulizi anatoa ufafanuzi kuhusu hali ya barabara ya kuingia kwa Mzee Majuto ambako mazishi ya Pendo yangefanyika. Anaeleza jinsi barabara hiyo ilivyokuwa katika hali mbovu hapo awali na hali yake baada ya kushughulikiwa na vijana wa kijiji.

Uk. 161: Aya 3

> *… Jengo hili (jengo la ufuo) lilikuwa kwenye hospitali kuu ya wilaya iliyokuwa takriban kilomita sita kutoka pale nyumbani.*

Maelezo yanayotolewa yanahusu umbali ulioko kati ya jengo la ufuo na nyumbani kwa Mzee Majuto.

Uk. 162: Aya 2-163: Aya 1

> *… Eneo ambalo shughuli za mazishi zingefanyiwa lilikuwa limefyekwa vyema na kuwekwa katika hali safi. Mahindi katika eneo hili yalikuwa yameng'olewa ilhali baadhi ya matawi kwenye migomba ya ndizi yaliyokuwa yakining'inia ovyo yalikuwa yamekatwa. Upepo mwanana uliokuwa ukivuma kutoka upande wa chini uliwapa kitulizo waliohudhuria kutokana na jua kali. …Udongo uliotokana na ujenzi wa nyumba hii ulifanya kijilima kidogo kisichoota mmea wa aina yoyote. Sepeto zilionekana kando ya kijilima hiki kama ishara kuwa zilikuwa tayari wakati wowote kuweza kutoa heshima za mwisho. Kulikuwa na viti vichache ambavyo vilikuwa vimetengewa jamaa mahsusi… Jamaa wengine walijitafutia mahali pa kuketi huku wakifuatilia kwa karibu kila hatua ya ibada.*

Maelezo yanayotolewa na msimulizi yanahusu eneo la kaburi la Pendo. Msimulizi anatoa ufafanuzi wa jinsi sehemu hiyo ilivyoonekana pamoja na hali ya anga na matokeo ya uchimbaji wa kaburi.

Uk. 164: Aya 2

> *…Yalipokaribia kiasi cha kuweza kuonekana vizuri, ilibainika wazi kuwa mabasi haya yalikuwa yale ya Chuo Kikuu cha Kwenukwetu. Ubavuni yalikuwa yameandikwa kwa herufi kubwa na nzito: CHUO KIKUU CHA KWENUKWETU…*

Msimulizi anatoa ufafanuzi kuhusu mabasi yaliyobeba wanafunzi ambao walihudhuria mazishi ya Pendo. Anaeleza idadi ya mabasi yaliyoleta

wanafunzi katika mazishi ya Pendo, jinsi yalivyoandikwa pamoja na idadi ya waliokuwamo ndani ya mabasi hayo.

Uk. 165: Aya 4

> *…Huyu alikuwa si mwingine bali ni Faridi, rafiki wa karibu sana wa Pendo. Alikuwa msichana mrefu, mweupe pepepe, na mwenye nywele za singa…*

Ufafanuzi unaotolewa unahusu Faridi rafikiye marehemu Pendo. Msimulizi anaeleza uhusiano wake na marehemu Pendo, urefu wake, rangi yake na aina ya nywele zake.

Kutokana na mifano iliyotolewa ya vielezo, ni dhahiri kuwa waandishi mbalimbali wa hadithi wametumia kipengele cha vielezo kusawiri nafasi katika simulizi zao.

**2.5 Hitimisho**

Sura hii ilishughulikia vipengele vya nafasi na mahali kama vinavyodhirika katika hadithi fupi teule. Mtafiti alibainisha kati ya nafasi ya hadithi na nafasi ya msimulizi pamoja na kuonyesha kipengele cha fremu na vielezo. Vipengele hivi vyote vya nafsi vilitolewa mifano kutoka kwa hadithi fupi teule za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine.* Ilibainika kuwa, waandishi tofauti wa hadithi fupi wametumia vipengele vya nafasi ya hadithi, nafasi ya msimulizi, fremu na vielezo. Waandishi hawa wanaonyesha mazingira halisi ambapo matukio ya hadithi yanatukia kama vile; kibanda cha biashara, jiji kuu, nyumbani kwa mhusika, hospitalini, wadi, uga mtakatifu, pango, chumba cha kulala na nchi ya Uingereza. Isitoshe, waandishi hawa wameonyesha nafasi ya msimulizi. Kwa mfano, mwandishi anaonyesha kuwa msimulizi anasimulia

hadithi katika mazingira ya mbali na alikotoka. Anaonyesha kwamba mhusika fulani anasimulia kisa chenye matukio yanayotukia mbali na kwao. Vilevile, waandishi wametumia fremu katika kazi zao. Wametaja maeneo walikotoka wahusika bila kuonyesha matukio yoyote katika maeneo hayo. Pia wanaonyesha mahali ambako wahusika wengine walitamani kuzuru pamoja na nafasi nyingine zinazotajwa tu bila maelezo. Aidha, waandishi wametumia vielezo kwa kutoa fafanuzi za huduma, mahali, wahusika, hali, shughuli na vitu kama vile picha, sare, redio na mabasi

Sura itakayofuata ambayo ni sura ya tatu itashughulikia jinsi kipengele cha nafasi na mahali kinavyowasilishwa katika hadithi huku mifano ikitolewa kutoka hadithi sita teule za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine.*

# SURA YA TATU

# UWASILISHAJI WA NAFASI NA MAHALI KATIKA *DIWANI YA KURUDI NYUMBANI NA HADITHI NYINGINE*

## 3.0 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia namna kipengee cha nafasi na mahali kinavyowasilishwa kwa msomaji au msimuliwa katika hadithi fupi ya Kiswahili kwa kuchambua hadithi sita zilizoteuliwa katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine.*

Kwa mujibu wa De Jong (2012), uwasilishaji wa nafasi unahusu mambo manne makuu ambayo ni uhusishaji, mtazamo, kinachofafanuliwa na umbo la kile kinachofafanuliwa. Uhusishaji ni namna nafasi inavyowasilishwa kupitia kwa, mtazamaji ambaye anatambuliwa kama msimulizi, kivuli au mhusika wa hadithi. Katika uhusishaji tunajiuliza, “Je, ni kupitia kwa jicho la nani ambapo nafasi au kielezo kinawasilishwa?” Mtazamo unahusu umbali uliopo kati ya mwasilishaji na nafasi au kielezo kinachowasilishwa. Swali la mtazamo ni, “Je, mwasilishaji yuko umbali wa kiwango gani akihusishwa na nafasi au kielezo? Je, yuko karibu, kiwango cha wastani au mbali?” Swali jingine la kuuliza kuhusu nafasi ni nini kinachofafanuliwa na kina umbo gani?

## 3.1 Uhusishaji

De jong (2012) anaeleza kuwa katika uhusishaji wa nafasi katika hadithi tunafaa kujiuliza swali, “Je, ni kupitia kwa jicho la nani ambapo nafasi au kielezo kinawasilishwa?” Anaendelea kusema kuwa kuna jinsi tatu za

uhusishaji: Kupitia jicho la msimulizi, jicho la kivuli na jicho la mhusika. Utafiti wetu ulishughulikia njia mbili ambazo ni uhusishaji kupitia jicho la msimulizi na jicho la wahusika.

### 3.1.1 Uhusishaji Kupitia kwa Jicho la Msimulizi

Kwa mujibu wa De jong (2012), uwasilishaji wa nafasi au mahali unaweza kufanywa kupitia kwa jicho la msimulizi wa hadithi. Njia hii ya uwasilishaji hubainika kupitia kwa matumizi ya wakati uliopo. Hadithi teule zinahusisha nafasi kama inavyobainika katika mifano ifuatayo.

**Vinyago vya Watalii**

Uk.7: Aya 1

> *"STUDIO YA CHOMBO" ndiyo maneno yaliyokukaribisha kwenye kibanda kimojawapo kando ya Barabara ya Moi. Vibanda vyote katika sehemu hii ya jiji la Mombasa viliendesha biashara ya kuuza sanaa kwa watalii. Jiji la Mombasa lilikuwa maarufu miongoni mwa miji ya Kenya kwa kuwavutia watalii. Walitoka katika pembe zote za dunia: Marekani, Ulaya hata Ujapani na Uchina siku hizi. Watalii wa Kimarekani ndio waliowavutia zaidi wafanyibiashara mbalimbali. Sababu yake? Walikuja na dola- sarafu yenye nguvu kuzidi zote. Wenye mahoteli na vioski, wenye teksi, wauza michoro na vinyago, makahaba… wote walishindania watalii wa Kimarekani. Wenyeji wa Mombasa walishataalamika katika ujuzi wa kuwatambua watalii wa Kimarekani. Hata mwenyeji ambaye alikuwa hajawahi kukanyaga darasani aliweza kumtambua Mwamerika kutokana na matamshi yake. Mitindo yao ya mavazi, miondoko na ulaji yaliwatambulisha kwa urahisi.*

Nafasi hapa inawasilishwa kupitia kwa msimulizi. Msimulizi anamweleza msimuliwa kibanda cha Chombo kilivyowakaribisha watu

kupitia kwa maandishi makubwa yaliyoonyesha jina la kibanda hicho. Msimulizi anafululiza kueleza nafasi hiyo kwa upana.

### 3.1.2 Uhusishaji Kupitia kwa Jicho la Mhusika

De jong (2012) anasema kuwa uwasilishaji wa nafasi na mahali unaweza kufanyika kupitia kwa mmoja wa wahusika wa hadithi inayosimuliwa. Njia hii ya uwasilishaji hubainishwa kwa matumizi ya wakati uliopita katika hadithi. Kuna miundo tofauti ya uwasilishaji kupitia jicho la mhusika ambayo ni mhusika kutazama kupitia dirishani, kutazamama kwa mhusika akiingia mahali kama vile nyumba, mhusika kutembea mahali fulani kwa mfano mjini**,** mhusika kutazama kifaa au chombo huku akimwelezea mhusika mwingine kukihusu na mhusika anapotengeneza kitu husika. Njia hizi zimeshughulikiwa ifuatavyo na waandishi wa hadithi teule.

#### 3.1.2.1 Mhusika kuangalia kupitia dirishani

**Mioyo ya Chuma**

Uk. 38: Aya 1

> *Kupitia dirishani, Milka aliweza kuona mbingu lililotanda huko kwenye upeo wa macho. Chini ya mbingu, shamba lililolimwa lilisubiri mvua. Je, ni Kaikai aliyelima au alikuwa amekodisha shamba? Milka alijiuliza kimoyomoyo.*

Shamba la Kaikai linawasilishwa kupitia kwa jicho la mhusika Milka ambaye anapoangalia nje kupitia kwa dirisha analiona na kulitambulisha kwa msimuliwa.

#### 3.1.2.2 Mhusika akiingia mahali fulani kama vile nyumba

**Vinyago vya Watalii**

Uk. 14: Aya 8

> *Pindi alipopokea dola mia mbili kutoka kwa Chris, alikimbia benki na kubadilisha dola kwa sarafu ya Kenya. Kisha huyo! Mpaka shule ya upili alikosomea mdogo wake, Rukia. Akalipa na kumalizia karo iliyobaki…*

Msimulizi anamfahamisha msimuliwa kuhusu benki kwa kumtumia mhusika Chombo ambaye anaelekea pale punde tu, anapopokea dola kutoka kwa Chris kama malipo ya picha aliyomuuzia. Vilevile kupitia kwa Chris, msimuliwa anafahamishwa kuhusu shule ya upili alikosomea Rukia.

#### 3.1.2.3 Mhusika akitembea mahali fulani kwa mfano mjini.

**Vinyago vya Watalii**

Uk. 19-20: Aya 10

> *Wakawa wanatembea kimyakimya kando ya barabara, chini ya kivuli cha minazi. Chombo alizama katika mawazo ya jinsi alivyompata Sally kwa urahisi kuliko alivyotarajia…*

Chombo na Sally wanatembelea kando ya barabara wakielekea nyumbani kwa Chombo na kupitia kwa wahusika hawa msimuliwa anafahamishwa kuwa barabara hiyo ilizingirwa na minazi kwa sababu wanapitia kando ya barabara chini ya kivuli cha minazi.

#### 3.1.2.4 Mhusika kutazama kifaa au chombo huku akimwelezea mhusika mwingine kukihusu

**Vinyago vya Watalii**

Uk.12. Aya 7

> *"Picha nzuri sana bila shaka," Chris alisema kwa sauti ya chini kana kwamba alikuwa akijizungumzia.*
>
> *… "Lakini kuna kitu nataka kibadilishwe. Kitu kidogo tu."*
>
> *...Yule nyoka ambaye alikuwa karibu kumwangamiza kipusa alipewa nafasi kubwa sana katika mchoro. Ingekuwa bora kama hatari iliyowakilishwa na adui ya kipusa ipunguzwe. Yaani nyoka awe sehemu tu ya mazingira na asiwe tisho kubwa kwa kipusa. Kama vile kipusa hakuwa na habari juu ya kuwepo kwa nyoka, naye nyoka asiwe na habari juu ya kuwepo kwa kipusa…*

Msimuliwa anafahamu kuhusu picha ya chombo jinsi ilivyokuwa kupitia kwa ufafanuzi wa Chris. Chris anaitazama picha hiyo kwa undani na hatimaye kutoa maagizo ya jinsi alivyotaka ibadilishwe na Chombo huku akitaja sehemu ambazo alitaka zibadilishwe. Kupitia kwa mhusika Chris, msimuliwa anaifahamu nafasi hii barabara.

**Kurudi Nyumbani**

Uk.80: Aya 3

> *"Ukitaka msaada wowote, bonyeza swichi hii. Itapiga kengele kwenye ofisi iliyomo mkabala na jengo hili na wanaohusika watakuja kukusaidia", muuguzi alieleza, huku akinionyesha swichi iliyokuwa ukutani, juu ya kichwa changu.*

Muuguzi anaitazama swichi na kumwelekeza Gatobu jinsi ya kuitumia. Pia anamfahamisha jinsi swichi hiyo inavyotumika na vile itakavyomfaa. Kifaa hiki kinafahamika na msimuliwa kupitia kwa mhusika muuguzi.

### 3.1.2.5 Mhusika anapotengeneza kitu husika

De jong (2012) anaeleza kuwa, muundo huu huhusisha mawakala wanne ambao ni msanii anayeunda chombo au aliyekiunda awali, mhusika mtazamaji, msimuliwa anayechora picha ya mawazoni au kutafakari kuhusu kinachoundwa na msimulizi.

**Vinyago vya Watalii**

Uk. 12: Aya 7

> *"Unataka nini kibadilishwe?" Chombo aliuliza kwa sauti iliyofichua wasiwasi mkubwa.*
>
> *Chris alisafisha koo na kufafanua wazo lake. Yule nyoka ambaye alikuwa karibu kumwangamiza kipusa alipewa nafasi kubwa sana katika mchoro. Ingekuwa bora kama hatari iliyowakilishwa na adui ya kipusa ipunguzwe. Yaani nyoka awe sehemu tu ya mazingira na asiwe tisho kubwa kwa kipusa. Kama vile kipusa hakuwa na habari juu ya kuwepo kwa nyoka naye nyoka asiwe na habari juu ya kuwepo kwa kipusa…*

Mazungumzo haya yanahusisha Chombo ambaye ni msanii wa vinyago na Chris ambaye ni mteja wa Kimarekani, aliyekuja kununua mojawapo ya picha alizokuwa amezichora Chombo. Mhusika Chris anafafanua jinsi picha hiyo ilivyo huku akitaka Chombo aifanyie marekebisho kulingana na maagizo anayompa. Maelezo haya yanahusisha mawakala wanne ambao ni Chombo

mtengenezaji, Chris mnunuzi anayetaka picha itengenezwe upya, msimulizi na msimuliwa anayepata taswira ya mchoro huu katika hadithi.

### 3.2 Mtazamo / Mahali pa Msimamo

De jong (2012) anasema kuwa wawasilishaji wa nafasi na mahali hutazama na kuwasilisha wakiwa na umbali fulani kati yao na mandhari wanayowasilisha au vielezo wanavyowasilisha. De Jong anataja mbinu za mtazamo kama; mtazamo wa kipanorama, mtazamo wa kimandhari na mtazamo karibu. Mtazamo wa nafasi katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* umeshughulikiwa ifuatavyo.

#### 3.2.1 Mtazamo wa Kipanorama

Kwa mujibu wa De jong (2012) huu ni mtazamo ambao umbali kati ya mwasilishaji wa nafasi na nafasi anayowasilisha ni mkubwa. Mwasilishaji hutazama kutoka mbali na hivyo huweza kuona eneo kubwa bila kuzuiliwa na kitu chochote. Kuna hali mbili za kuelezea aina hii ya mtazamo.

##### 3.2.1.1 Mtazamo wa kipanorama kando

De jong (2012) anaeleza mtazamo huu na kusema kuwa, msimulizi wa hadithi husimama mahali mbali ambapo anaweza kuona sehemu kubwa ya kile anachowasilisha. Mtazamo huu ulibainika kwa namna zifuatazo:

**Vinyago vya Watalii**

Uk.7: Aya 1

> *"STUDIO YA CHOMBO" ndiyo maneno yaliyokukaribisha kwenye kibanda kimojawapo kando ya Barabara ya Moi. Vibanda vyote katika sehemu hii ya jiji la Mombasa viliendesha biashara ya kuuza sanaa kwa watalii. Jiji la Mombasa lilikuwa maarufu miongoni mwa miji ya Kenya kwa kuwavutia watalii…Wenye mahoteli na vioski, wenye teksi, wauza michoro na vinyago, makahaba… wote walishindania watalii wa Kimarekani.*

Msimulizi wa mandhari ya jiji la Mombasa amesimama mahali ambapo anaweza kuona hata vitu vilivyo mbali na yeye. Anaeleza kibanda cha Chombo pamoja na vibanda vingine katika Barabara ya Moi. Aidha anafahamu yote yanayoendelea katika biashara zote za jiji la Mombasa.

**Mioyo ya Chuma**

Uk. 38: Aya 1

> *Kupitia dirishani, Milka aliweza kuona mbingu lililotanda huko kwenye upeo wa macho. Chini ya mbingu, shamba lililolimwa lilisubiri mvua. Je, ni Kaikai aliyelima au alikuwa amekodisha shamba? Milka alijiuliza kimoyomoyo.*

Mbingu lililotanda na shamba la Kaikai ni nafasi zizotazamwa na mhusika Milka kutoka kwa mbali. Milka yuko ndani ya chumba cha kulala cha Kaikai ambapo anatazama nje kupitia dirishani na kuona mbingu na shamba kwenye upeo wa macho. Mhusika huyu anapotazama hazuiliwi na chochote.

### 3.2.1.2 Mtazamo wa kipanorama igizi

De jong (2012) anasema kuwa, katika mtazamo huu msimulizi huchukua nafasi ya mhusika mojawapo na kupachika mtazamo wake kwa kuchukua nafasi nzuri kama juu ya mnara au kilima.

**Mihuri ya Mjanga**

Uk.116: Aya 1

> *… Tajriba ya Obando ya usasi ilimfahamisha kuwa hali ilikuwa mbaya. Mkosi ulikuwa ukiwakonyezea. Kama amiri jeshi mweledi aliwaamrisha wasakaji wakimbilie usalama wao hadi mitini na vichuguuni. Wote walitawanyika kutii amri. Waling'ang'ania kila nafasi iliyokuwa kwenye miti mirefu na vichuguu virefu…*

Uk.117: Aya 2

> *Wakati huu wote Obando alikuwa akiyatazama haya yote katika kijipango kilichokuwa katika mojawapo ya vichuguu. Alimwona Mulisi na kumkumbuka Sihaha. Aliuchomoa mkuki wake. Jinyama lilikuwa likimtafuta mwanamume mwigine kuthibitisha uwezo wake…*

Msimulizi anaeleza matukio haya akiwa mahali ambapo anatazama yote bila kuzuiliwa. Ako mahali ambapo anawaona wasakaji wote wakiwa pale bondeni na pia mahali anamwona Obando akiwa ndani ya pango.

### 3.2.2 Mtazamo wa Kimandhari

De jong (2012) anasema kuwa katika mtazamo wa kimandhari, mwasilishaji hujiweka kwenye mandhari fulani na kuyaeleza. Mwasilishaji hupatikana ndani ya mandhari anayowasilisha. Mtazamo huu una aina mbili ambazo ni: Mtazamo wa kimandhari hamaji na mtazamo wa kimandhari tuli.

#### 3.2.2.1 Mtazamo wa kimandhari hamaji

De jong (2012) anaeleza kuwa huu ni mtazamo ambao mwasilishaji huhamahama katika mandhari anayowasilisha. Mwasilishaji huwa msimulizi ambaye huamuwa kuandamana na mmoja wa wahusika na kueleza mandhari yake.

**Kurudi Nyumbani**

Uk.80: Aya 1

> "*Baas, baas. Tayari", daktari alisema.*
>
> *Sasa nilikuwa nimelala chali kwenye kitanda cha wadi maalum. Wale wauguzi walikisukuma kikatoka nje. Cathy na daktari walitufuata. Tulipinda kulia tukafuata kijia cha changarawe, mwendo wa mita kumi hivi. Tulifikia jengo kubwa, umbo la mstatili, lililoezekwa kwa matofali mekundu. Jengo hili lilikuwa na vyumba vingi ambavyo havikuonyesha dalili kwamba vilikaa watu. Chumba nambari mbili kilifunguliwa, kitanda kikasukumwa ndani.*

Msimulizi ambaye pia ni mhusika Gatobu anafafanua mandhari yake huku akihamahama kutoka sehemu moja hadi nyingine. Anafafanua njia anayopita akipelekwa kwenye wadi maalum. Katika ufafanuzi wake, inabainika jinsi njia hiyo ilivyoundwa, umbali na umbo la jengo kubwa lililokuwa na chumba alicholazwa.

#### 3.2.2.2 Mtazamo wa kimandhari tuli

Huu ni mtazamo ambao mwasilishaji hujiweka mahali mahsusi katika mandhari na kuyawasilisha mandhari hayo bila kuhamahama.

**Kurudi Nyumbani**

Uk.67: Aya 2

> *Meza ya kupasulia ilikuwa ndogo kuliko kitanda. Juu yake umbali wa mita moja unusu hivi, palikuwa na kidude kikubwa cha mviringo, chenye kipenyo cha mita moja hivi, na umbo la sahani. Kidude hicho kilikuwa na "visahani" vingine vingi ndani yake, vyenye kutoa mwanga mkali. Uchunguzi wangu wa chumba cha kupasulia na vifaa vyake ulikatishwa ghafla nilipoinuliwa na kuketishwa kwenye ile meza…*

### 3.2.3 Mtazamo Karibu

Kwa mujibu wa De jong (2012), huu ni mtazamo ambao mwasilishaji wa nafasi hutazama nafasi au kielezo kwa karibu na kuwasilisha kwa msomaji au msimuliwa wa hadithi.

**Kurudi Nyumbani**

Uk.80: Aya 2

> *"Sasa hapa ndipo kwako", muuguzi mmoja alinieleza.*
>
> *"Unapapenda?" wa pili aliniuliza.*
>
> *"Si pabaya", nilijibu ingawa sikuwa nimekikagua chumba vizuri.*
>
> *"Ukitaka msaada wowote, bonyeza swichi hii. Itapiga kengele kwenye ofisi iliyo mkabala na jengo hili na wanaohusika wakuja kukusaidia", muuguzi alieleza, huku akinionyesha swichi iliyokuwa ukutani juu ya kichwa changu.*

Muuguzi anamfahamisha msimuliwa kuhusu swichi iliyokuwa karibu sana naye na mgonjwa aliyelazwa katika wadi maalum. Ni wazi kuwa swichi yenyewe iko karibu sana na msimulizi kwa sababu anasema "swichi hii". Kupitia mazungumzo kati ya Gatobu na wauguzi, ufafanuzi wa wadi maalum

unatolewa huku ikibainika kuwa mna swichi ya kuwezesha mawasiliano kati ya mgonjwa na wahudumu wa wadi ile. Muuguzi anafafanua wadi akiwa ndani yake kwa kuwa anasema “hapa”.

Wauguzi wanapotoka kwenye wadi, Gatobu anasalia pale na kwendelea kukikagua chumba kile alimolazwa huku akitoa ufafanuzi wa chumba hicho kwa sifa alizoziona kwa karibu.

### 3.3 Sifa za Ufafanuzi katika Vielezo

Dennerline (2009) akiwanukuu Hamo (1993) na Lopes (1995) anasema kuwa kigezo wazi cha kueleza kielezo ni kwa kuwapa wahusika na vitu sifa. Anaendelea kumnukuu Wolf (2007) na kusema kuwa, kinyume na masimulizi ambayo kwa kawaida huwa na uwasilishaji wa matukio wenye maana, kielezo hutoa uwakilishi wa kuwepo. Msisitizo huwekwa kwenye mwonekano wa kielezo kwa kuwa aghalabu vielezo huwa vitu tuli na vinavyoonekana. Uwepo wa vielezo sio kwa lengo la kuvitambulisha tu ila kwa kuviwasilisha kwa kuvipa sifa.

De jong (2012) akimnukuu Ford (1982) anasema kuwa msimulizi wa hadithi huangazia sifa mbalimbali za kifaa, chombo, mahali au mtu katika ufafanuzi wake wa vielezo. Ufafanuzi wake hujuisha sifa za: Mwonekano, sauti, harufu, na mguso.

### 3.3.1 Sifa za mwonekano/ kuangazwa

De jong (2012) anasema kwamba haya ni maelezo yanayochochea hisia za kuona kwa kutumia macho. Msimulizi hutumia sifa za kielezo kwa kutumia vitu ambavyo vinaweza kuonekana kwa macho na msimuliwa. Sifa hii imebainika kama ifuatavyo katika hadithi teule.

**Vinyago vya Watalii**

Uk 10: Aya1

> *…Kama kawaida, alikuwa ametia sahihi yake pembeni chini ya picha. Ilikuwa picha ya msichana mrembo aliyevalia nguo za ndani tu. Alikuwa amejipweteka kochini huku ameshikilia kioo kwa mkono wa kulia. Alikuwa akikagua uso wake kwenye kioo. Chini ya kochi kwenye mguu wake mmojawapo, nyoka alikuwa amejiviringisha. Alikuwa karibu kumshambulia kipusa ambaye alikuwa amepumbazwa na uzuri wake mwenyewe kiasi kwamba hakujua hatari iliyomkabili…*

Katika maelezo ya picha hii, vitu vya kuonekana kwa macho ni: Sahihi ya msanii Chombo, msichana mrembo aliyevalia nguo za ndani tu, kioo, kochi, nyoka aliyejivingirisha kwenye mguu wa msichana na kichaka.

**Kurudi Nyumbani**

Uk. 67: Aya 1

> *…Wanawake walikuwa wauguzi wa hapo chumba cha upasuaji. Sare zao za chanikiwiti zilitofautiana na za wale wa wadini ambao walivaa sare za buluu.*

Maelezo kuhusu sare za wauguzi ya sifa za kuonekana ambazo ni rangi za sare hizo. Msimuliwa anafahamishwa kuwa sare za wauguzi wa chumba cha

upasuaji zilikuwa za rangi ya chanikiwiti huku za wale wa wadini zikiwa za buluu, hivyo zilitofautiana.

Uk.67: Aya 2

> *Meza ya kupasulia ilikuwa ndogo kuliko kitanda. Juu yake umbali wa mita moja unusu hivi, palikuwa na kidude kikubwa cha mviringo, chenye kipenyo cha mita moja hivi, na umbo la sahani. Kidude hicho kilikuwa na "visahani" vingine vingi ndani yake, vyenye kutoa mwanga mkali.*

Ufafanuzi wa meza ya kupasulia unahusu viungo vinavyoonekana kama vile, kidude cha mviringo, kipenyo chenye umbo la sahani na visahani vilivyotoa mwanga mkali.

### 3.3.2 Sifa za sauti

De jong (2012) anaeleza kwamba baadhi ya wasimulizi huibua vielezo kwa kutoa sifa zinazohusiana na hisia za kusikia. Sifa hizi zimebainika katika hadithi mbalimbali kama ifuatavyo.

**Mihuri ya Majanga**

Uk. 113: Aya 3

> *Malalamishi ya pili yalitoka kwa akina mama waliokwenda bondeni kuchota maji ya kutumia nyumbani. Wanawake hawa walilalamika kuhusu sauti za ajabuajabu kama za mtu akipiga mwenzake kofi zito, au sauti inayotolewa na mtego ufyatukapo unapokamata kitu….*

Msimulizi anaeleza sauti zilizosikika kule bondeni walikokwenda kuteka maji wanawake kwamba zilikuwa kama za kofi zito au ya mfyatuko wa mtego. Sauti hizi zinatumika kulifafanua bonde hilo.

**Safari ya Maangamizi**

Uk. 164: Aya 2

> *Nyimbo ziliimbwa na vifungu vya Biblia kusomwa ili kuwafariji jamaa na marafiki na kuthibitishia halaiki kuwa hiyo ndiyo njia ya kila mmoja wao. Wakati mahubiri yalipokuwa yakiendelea, milio, vifijo na kamsa za kila nui zilisikika kutoka kwa mbali. Wote waliokuwepo waligeuka na kutazama upande ambapo kamsa hizi zilitokea.*

Sauti na milio, vifijo na kamsa za kila aina zinasikika zikitoka mbali na eneo lililokuwa na huduma ya mazishi ya Pendo. Hatimaye inabainika kuwa sauti hizi zilitoka kwenyae mabasi mawili ya chuo kikuu ambayo yalisafirisha wanafunzi waliohudhuria mazishi ya mwenzao Pendo. Sauti hizi zinatumika kama ufafanuzi wa mabasi hayo.

### 3.3.3 Sifa za harufu

Kwa mujibu wa De jong (2012) wakati mwingine msimulizi hubainisha kielezo kwa kutoa maelezo yanayoibua hisia za mnuso. Baadhi ya wasimulizi wa hadithi za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* wameishughulikia sifa hii ifuatavyo.

**Kurudi Nyumbani**

Uk. 66: Aya 1-3

> *"Haya, Gatobu sasa tumefika. Mambo yatakuwa mazuri", yule wa kwanza alitangaza, huku akiongoza kitanda kuingia chumbani. Harufu kali ya madawa ilinipiga puani.*

Harufu kali ya dawa inatumiwa na msimulizi kufafanua chumba cha upasuaji alikopelekwa Gatobu ili kupata matibabu baada ya kupata ajali ya barabarani. Harufu kali ya madawa inaibua hisia za mnuso.

Uk.80: Aya 4

> *Baada ya muda, Cathy aliingia chumbani. Alifunga mlango, akavuta kiti kimojawapo, akaketi karibu na kitanda akanikabili. Harufu ya marashi ghali aliyojipaka ilinipenya puani. Alikuwa mwanamke mzuri aliyependa kujipamba kwa mavazi na vipodozi vya aina mbalimbali. Macho yetu yalipokutana, alitabasamu. Sikujua nifanyeje au nisemeje.*

Maelezo yanayotolewa kuhusu marashi ya Cathy yanatumia sifa ya harufu kumfafanua mhusika huyu. Msimulizi anaeleza kuwa hii haikuwa harufu tu bali harufu ya marashi ghali.

### 3.3.4 Sifa za mguso

De jong (2012) anasema kwamba hizi ni sifa za kitu ambazo zinahusisha hisia za mguso. Msimulizi hutoa maelezo ambayo yanabainisha ugumu au ulaini wa kile anachokifafanua. Sifa hii imebainika katika hadithi fupi teule kupita kwa mifano ifuatayo.

**Safari ya Maangamizi**

Uk. 165: Aya 4

> *Hapo, kijana mmoja wa kike alisimama ghafla na kusogea mbele huku akiwa ameshika kijikaratasi mkononi. Huyu alikuwa si mwingine bali ni Faridi, rafiki wa karibu sana wa Pendo. Alikuwa msichana mrefu, mweupe pepepe, na mwenye nywele za singa. Macho yote yaligeuka kumtazama…*

Msimulizi anafafanua nywele za Faridi na kuibua hisia za mguso anaposema kuwa alikuwa na nywele za singa. Hizi ni nywele laini au nyororo na ulaini wa kitu hubainika kwa kukigusa. Msimulizi ametumia sifa ya mguso katika maelezo haya.

### 3.4 Maumbo ya Vielezo

De jong (2012) anasema kuwa vielezo vina maumbo tofauti tofauti. Anasema kwamba katika kutoa ufafanuzi, msimulizi hushughulika maumbo kwa kueleza, urefu, ufupi, muhtasari, maumbile na historia ya kielezo.

#### 3.4.1 Vielezo virefu

De jong (2012) anasema kuwa vielezo hivi vinatumia mitindo tofauti ya uwasilishaji kama vile, orodha, uhusishi au mtindo changamano wa kuunganisha mitindo mingi.

**Vinyago vya Watalii**

Uk 10: Aya1

> *... Chombo alikuwa ameipa picha hii jina la “Kipusa na Adui Yake.” Kama kawaida, alikuwa ametia sahihi yake pembeni chini ya picha. Ilikuwa picha ya msichana mrembo aliyevalia nguo za ndani tu. Alikuwa amejipweteka kochini huku ameshikilia kioo kwa mkono wa kulia. Alikuwa akikagua uso wake kwenye kioo. Chini ya kochi kwenye mguu wake mmojawapo, nyoka alikuwa amejiviringisha. Alikuwa karibu kumshambulia kipusa ambaye alikuwa amepumbazwa na uzuri wake mwenyewe kiasi kwamba hakujua hatari iliyomkabili. Kichaka kilichozingira mahali hapo kilitilia mkazo ujumbe wa hatari iliyofichika na ambayo ingemfikia kipusa wakati wowote. Chombo*

*alimfafanulia mteja wake kwamba maudhui ya mchoro ni hatari za kutokuwa macho.*

Msimulizi anatoa ufafanuzi mrefu kuhusu picha ya "Kipusa na Adui Yake". Katika maelezo yake anatumia mtindo wa orodha anapoeleza vitu vinavyopatikana katika picha hii kwa utaratibu wenye mantiki. Kwanza anatoa maelezo ya msichana ambaye ni kiungo muhimu cha picha hii kisha anamfafanua nyoka ambaye pia ni kiungo cha picha hii.

**Kurudi Nyumbani**

Uk.67: Aya 2

*Meza ya kupasulia ilikuwa ndogo kuliko kitanda. Juu yake umbali wa mita moja unusu hivi, palikuwa na kidude kikubwa cha mviringo, chenye kipenyo cha mita moja hivi, na umbo la sahani. Kidude hicho kilikuwa na "visahani" vingine vingi ndani yake, vyenye kutoa mwanga mkali. Uchunguzi wangu wa chumba cha kupasulia na vifaa vyake ulikatishwa ghafla. Nilipoinuliwa na kuketishwa kwenye ile meza…*

Msimulizi anatoa ufafanuzi wa kina kuhusu chumba cha upsuaji. Anaeleza kwa kina vifaa vilivyokuwemo pamoja na ukubwa wake, maumbo yake, kazi za vifaa hivyo pamoja na shughuli zilizoendeshwa mle.

### 3.4.2 Vielezo vifupi

De jong (2012) anasema kuwa wakati mwingine vielezo katika simulizi huwa vifupi. Anaendelea kusema kuwa vielezo vifupi huchuku muundo wa ordha ambapo sifa za kimhutasari hutolewa.

**Kurudi Nyumbani**

Uk. 67: Aya 1

> *Mengine yalifuata kwa haraka. Wale wauguzi walionileta walitoka na kitanda chao, wakamwacha daktari wa upasuaji na timu yake kunishughulikia. Pamoja na daktari huyo, timu hiyo ilikuwa na watu watano. Wanaume watatu na wanawake wawili. Wanawake walikuwa wauguzi wa hapo chumba cha upasuaji. Sare zao za chanikiwiti zilitofautiana na za wale wa wadini ambao walivaa sare za buluu.*

Maelezo yanayotolewa ni mafupi kuhusu timu ya daktari wa upasuaji aliyemshughulikia Gatobu. Anasema kwamba timu hii ilikuwa na wauguzi wa kike na wa kiume ambao jumla ya idadi yao ni watano. Msimulizi pia anaelza kwa kifupi sifa za sare zilizovaliwa na timu hiyo kwa kutaja rangi tu na kubana sifa nyinginezo.

**Njozi ya Mtu Mweupe**

Uk. 30: Aya 2

> *Tuliachwa pekee yetu. Haikuwa rahisi kuanzisha mazungumzo kwa sababu katika siku za nyuma uhusiano wetu uliishia kwenye salamu tu. Saida alikuwa msichana mwenye urefu wa wastani, mwembamba na mwingi wa madaha ya kike. Nilihisi kwamba nilitaka kufanya urafiki wa dhati naye.*

Maelezo mafupi yanatumika kumfafanua mhusika Saida kwa kuangazia tu kimo chake na tabia moja tu kuwa, alikuwa mwenye urefu wa wastani, mwembamba na mwingi wa madaha ya kike.

### 3.4.3 Vielezo vya kimhutasari

Haya ni maelezo ya kielezo ambayo yanatumia idadi ndogo ya maneno kufafanua kielezo husika. Msimulizi aghalabu hutumia neno moja linalotoa muhtasari wa kile anachokifafanua. Umbo hili limetumika ifuatavyo.

**Vinyago vya Watalii**

Uk.7: Aya 1

> *…Watalii wa Kimarekani ndio waliowavutia zaidi wafanyibiashara mbalimbali. Sababu yake? Walikuja na dola- sarafu yenye nguvu kuzidi zote. Wenye mahoteli na vioski, wenye teksi, wauza michoro na vinyago, makahaba… wote walishindania watalii wa Kimarekani…*

Ufafanuzi wa dola ya Kimarekani ni wa muhtasari kwa kuwa tunaambiwa tu kuwa ndiyo sarafu yenye nguvu kuzidi zote. Msimulizi hakupewa sifa nyingine wala kuelezwa nguvu hizi zilitokana na nini.

**Kurudi Nyumbani**

Uk.67: Aya 2

> *Meza ya kupasulia ilikuwa ndogo kuliko kitanda. Juu yake umbali wa mita moja unusu hivi, palikuwa na kidude kikubwa cha mviringo, chenye kipenyo cha mita moja hivi, na umbo la sahani. Kidude hicho kilikuwa na "visahani" vingine vingi ndani yake, vyenye kutoa mwanga mkali. Uchunguzi wangu wa chumba cha kupasulia na vifaa vyake ulikatishwa ghafla nilipoinuliwa na kuketishwa kwenye ile meza…*

Msimulizi anatoa muhtasari wa kidude kilichokuwa juu ya meza ya kupasulia kwa kusema kuwa kilikuwa cha mviringo na kikubwa. Vilevile kwa muhtasari anaeleza kuwa visahani vingi vilivyopatikana ndani ya kidude kile vilitoa mwanga mkali.

Uk. 91: Aya 1

> *…Nilikuwa chumbani mwangu nikisikiliza muziki kwenye redio yangu ndogo, kwa hivyo sikupata maneno hasa ya mazungumzo…*

Msimulizi Gatobu anatoa muhtasari wa maelezo kuhusu redio yake kwa kusema tu kwamba ilikuwa ndogo. Haya ni maelezo ya kimuhtasari.

### 3.4.4 Ufundi

De jong (2012) anasema kuwa katika kufafanua ufundi wa kielezo, msimulizi huamua kumweleza msimuliwa jinsi kifaa fulani kilivyotengenezwa kwa kufafanua viungo vikivyotumika kutengeneza kifaa hicho. Vilevile, hueleza ukubwa au udogo wake, thamani na sifa nyinginezo zinazokipa kifaa hicho upekee fulani.

**Vinyago vya Watalii**

Uk.8: Aya1

> *Chombo alikuwa kijana wa miaka ishirini na sita. Licha ya ujana wake alikuwa msanii aliyekomaa…kila mtu aliisifu sanaa ya chombo…*

Sanaa ya chombo inasifiwa na kila mtu kwa kuwa na sifa za kipekee. Alikuwa na michoro ya mandhari ya kuvutia jijini Mombasa. Isitoshe, alikuwa na michoro ya binadamu waliodhihirisha hisia toauti kulingana na hali zao.

**Kurudi Nyumbani**

Uk.67: Aya 2

> *Meza ya kupasulia ilikuwa ndogo kuliko kitanda. Juu yake umbali wa mita moja unusu hivi, palikuwa na kidude kikubwa cha mviringo, chenye kipenyo cha mita moja hivi, na umbo la sahani. Kidude hicho kilikuwa na "visahani" vingine vingi ndani yake, vyenye kutoa mwanga*

> *mkali. Uchunguzi wangu wa chumba cha kupasulia na vifaa vyake ulikatishwa ghafla nilipoinuliwa na kuketishwa kwenye ile meza…*

Msimulizi anaifafanua thieta kwa kueleza sifa za kipekee kama vile kuwa na meza ya kupasulia, kidude kikubwa cha mviringo chenye kipenyo na visahani vilivyotoa mwangaza mkali ndani ya kidude kile. Maelezo ya meza ya kupasulia na kipenyo yanaonyesha kimo. Kwamba meza ya kupasulia ni ndogo ikilinganishwa na kitanda, na kipenyo ni cha mita moja hivi.

Uk.80: Aya 1

> "*Baas, baas. Tayari", daktari alisema.*
> *Sasa nilikuwa nimelala chali kwenye kitanda cha wadi maalum. Wale wauguzi walikisukuma kikatoka nje. Cathy na daktari walitufuata. Tulipinda kulia tukafuata kijia cha changarawe, mwendo wa mita kumi hivi. Tulifikia jengo kubwa, umbo la mstatili, lililoezekwa kwa matofali mekundu. Jengo hili lilikuwa na vyumba vingi ambavyo havikuonyesha dalili kwamba vilikaa watu. Chumba nambari mbili kilifunguliwa, kitanda kikasukumwa ndani.*

Maelezo ya kiufundi yanatolewa kuhusu njia iliyotumika. Msimulizi anaeleza kuwa njiia hii ilikuwa ya changarawe. Isitoshe, msimulizi anaeleza kuhusu jingo ambalo lilikuwa la umbo la mstatili na kuezekwa kwa matofali.

### 3.4.5 Historia ya kielezo

Historia ya kifaa au kielezo inahusu wakati wa zamani au wa muda mfupi uliopita ambao hauwezi kuhusishwa na wakati wa hadithi husika.

**Mioyo ya Chuma**

Uk. 36: Aya 4

> *Milka alijaribu kumtuliza. Akamhakikishia kwamba yeye na watoto wake hawakumchukia. Walimpenda. Alimkubusha kwamba watoto*

> *walikuwa wamemjengea duka na kulijaza bidhaa. Naam, duka kubwa kushinda zote kote Mung'etho. Mazuri haya yaliyotokea miaka mingi iliyopita, yalizikwa katika kaburi la sahau…*

Inabainika wazi kwamba duka ambalo Kaikai alikuwa amejengewa na watoto wake lilikuwa limejengwa hapo awali walipokuwa na uhusiano mwema nao. Wakati huo ni tofauti na wakati wa hadithi kwa sababu kwa sasa hamna uhusiano mwema kati ya Kaikai na familia yake. Familia ya Kaikai imemtoroka na kuhamia Nairobi huku wakimwacha pweke Mung'etho. Hii ndiyo sababu Milka anajaribu kumhakikishia Kaikai kwamba yeye na watoto wake hawamchukii.

### 3.5 Hitimisho

Sura ya tatu ilishughulikia uwasilishaji wa nafasi na mahali katika hadithi fupi. Katika uwasilishaji, mtafiti alibainisha uhusishaji uliojibu swali kuwa ni kupitia kwa jicho la nani ambapo nafasi na mahali zinawasilishwa. Aidha, kipengee cha mtazamo au mahali pa msimamo kilishughulikiwa. Mtafiti pia alionyesha sifa fafanuzi katika vielelezo pamoja na maumbo ya vielezo.

Sura ifuatayo itashughulikia dhima ya mahali na nafasi katika simulizi hususan ujenzi wa maudhui na wahusika.

# SURA YA NNE

## DHIMA YA NAFASI NA MAHALI KATIKA SIMULIZI

### 4.0 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia dhima ya nafasi na mahali katika kujenga maudhui na wahusika wa hadithi. De jong (2012) akimnukuu Lausberg ([1960] 1998), anasema kuwa nafasi na mahali ni kipengele ambacho kilichukuliwa na waandishi wa kipindi cha usasa kama kiungo kidogo kisicho muhimu sana katika hadithi. Waandishi hawa walivipa vipengele vya ploti na wahusika hadhi kubwa katika hadithi ikilinganishwa na nafasi na mahali. Kipengele kilipewa dhima ya kutoa uwanja wa matukio kwa hadithi. Zaidi ya hayo, vielezo virefu vilichukuliwa kuwa na dhima ya kuipamba hadithi.

Hata hivyo, De jong (2012) anasema kuwa kipengele cha nafasi na mahali kina dhima zaidi. Kwanza, akiwanukuu Bal ([1985]1997), na Hammon (1987[199]) anasema kuwa, nafasi na mahali hutumika kujenga maudhui ya hadithi katika muktadha ambapo kipengele hiki ni kiungo kikuu kinachosimuliwa katika hadithi husika. Dhima ya pili ni kuangaza au kumulika maudhui ya hadithi inamopatikana. Nafasi na mahali hutumiwa kufafanua baadhi ya maudhui yanayoshughulikiwa katika hadithi zima. Isitoshe, kipengele hiki hutumika kijazanda kuashiria mambo fulani muhimu katika hadithi kama vile itikadi na tamaduni za jamii. Vilevile, kipengele hiki kina dhima ya kujenga wahusika kwa kueleza tabia, hali na mazingira ya kijamii anamofanyia kazi mtu. Katika sehemu hii tutachambua dhima tatu za nafasi na mahali ambazo ni; kujenga

maudhui ya hadithi, kuangaza au kumulika maudhui ya hadithi na kujenga wahusika wa hadithi.

### 4.1 Nafasi na Mahali katika Ujenzi wa Maudhui

De jong (2012) anasema kuwa mojawapo ya majukumu ya kipengele cha nafasi na mahali ni kujenga maudhui ya hadithi. Anaeleza kuwa ujenzi wa maudhui ya hadithi unaweza kutendeka kwa namna mbili. Namna ya kwanza ni nafasi na mahali kuwa kitovu cha hadithi. Yaani muktadha ambapo msimulizi hujikita katika kukishughulika kipengele hiki kwa kina katika hadithi yake. Jinsi ya pili ya kujenga maudhui ni hali ambapo kipengele cha nafasi na mahali hutumika kumulika au kuangaza na kufafanua maudhui ambayo tayari yanashughulikiwa katika hadithi zima. Katika hali hii, kipengele hiki sio kitovu cha hadithi ila skina mchango katika kujenga mambo muhimu yanayoshughulikiwa katika hadithi.

#### 4.1.1 Nafasi na Mahali kama Maudhui

Kipengele cha nafasi na mahali kimetumiwa kama kitovu cha hadithi katika hadithi teule za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* na hivyo kujenga maudhui ya hadithi zifuatazo.

##### 4.1.1.1 Vinyago vya Watalii

###### 4.1.1.1.1 Utalii

Msimulizi anajenga maudhui ya utalii anapofafanua Studio ya Chombo na kusema kuwa kilikuwa kibanda cha kuendesha biashara ya kuuza sanaa kwa

watalii. Anasema kuwa kibanda hiki kilikuwa miongoni mwa vibanda vingi vilivyopatikana kando ya Barabara ya Moi jijini Mombasa ambalo lilikuwa maarufu miongoni mwa miji ya Kenya kwa kuwavutia watalii kutoka pembe zote za dunia.

Uk. 7. Aya 1

> *…Vibanda vyote katika sehemu hii ya jiji la Mombasa viliendesha biashara ya kuuza sanaa kwa watalii. Jiji la Mombasa lilikuwa maarufu miongoni mwa miji ya Kenya kwa kuwavutia watalii. Walitoka katika pembe zote za dunia: Marekani, Ulaya hata Ujapani na Uchina siku hizi. Watalii wa Kimarekani ndio waliowavutia zaidi wafanyibiashara mbalimbali…*

**4.1.1.1.2 Biashara**

Msimulizi anaeleza kuwa kibanda cha Chombo kiliendesha biashara ya kuuza sanaa kwa watalii sawa na vibanda vyote vilivyokuwa kando ya Barabara ya Moi jijini Mombasa. Aidha anasema kuwa wenye mahoteli na vioski, wenye teksi, wauza michoro na vinyago na hata makahaba walishindania watalii wa Kimarekani kwa sababu walikuja na sarafu yenye nguvu zaidi ya zote duniani-dola.

Uk. 7, Aya 1

> *"STUDIO YA CHOMBO" ndiyo maneno yaliyokukaribisha kwenye kibanda kimojawapo kando ya Barabara ya Moi. Vibanda vyote katika sehemu hii ya jiji la Mombasa viliendesha biashara ya kuuza sanaa kwa watalii…*

#### 4.1.1.1.3 Mashindano

Msimulizi anaitumia picha ya Kipusa na Adui Yake ili kujenga maudhui ya mashindano. Anasema kuwa picha hii ndiyo iliyochukuliwa na Chombo kama kilele cha ufanisi wake kama msanii. Alikuwa na maazimio ya kuipeleka picha hii kushindania tuzo mojawapo.

Uk. 9 Aya 2

> *Kulikuwa na picha moja ambayo Chombo aliipenda sana. Aliichukulia picha hii kama kilele cha ufanisi wake kama msanii. Aliposikia habari za mashindano ya uchoraji, aliazimia kuipeleka picha hii kushindania tuzo mojawapo…*

Uk. 10 Aya 1

> *…Chris aliigeukia ile picha ambayo Chombo alidhamiria kuipeleka mashindanoni. Chombo alikuwa ameipa picha hii jina la "Kipusa na Adui Yake"…*

#### 4.1.1.1.4 Bidii

Bidii ya Chombo inadhihirika kupitia michoro ya kila aina ambayo inapatikana katika kibanda chake cha biashara. Kibanda hiki kimejaa michoro ya mandhari ya kuvutia jijini Mombasa. Vilevile, kibanda hiki kina michoro ya wanadamu katika hali mbalimbali za maisha.

Uk.8 Aya 2

> *Chombo alikuwa kijana wa miaka ishirini na sita. Licha ya ujana wake, alikuwa msanii aliyekomaa. Sanaa yake ilikuwa uchoraji. Kibanda chake kilijaa mabango ya michoro yake…*

#### 4.1.1.1.5 Ubunifu

Kibanda cha Chombo kinadhirisha ubunifa wa hali ya juu. Msimulizi anaeleza jinsi kilivyo na mabango mengi ya michoro ya Chombo. Aidha mna picha moja maalum ambayo ilimvutia Chris ambaye ni mtalii wa Kimarekani. Picha hii ni ya thamani ya juu ingawa Chombo hatambui hivyo kwani anapotamka bei ya juu ya picha kimakosa, Chris halalamiki ila anaendelea na mpango wa kuinunua. Isitoshe, baada ya Chombo kumweleza mteja wake maudhui ya picha ile, Chris anakubaliana naye na kwendelea kufikiria maudhui ya ndani ambayo Chombo hakuyatambua.

Uk.8 Aya 2

> *Chombo alikuwa kijana wa miaka ishirini na sita. Licha ya ujana wake, alikuwa msanii aliyekomaa. Sanaa yake ilikuwa uchoraji.*

Uk. 10 Aya 1

> *… Baada ya kuzikagua picha zote zilizoegemezwa kwenye kuta za kibanda na nyingine kutundikwa, Chris aliigeukia ile picha ambayo Chombo alidhamiria kuipeleka mashindanoni. Chombo alikuwa ameipa picha hii jina la "Kipusa na Adui Yake"…*

Uk. 10 Aya 2

> *Chris alikubaliana naye kwa kutikisa kichwa. Lakini aliendelea kuikagua picha kana kwamba alikuwa akiyafikiria maudhui ya ndani ambayo Chombo hakuyatambua…*

#### 4.1.1.1.6 Ukengeushi

Nchi ya Marekani inajenga maudhui ya ukengeushi kwa kuwa Sally anajivuna kuwa wanaenda kufunga ndoa na Chris huko ingawa Chris anakwepa mada hiyo kabisa. Chombo naye anaamini kuwa Sally kandanganywa kwa kuwa ni

mazoea ya wazungu kudanganya wasichana waaafrika. Isitoshe, Chombo aliamini kuwa mambo ya Sally na Chris kwenda kuoana ni porojo tupu. Anasema kuwa kila kahaba mjini alikuwa na ndoto kama hiyo.

Uk. 15. Aya 4

> *"Ndiyo. Mimi na Chris tunakwenda States kufunga ndoa," Sally alisema kwa sauti iliyojaa fahari.*
>
> *Chombo hakuamini. Alijiambia kimoyomoyo kwamba Sally kandanganywa na Chris. "Ndiyo mazoea ya hawa wazungu kuja kundanganya wasichana wetu," aliwaza.*

Uk.16 Aya 2

> *... Yale mambo ya kwenda na Chris kuoana, aliamini kwamba ni porojo tupu. Kila kahaba mjini alikuwa na ndoto kama hiyo.*

**4.1.1.2 Njozi ya Mtu Mweupe**

**4.1.1.2.1 Ubabe**

Bila kuihusisha nchi ya Kenya, Waingereza walitaka kuifanya Kenya kuwa Nchi ya Mtu Mweupe, jambo ambalo lilishabikiwa sana nchini Uingereza na kwingineko katika makoloni ya Uingereza.

Uk. 23. Aya ya 2

> *Mwanzoni mwa karne ya ishirini, Waingereza walikuwa na njozi. Walitaka kuifanya Kenya "Nchi ya Mtu Mweupe". Nchini Uingereza kwenyewe, na kwingineko katika makoloni yake, ndoto hii likuwa na mashabiki wengi. Babangu, marehemu Robert Stoneheart, alikuwa mmoja wa mashabiki wake wakubwa. Hata baada ya Uingereza kuutambua ujinga wake na kuitupilia mbali njozi yake, babangu aliishikilia kwa nguvu...*

#### 4.1.1.2.2 Ubinafsi

Nchi ya Kenya imetumika kuonyesha ubinafsi wa Waingereza. Waingereza walitaka kuifanya Kenya Nchi ya Mtu Mweupe ingawa wana nchi yao na makoloni mengine. Pia walieneza ndoto yao na kupata mashambiki wengi kutoka nchi mbalimbali.

Uk. 23. Aya 2

> *Mwanzoni mwa karne ya ishirini, Waingereza walikuwa na njozi. Walitaka kuifanya Kenya "Nchi ya Mtu Mweupe". Nchini Uingereza kwenyewe, na kwingineko katika makoloni yake, ndoto hii likuwa na mashabiki wengi. Babangu, marehemu Robert Stoneheart, alikuwa mmoja wa mashabiki wake wakubwa. Hata baada ya Uingereza kuutambua ujinga wake na kuitupilia mbali njozi yake, babangu aliishikilia kwa nguvu...*

#### 4.1.1.2.3 Kujitegemea

Jiji la Mombasa linatumiwa kuonyesha hali ya kujitegemea ya Stoneheart. Ijapokuwa mzungu huyo aliaandamana na wengine kutoka Uingereza hadi Mombasa, wenzake walipofululiza hadi White Highlands kustakimu huko, yeye alibaki jijini Mombasa.

Uk. 24. Aya 2

> *...Mwaka wa 1930 alijiunga na wahamiaji wa Kiingereza nchini Kenya, akafika Mombasa. Nilikuwa na umri wa miaka mitano wakati huo. Babangu alikuwa na umri wa miaka 35 na mamangu, Betsy Stoneheart, alikuwa na miaka 30. Tuliselelea Mombasa badala ya kufululiza mpaka White Highlands, kama wahamiaji wengi walivyofanya.*

#### 4.1.1.2.4 Mabadiliko

Nyumba aliyoinunua Stoneheart ilikuwa kubwa na nzuri zsaidi ikilinganishwa na ile aliyopewa na mwajiri wake. Haya yalifanyika baada ya Stoneheart kufanya jitihada kuondoa umaskini na kuimarisha hali ya familia yake kiuchumi.

Uk. 25. Aya 2

> *Babangu alifanya jitihada kubwa kuepukana na umaskini tuliozaliwa nao. Polepole, hali yetu kiuchumi ilianza kuwa nzuri zaidi. Baada ya miaka kumi, tuliweza kununua nyumba yetu, ambayo ilikuwa kubwa na nzuri kuliko ile ya tajiri wa babangu…*

#### 4.1.1.2.5 Safari

Allan anaeleza kuwa baada ya biashara ya mwajiri wa babake kuimarika, Stoneheart na mwajiri wake walipata mawazo ya ajabu ya kwenda Afrika Kusini wakisafiri baharini.

Uk. 25. Aya 2

> *…Ghafla wakaanza kuwa na mawazo ya ajabu. Walikata shauri kwenda Afrika Kusini wakisafiria baharini. Kwa hivyo shughuli zote za biashara yao wakamwachia mamangu…*

#### 4.1.1.2.6 Subira

Kitanda cha Allan kinatumiwa kudhihirisha subira aliyokuwa nayo. Baada ya kugutushwa na mlipuko mkubwa, Allan alikaa kitandani akijadiliana na nafsi yake ikiwa alikuwa ndotoni au mlipuko aliousikia ulikuwa wa ukweli.

Uk. 25. Aya 3

*…Baada ya muda, niligutushwa na mlipuko mkubwa. Kwa kitambo fulani nilikaa kitandani nikijadiliana na nafsi yangu ikiwa nilikuwa ndotoni, au mlipuko nilousikia ulikuwa wa kweli…*

**4.1.1.2.7 Ujirani mwema**

Allan alishangaa kuona kundi la watu nje ya nyumba yao. Hii ilikuwa baada ya mlipuko mkubwa kusikika toka nyumbani mwao. Aidha polisi walikuwa wakishughulika nje na ndani ya nyumba yao.

Uk. 25. Aya 3

*…Niliamka na kulivuta pazia. Kulikuwa ni asubuhi. Nilishangaa kuona kundi la watu nje ya nyumba yetu. Nilipotoka chumbani mwangu, niliona polisi wakishughulika nje na ndani ya nyumba…*

**4.1.1.2.8 Siri**

Chumba cha wazazi wa Allan kilihifadhi siri ya kilichotendeka mle ndani. Allan hakukubaliwa kuingia kwenye chumba cha wazazi wake cha kulala. Isitoshe, waliokuwa pale hawakutaka kuzungumza naye. Kumweleza yaliyotokea.

Uk. 26. Aya 1

*…Sikukubaliwa kuingia katika chumba cha wazazi wangu nilipotaka kufanya hivyo. Hakuna aliyetaka kuzungumza nami kunieleza yaliyotokea.*

#### 4.1.1.2.9 Sheria

Gereza linatumiwa kuashiria kwamba sheria hufuatwa mtu anapofanya hatia. Stoneheart aliachiliwa kutoka gerezani baada ya vita kuu vya pili. Alikuwa amefungwa kwa miaka mitano baada ya kumuua mkewe Betsy kwa kuisambaratisha biashara yao.

Uk. 26. Aya 2 na 3

> *…Babangu alitiwa nguvuni, akashtakiwa, akapatikana kuwa na hatia, akafungwa miaka mitano…Vita kuu vya pili vilikuwa vimekwisha wakati babangu alipoachiliwa kutoka gerezani…*

### 4.1.1.3 Mioyo ya Chuma

#### 4.1.1.3.1 Utengano

Nafasi ya nyumbani kwa Kaikai na Nairobi zimetumika kujenga maudhui ya utengano. Milka anatengana na mumewe Kaikai anapoondoka nyumbani kwake na kuenda kuishi Nairobi na watoto wake huku akimwacha Kaikai pweke.

Uk. 34: Aya 1

> *Mzee Kaikai alikuwa mtu mwenye ghadhabu na uchungu. Kiini cha hali hii kilikuwa pigo kubwa la kuwachwa na watoto wake. Ndoa yake na Milka ilidumu kwa zaidi ya miaka thelathini lakini hili halikuizuia kuporomoka. Haya yalipotokea, Milka aliondoka kwenda Nairobi kuishi na watoto wake waliofanya kazi huko. Kaikai akaachwa pweke nyumbani kumenyana na majuto na machungu.*

#### 4.1.1.3.2 Bidii

Duka kubwa ambalo Kaikai alijengewa na watoto wake huko Mung'etho linatumika kuonyesha bidii kubwa ya watoto hao. Duka hilo lilikuwa kubwa kushinda zote kote Mung'etho na baada ya kulijenga walilijaza bidhaa.

Uk. 36: Aya 4

> *Milka alijaribu kumtuliza. Akamhakikishia kwamba yeye na watoto wake hawakumchukia. Walimpenda. Alimkubusha kwamba watoto walikuwa wamemjengea duka na kulijaza bidhaa. Naam, duka kubwa kushinda zote kote Mung'etho. Mazuri haya yaliyotokea miaka mingi iliyopita, yalizikwa katika kaburi la sahau…*

#### 4.1.1.3.3 Uwajibikaji

Kitendo cha watoto wa Kaikai cha kumjengea baba yao duka kubwa kinadhihirisha uwajibikaji. Watoto hao walimjali baba yao kiasi cha kujitwika jukumu la kumjengea duka nzuri kwani linapolinganishwa na maduka mengine huko Mung'etho liliyapiku kwa ukubwa. Isitoshe, watoto hao walilijaza duka hilo bidhaa.

Uk. 36: Aya 4

> *...Alimkubusha kwamba watoto walikuwa wamemjengea duka na kulijaza bidhaa. Naam, duka kubwa kushinda zote kote Mung'etho. …*

### 4.1.1.4 Kurudi Nyumbani

#### 4.1.1.4.1 Uwajibikaji

Hospitali alikolazwa Gatobu baada ya kupata ajali imetumika kuonyesha uwajibikaji wa wahusika wa hadithi. Cathy alienda kumtembelea Gatobu

hospitalini. Aidha, wahudumu wa hospitalini wanashughulika kumwandaa Gatobu ili kumpeleka kwenye chumba cha kupasuliwa.

Uk. 64: Aya 1

*Cathy alikuja kuniona hospitalini siku ya pili. Alipoingia kwenye wadi, alikuta nikiandaliwa kupelekwa kwenye chumba cha kupasuliwa…*

#### 4.1.1.4.2 Mazingira

Njia ya changarawe iliyotumiwa kuelekeza mgonjwa kwa thieta inaonyesha mazingira mabovu ya hospitali. Hii ni kwa sababu Gatobu anasema kuwa alipopelekewa njia, hii kitanda kilitikisika na kumsababishia maumivu makali yaliyosambaa kutoka mguu uliokuwa umevunjika hadi mwili mzima.

Uk. 65: Aya 4

*…Njia ilikuwa ya changarawe, na hivyo kilisukasuka sana. Si uchungu huo uliosambaa kutoka mguu wa kushoto uliovunjika hadi mwili mzima.*

#### 4.1.1.4.3 Utabaka

Wadi ya kawaida na Amnesty Ward zimetumika kuonyesha tofauti za kitabaka hospitalini. Huduma katika Amnesty Ward ni bora kuliko zile za wadi ya kawaida kwa kuwa mgonjwa hukaa katika chumba chake, hula apendacho na hutunzwa na jamaa zake.

Uk. 69: Aya 4

*"Kwanza hii wadi ya kawaida nataka utoke leo hii," aliendelea. "Nataka upelekwe Amnesty Ward. Huko chakula na huduma nyingine ni afadhali. Utakaa kwenye chumba chako na utakula chochote upendacho. Nitafanya mipango ili nije kukutunza mimi mwenyewe."*

#### 4.1.1.4.4 Malezi

Hali ya nyumbani kuwa Meru ni funzo lililotolewa na kusisitizwa sana na Inspekta Mawera na Bibi Mawera kwa watoto wao. Sehemu ya malezi yao ilikuwa kuhakikisha kwamba funzo hili limeeleweka na kuzama katika akili za watoto wao, kwamba nyumbani kwao ni Meru. Wazazi hawa walitaka watoto wao Kiambi na Gatobu waelewe kuwa japo waliishi Nairobi walikaa pale kwa sababu ndiko baba yao alikofanyia kazi, nyumbani kwao kulikuwa Meru.

Uk.74: Aya 1

> *Kwa nini niliita safari hiyo "Kurudi Nyumbani?" Kwanza nizungumzie hii dhana ya "nyumbani". Jambo moja ambalo wazazi wangu walihakikisha kuwa limezama katika akili za watoto wao wawili- yaani mimi na Kiambi- ni kuwa nyumbani kwetu ni Meru...*

#### 4.1.1.4.5 Utamaduni

Nyumbani kuwa Meru kwa Gatobu kunaonyesha Imani ya kitamaduni kwa sababu licha ya kuwa baba yao alifanyia kazi Nairobi, alimiliki nyumba katika mtaa wa Kileleshwa na familia yake kustakimu Nairobi katika nyumba ya kazini, wazazi walisisitiza kwamba nyumbani kwao ni Meru. Wazazi wanaonekana kuwa na jukumu la kufunza watoto wao utamaduni wao kwani hawakutaka wafikirie kwamba kwao ni Nairobi. Haya yanatokea licha ya kuwa marafiki za watoto hawa walikuwa wa Nairobi na hawakupatana na watoto waliokuwa majirani zao huko Meru walipoenda kutembea wakati wa likizo.

Uk.74: Aya 1

> *Kwa nini niliita safari hiyo "Kurudi Nyumbani?" Kwanza nizungumzie hii dhana ya "nyumbani". Jambo moja ambalo wazazi wangu*

*walihakikisha kuwa limezama katika akili za watoto wao wawili- yaani mimi na Kiambi- ni kuwa nyumbani kwetu ni Meru… tulizaliwa na kulelewa Nairobi. Tulikuwa tunapelekwa Meru, mara kwa mara, na hasa wakati wa likizo kwenda kutembea…*

**4.1.1.4.6 Maamuzi**

Maamuzi ya Gatobu anapoamua moyoni mwake kwamba nyumbani ni Nairobi licha ya vishawishi vya wazazi wake kwamba kwao ni Meru yanadhihirika. Gatobu alipofanya maamuzi haya hakuwa na nia ya kumshawishi yeyote kukubaliana naye.

Uk. 74: Aya 2

*Bila kujali mawazo ya watu wengine, nilikuwa nimeamua kwamba kwangu mimi, nyumbani ni Nairobi. Sikuwa na lengo la kumshawishi yeyote akubaliane nami…*

**4.1.1.5 Mihuri ya Majanga**

**4.1.1.5.1 Kiangazi**

Mto Sio unadhihirisha madhara ya jua kali liliozidi kuwaka katika kijiji cha Wagimbi. Mto huu ulizidi kupungua na kujikokota kwa sababu ya upungufu wa maji. Hata hivyo, maji machache yaliyobaki yaliwasaidia sana wakazi wa vijiji ambamo mto ulipitia.

Uk. 108: Aya 1

*… Mto wa Sio ulizidi kukonda kadili jua lilivyozidi kuwaka hata ikawa muhali kwa mbavu zake kufichika. Mwili wake ulimomonyoka kabisa. Licha ya madhila haya, mto huu ulihifadhi ile sifa yake ya uungwana wa kufa kikondoo. Kama chatu mkongwe aliyesheheni kibudi cha mbuzi*

> *aendavyo, Mto Sio ulienda taratibu, mwendo wa kinyonga ukipinda na kupenya baina ya vijiji. Maji yake yaliwasaidia sana wakazi wa eneo hili.*

**4.1.1.5.2 Dini**

Wagimbi wana uwanja matakatifu karibu na bonde la mto. Sehemu hii inaendeshewa shughuli rasmi ambazo zinaongozwa na kiongozi wa jamii. Uwanja wenyewe unatumiwa kama korti ya uma wanaposimama wanakjiji kujibu mashtaka waliyoshtakiwa. Katika sehemu hii wanajamii hufanyia matambiko maalum ya lazima ambayo yakiepukwa huleta madhara kwao.

Uk. 109: Aya 2

> *Muda si muda umati ulikusanyika katika uga mtakatifu uliokuwa karibu na bonde la Mto Sio. Wagimbi wote wakiongozwa na Oriang'i walihitajika kusimama mbele ya korti ya umma kwa mashtaka ya kupuuza na kuzembea wajibu…*

**4.1.1.5.3 Nafasi ya mwanamke**

Bondeni wanakokwenda kuchota maji akina mama, kunatumika kuonyesha majukumu ya wanawake katika jamii. Wanawake walijumuika kwenda kuteka maji ya kutumia nyumbani hivyo kuonyesha kwamba ndio wanaofanya kazi za nyumbani. Wanawake hawa wanawasimulia waume zao na wazee wa kijiji matukio yaliotukia bondeni.

Uk. 113: Aya 3

> *Malalamishi ya pili yalitoka kwa akina mama waliokwenda bondeni kuchota maji ya kutumia nyumbani. Wanawake hawa walilalamika*

*kuhusu sauti za ajabuajabu kama za mtu akipiga mwenzake kofi zito, au sauti inayotolewa na mtego ufyatukapo unapokamata kitu…*

#### 4.1.1.5.4 Mawasiliano

Mjumbe wa wanakijiji anapita katika njia na vijia vya kijijini ili kuwaita wanaume kwenye kongamano ambalo walihitajika kuhudhuria wakiwa wamejihami, ili kukabiliana na jinyama lililovamia kijiji chao.

Uk. 114: Aya 1

*Mimea ya wakulima iliharibiwa zaidi. Jambo hili liliwauma sana wanakijiji kiasi cha kuzika katika kaburi la sahau sauti za kofi bondeni. Vifua vyao vilichemka kwa hasira. Vilitishia kupasuka wakati wowote. Ilibidi hatua ichukuliwe. Ong'ura kurumbiza wa kijiji alikuwa ameshapata kazi tena. Kazi aliyoipenda na kuienzi. Hakusubiri kuraiwa maana hata yeye aliitegemea sana mimea iliyokuwa ikiharibiwa. Alipita katika njia na vijia vyote vya kijijini akitoa ilani ya kuwaita wanaume wote. Wazee kwa wavuli walihitajika kukongamana wakiwa wamejihami barabara.*

#### 4.1.1.5.5 Ushirikina

Bonde linatumika kudhihirisha imani ya ushirikina ya Wagimbi. Wanawake wanapokwenda kuteka maji bondeni wanasikia sauti kama za makofi mazito. Wanapolalamika kuhusu sauti hizi kwa waume zao na wazee wa kijiji wanaaswa kuwa waangalifu kwa kuwa zile ni sauti za mizuka ya watu waliokufa maji. Walishauriwa dhidi ya kuitana kwa majina mmoja wao asije akateuliwa na mizuka kujiunga nao.

Uk. 113: Aya 3

> *…Waliporudi makwao na kuwalalamikia waume zao pamoja na wazee wa kijiji, waliaswa na wazee hao kuwa hizo zilikuwa sauti za mizuka ya watu waliokufa maji ambao walirudi tena katika dunia yetu kutafuta wenzi wa kuandamana nao katika dunia ya pili. Waume na wazee waliwaasa wanawake kuwa waangalifu sana waendapo mtoni. Aidha wakisikia sauti hizo wasiitane kwa majina yao ili kujiepusha na janga la mmoja wao kuteuliwa na mizuka kujiunga nao.*

#### 4.1.1.6 Safari ya Maangamizi

##### 4.1.1.6.1 Utamaduni

Mahali pa kuchimba kaburi panatumika kuonyesha utamaduni wa jamii. Mzee Majuto babake marehemu Pendo ndiye anayeonyesha vijana mahali pa kuchimba kaburi. Mzee huyu hakuhusika moja kwa moja katika uchimbaji kwani hii ni kazi ya vijana wakiongozwa na mmoja wao. Kaburi linachimbwa mahali maalum kwenye shamba.

Uk. 156: Aya 5

> *Kabole alifuatana na mzee Majuto kwenda kuonyeshwa mahali ambapo kaburi lingechimbwa. Ilikuwa ni katika sehemu ya chini ya shamba karibu na mwembe…*

##### 4.1.1.6.2 Mazingira

Mazingira ya eneo la kuendeshea shughuli za mazishi yanaandaliwa hivyo, kusaidia kutunza mazingira. Eneo hilo lilifyekwa huku mimea iking'olewa na matawi yaliyoning'inia kukatwa. Shughuli hii kwa upande mmoja inatunza

mazingira kwa kuyanadhifisha kwa upande mwingine inayaharibu kwa kung'oa mimea ya chakula na kukata matawi.

Uk. 162: Aya 2-163: Aya 1

> *... Eneo ambalo shughuli za mazishi zingefanyiwa lilikuwa limefyekwa vyema na kuwekwa katika hali safi. Mahindi katika eneo hili yalikuwa yameng'olewa ilhali baadhi ya matawi kwenye migomba ya ndizi yaliyokuwa yakining'inia ovyo yalikuwa yamekatwa...*

### 4.1.2 Nafasi na Mahali katika Kumulika Maudhui ya Hadithi

Kipengele cha nafasi na mahali kimetumika kumulika au kuangaza na kufafanua maudhui ambayo tayari yanashughulikiwa katika hadithi teule za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*.

#### 4.1.2.1 Vinyago vya Watalii

##### 4.1.2.1.1 Madhara ya kutokuwa makini

Msimulizi anatumia picha ya Chombo aliyoiita "Kipusa na Adui Yake" kumulika maudhui ya madhara ya kutokuwa makini yanayoshughulikwa katika hadithi. Picha hii inaonyesha msichana mrembo aliyekuwa katika hatari ya kushambuliwa na nyoka bila kufahamu. Maudhui haya yanafafanuliwa na Chombo kwa mteja wake Chris. Maudhui haya yanalingana sana na hatari iliyomkumba Chombo kwa kusalitika na mapenzi ya kinafiki ya Sally hata akamwibia dola, pesa na saa yake ya thamani. Aidha, chumba cha Chombo kinachangia maudhui haya kwani baada ya kula, Chombo anasalitika na mapenzi ya Sally na kujisahau hadi akaibiwa pesa zake, dola zake na saa yake ya thamani na Sally aliyemdhania kuwa mpenzi.

Uk 10: Aya1

> *...Alikuwa karibu kumshambulia kipusa ambaye alikuwa amepumbazwa na uzuri wake mwenyewe kiasi kwamba hakujua hatari iliyomkabili. Kichaka kilichozingira mahali hapo kilitilia mkazo ujumbe wa hatari iliyofichika na ambayo ingemfikia kipusa wakati wowote. Chombo alimfafanulia mteja wake kwamba maudhui ya mchoro ni hatari za kutokuwa macho.*

Uk.20 Aya 2 na 3

> *Chumbani mwa Chombo. Walishakula sasa wamejilaza kitandani kulipisha jua la adhuhuri lililowaka moto…Chombo akaingiwa na wasiwasi. Akashuka kutoka kitandani. Aliingiza mkono uliokuwa ukitetemeka kwenye ule mfuko alimotia zile dola. Hazikuwemo. Akainama na kuvuta sanduku kutoka mvunguni. Akalifungua kuangalia zile pesa alizobakisha kutokana na malipo ya kwanza. Hazikuwepo. Akagutuka tena alipokumbuka saa yake ya thamani. Wakati wa kunywa dawa, alikuwa ameitoa na kuiweka juu ya kiti. Haikuwepo. Pigo la kutambua kilichotokea lilimwangukia kama jabali lililorushwa kutoka angani.*

**4.1.2.1.2 Mapenzi**

Kibanda cha Chombo kinatumika kumulika maudhui ya mapenzi yanayodhihirishwa na Sally kwa Chris. Msimulizi anaeleza jinsi Sally alivyojitoma katika kibanda cha Chombo akamkumbatia Chris na kumbusu midomoni, kisha Chris akamgeukia Chombo na kumtambulisha Sally kama mpenzi wake. Kibanda cha Chombo kinatumika kama mahali pa kudhirisha mapenzi. Vilevile Chris anaonyesha mapenzi yake kwa Sally kwa kushauriana naye kuhusu suala la kurejea kibandani mwa Chombo kuchukua picha.

Uk.11 Aya 5

> *Kabla Chris hajatoka katika kibanda cha Chombo, msichana mrembo wa Kiafrika alikuja mbio mbio na kujitoma humo. Alimkumbatia Chris na kumbusu midomoni. Chris alimgeukia Chombo na kusema kwa kicheko:*
>
> *"Sally – mpenzi wangu."…*

Uk.15 Aya 2

> *…"Utarudi lini kuichukua picha?" Chombo aliuliza.*
>
> *Chris alimgeukia Sally kana kwamba hakuweza kulijibu swali hilo bila msaada wa mpenzi wake.*

**4.1.2.2 Njozi ya Mtu Mweupe**

**4.1.2.2.1 Utabaka**

Waingereza wanadhihirisha utabaka kwa kuweka mipaka kati ya watu weupe na watu weusi kwa kutaka kuifanya Kenya ambayo ni nchi ya mtu mweusi kuwa nchi ya mtu mweupe, wanaonyesha kuwa kuna tofauti kati ya mtu mweupe na mweusi. Aidha, mtu mweupe ni bora kuliko mtu mweusi. Isitoshe, taifa la Uingereza linataka kuchagua Kenya miongoni mwa makoloni mengine yake.

Uk.23. Aya 2

> *Mwanzoni mwa karne ya ishirini, Waingereza walikuwa na njozi. Walitaka kuifanya Kenya "Nchi ya Mtu Mweupe". Nchini Uingereza kwenyewe, na kwingineko katika makoloni yake, ndoto hii likuwa na mashabiki wengi. Babangu, marehemu Robert Stoneheart, alikuwa mmoja wa mashabiki wake wakubwa. Hata baada ya Uingereza kuutambua ujinga wake na kuitupilia mbali njozi yake, babangu aliishikilia kwa nguvu...*

Maudhui haya yameshughulikiwa kwa kina katika hadithi hii, kwa mfano, msimulizi anapoeleza jinsi wazungu wahafidhina walivyoshikilia kuwa mzungu alikuwa binadamu bora kuliko binadamu wa rangi nyinginezo na kwa hivyo nafasi yake lazima ingetambuliwa.

Uk. 26. Aya 3

> *…Sauti iliyonguruma mwanzoni mwa karne kuwa Kenya ni Nchi ya Mtu Mweupe, sasa ilikuwa imedhoofishwa na mabadiliko makubwa ya kihistoria ambayo yalithibitisha kuwa sauti hiyo ilikuwa kwenye kinywa cha kichaa aliyekuwa ndotoni. Hata hivyo, bado kulikuwa na wazungu wahafidhina, kama Robert Stoneheart, ambao walishikilia kwamba mzungu alikuwa binadamu bora kuliko binadamu wa rangi nyinginezo, na kwa hivyo lazima nafasi yake itambuliwe…*

#### 4.1.2.2.2 Uhamaji

Msimulizi anaeleza kuwa babake Robert Stoneheart licha ya kuzaliwa Uingereza alijiunga na wahamaji wa Kiingereza nchini Kenya na kufika Mombasa mwaka wa 1930. Anaendelea kusema kuwa, yeye na wazazi wake waliselelea Mombasa badala ya kufululiza mpaka White Highlands kama wahamaji wengine.

Uk.24. Aya2

> *...Mwaka wa 1930 alijiunga na wahamiaji wa Kiingereza nchini Kenya, akafika Mombasa. Nilikuwa na umri wa miaka mitano wakati huo... Tuliselelea Mombasa badala ya kufululiza mpaka White Highlands, kama wahamiaji wengi walivyofanya.*

Maelezo haya yanamulika maudhui ya uhamaji ambayo yameelezwa kwa upana katika hadithi. Mfano mwingine ni huu unaoonyesha jinsi babake

msimulizi anavyotaka kuhama kutoka Mombasa hadi mahali pengine baada ya kutoka jela.

Uk.27 Aya 2

> *Babangu alipotoka jela, hakutaka kuendelea kukaa Mombasa. Aliniambia kuwa alitaka tuhamie mahali pengine, ili aweze kusahau yaliyotokea. Kilichonishangaza ni kuwa ijapokuwa alitaka kusahau yaliyotokea, hakuonyesha masikitiko kwa kumuua mamangu…*

**4.1.2.2.3 Ukoloni**

Msimulizi ametaja Italia alikotoka tajiri mmoja jijini Mombasa. Licha ya kuwa mfanyibiashara huyu alikuwa mgeni mjini Mombasa, alimiliki hoteli alikoajiri wazungu na ana sehemu ya kuwajengea wafanyikazi wake nyumba. Kwa mfano, alimwajiri Stoneheart na kumpa nyumba nzuri ya kuishi.

Uk. 24. Aya 3

> *Babangu aliajiriwa kazi na tajiri mmoja kutoka Italia aliyekuwa na biashara ya hoteli. Tajiri huyo alitupa nyumba nzuri yenye vyumba viwili ambamo tuliishi. Nilianza kuenda shule wakati huu. Bado tuliishi katika umaskini lakini maisha nchini Kenya yalikuwa mazuri ikilinganishwa na hali ilivyokuwa tulikotoka.*

Maudhui ya ukoloni yametamalaki katika hadithi. Msimulizi anaeleza kuwa nchi ya Kenya ilikuwa mojawapo ya makoloni ya nchi ya Uingereza na jinsi kulikuwa na mpango wa Waingereza wa kuifanya Kenya kuwa nchi ya mtu mweupe. Nchi ya Kenya na Uingereza zinachangia kujenga maudhui haya kwa sababu zinahusishwa na mpango huu wa wakoloni.

Uk.23. Aya 2

> *Mwanzoni mwa karne ya ishirini, Waingereza walikuwa na njozi. Walitaka kuifanya Kenya "Nchi ya Mtu Mweupe". Nchini Uingereza kwenyewe, na kwingineko katika makoloni yake, ndoto hii likuwa na mashabiki wengi…*

#### 4.1.2.3 Mioyo ya Chuma

##### 4.1.2.3.1 Mapenzi

Nafasi ya nyumbani kwa Kaikai inatumiwa kuonyesha mapenzi ya Milka kwa Kaikai. Milka, japo alikuwa amemtoroka Kaikai, alitoka Nairobi kwenda nyumbani kwa mumewe Kaikai kumjulia hali kufuatia ujumbe aliopashwa na Kiama kwamba Kaikai alikuwa hali mahututi.

Uk. 34 Aya 2

> *Siku moja Milka alipeperushwa na upepo fulani kuja kumtembelea nyumbani. Kilicholeta upepo huu ni salamu alizopokea kutoka kwa Kiama. Yule mwandani wa Kaikai kutoka Mung'etho madukani. Alipofika nyumbani, Milka alikwenda moja kwa moja na kuingia chumabani. Alijikaza kuutawala wahaka uliomtawala moyoni. Alijiambia kwamba kilichomrudisha hapa ni wajibu ambao lazima autekeleze. "Hata unapofarakana na mtu, huwezi kusikia anakufa usiende kumuona", aliwaza.*

Mwandishi anayamulika maudhui ya mapenzi amabayo ameyashughulika kwa upana katika hadithi hii. Maudhui haya yanadhihirika pale ambapo Kaikai anaketi kitandani na mtazamo wake kwa Milka unamkumbusha jinsi zamani macho hayo yalivyochochea mapenzi kwa Milka.

Uk.36 Aya 1

> *Kaikai aliinuka na kuketi kitandani kisha akalirudia swali lake. Milka aligeuka na kumtupia jicho. Macho ya Kaikai ambayo yalionekana kana kwamba yanaelea majini yalimkumbusha mengi. Alikumbuka jinsi macho hayo yalivyomvutia zamani na kuwasha cheche za mapenzi moyoni mwake…*

**4.1.2.3.2 Ushirikiano**

Duka kubwa la Kaikai lililokuwa eneo la Mung'etho lilijengwa kwa ushirikiano wa watoto wake. Baada ya kulijenga duka hilo watoto hao pia walishirikiana kulijaza bidhaa.

Uk. 36: Aya 4

> *…Alimkubusha kwamba watoto walikuwa wamemjengea duka na kulijaza bidhaa. Naam, duka kubwa kushinda zote kote Mung'etho. Mazuri haya yaliyotokea miaka mingi iliyopita, yalizikwa katika kaburi la sahau…*

Ushirikiano ni maudhui ambayo yameshughulikiwa na mwandishi wa hadithi hii, hivyo, duka kubwa la Kaikai linatumika kuyamulika maudhui haya.

Uk.37 Aya 2

> *Siku moja alipokuja kumtembelea mamake, aliamua kumsaidia kuyaokoa maisha yake. Ilikuwa Jumapili…Celina alivikusanya vitu vya mama yake akavitia ndani ya mfuko. Kisha akaongoza njia kuelekea kituo cha matatu…*

Katika aya hii kuna ushirikiano kati ya Celina na mamake wanapokusanya vitu vya mama na kuondoka nyumbani kwa Kaikai.

#### 4.1.2.4 Safari ya Maangamizi

##### 4.1.2.4.1 Elimu

Mabasi ya chuo kikuu cha KWENUKWETU yametumika kuendeleza maudhui ya elimu. Ubavuni mwa mabasi haya pameandikwa kwa herufi kubwa na nzito CHUO KIKUU CHA KWENUKWETU. Hili linaonyesha kwamba mabasi haya yanamilikiwa na taasisi ya elimu. Vilevile, mabasi haya yalikuwa yamejazana wanafunzi wa chuo kikuu waliohudhuria mazishi ya Pendo.

Uk. 164: Aya 2

> ...*Yalipokaribia kiasi cha kuweza kuonekana vizuri, ilibainika wazi kuwa mabasi haya yalikuwa yale ya Chuo Kikuu cha Kwenukwetu. Ubavuni yalikuwa yameandikwa kwa herufi kubwa na nzito: CHUO KIKUU CHA KWENUKWETU. Wanafunzi walikuwa wamejazana ndi! Wengine walikua wamening'inia milangoni na madirishani bila kujali hatari ya kitendo chao*…

### 4.2 Umuhimu wa Nafasi na Mahali katika Kujenga Wahusika

De jong (2012) anaeleza kuwa nafasi na mahali ina dhima ya kujenga mhusika katika simulizi. Hili hufanyika kwa kubainisha mhusika kwa tabia zake za kudumu zinazorejerewa kama sifa au hulka zake. Vilevile, hutumika kuonyesha hali za kisaikolojia za mhusika ambazo hutegemea hali fulani mahususi na hubadilika hali hiyo inapobadilika, hivyo, sifa hizo hazidumu kwa muda mrefu ila ni za muda mfupi tu.

### 4.2.1 Hulka za Wahusika

De jong (2012) anasema kwamba hulka za wahusika ni sifa za kudumu ambazo hujenga maisha ya mhusika fulani. Sifa hizi hudumu kwa muda mrefu na hutumika kumbainisha mhusika fulani kwa maana huwa ni sehemu ya maisha yake.

#### 4.2.1.1 Vinyago vya Watalii

##### 4.2.1.1.1 Chombo

###### 4.2.1.1.1.1Msanii

Kibanda cha Chombo kinatumiwa kudhihirisha sifa yake kama msanii wa uchoraji. Aidha, msimulizi anaitumia picha ya “Kipusa na Adui Yake” kuonyesha usanii wa mhusika Chombo. Anasema kuwa picha hii ndiyo iliyochukuliwa na Chombo kama kilele cha ufanisi wake kama msanii na alikuwa na maazimio ya kuipeleka picha hii kushindania tuzo mojawapo.

Uk.8 Aya 2

> *Chombo alikuwa kijana wa miaka ishirini na sita. Licha ya ujana wake, alikuwa msanii aliyekomaa. Sanaa yake ilikuwa uchoraji. Kibanda chake kilijaa mabango ya michoro yake. Michoro ya mandhari ya kuvutia jijini Mombasa…*

Uk. 9 Aya 2

> *Kulikuwa na picha moja ambayo Chombo aliipenda sana. Aliichukulia picha hii kama kilele cha ufanisi wake kama msanii. Aliposikia habari za mashindano ya uchoraji, aliazimia kuipeleka picha hii kushindania tuzo mojawapo…*

#### 4.2.1.1.1.2 Mwenye tamaa

Kibanda cha Chombo kinatumika kumjenga Chombo kama mhusika mwenye tamaa. Sally anapoingia kibandani mwake na kumkumbatia na kumbusu Chris, kisha kutambulishwa kwa Chombo, alimmezea mate na kuapa kimoyomoyo kutia kila jitihada kumpata.

Uk.11 Aya 5

> *Kabla Chris hajatoka katika kibanda cha Chombo, msichana mrembo wa Kiafrika alikuja mbio mbio na kujitoma humo. Alimkumbatia Chris na kumbusu midomoni…Chombo alimmezea Sally mate. Aliapa kimoyomoyo kufanya juu chini kumpata.*

Msimulizi pia anatumia chumba cha Chombo kumdhihirisha Chombo kama mhusika mwenye tamaa. Anasema kuwa baada ya Chombo na Sally kula na kustarehe ili kulipisha jua la adhuhuri lililowaka sana, damu ya Chombo ilichemshwa na kiumbe aliyekuwa ubavuni pake na dawa yake ilikuwa Sally tu.

Uk. 20 Aya 2

> *Chumbani mwa Chombo. Walishakula sasa wamejilaza kitandani kulipisha jua la adhuhuri lililowaka moto... Dawa ya hali yake haikuwa nyingine bali Sally. Aliitaka dawa hii kuliko alivyowahi kutaka kitu chochote maishani mwake...*

### 4.2.1.3 Mioyo ya Chuma

#### 4.2.1.3.1 Watoto wa Kaikai

#### 4.2.1.3.1.1 Wenye bidii

Kupitia kwa duka kubwa ambalo watoto wa Kaikai walimjengea baba yao huko Mung'etho inabainika kuwa wao wana bidii kubwa. Duka walilomjengea

baba yao lilikuwa kubwa kuliko maduka yote. Isitoshe, walilijaza duka hilo bidhaa.

Uk. 36: Aya 4

> *...Alimkubusha kwamba watoto walikuwa wamemjengea duka na kulijaza bidhaa. Naam, duka kubwa kushinda zote kote Mung'etho…*

**4.2.1.3.1.2 Wenye ushirikiano**

Kwa pamoja, watoto wa Kaikai walimjengea baba yao duka kubwa kushinda yote katika eneo la Mung'etho. Fauka ya hayo, watoto hao walishirikiana kulijaza bidhaa.

Uk. 36: Aya 4

> *...Alimkubusha kwamba watoto walikuwa wamemjengea duka na kulijaza bidhaa…*

**4.2.1.4 Kurudi Nyumbani**

**4.2.1.4.1 Cathy**

**4.2.1.4.1.1 Mwajibikaji**

Hospitali alikolazwa Gatobu kunadhihirisha uwajibikaji wa Cathy. Cathy alikwenda kumwona Gatobu hospitalini na kumtakia mema ya kupata nafuu kwa haraka. Isitoshe, alimhakikishia Gatobu kwamba angepona haraka.

Uk. 64: Aya 1

> *Cathy alikuja kuniona hospitalini siku ya pili. Alipoingia kwenye wadi, alikuta nikiandaliwa kupelekwa kwenye chumba cha kupasuliwa.*
>
> *"Maskini Gatobu! Yalikupata kwa nini haya?" Alisikitika.*
>
> *"Lakini utapona. Utapona haraka. Hilo nitahakikisha."*

#### 4.2.1.4.1.2 Mwenye mapenzi ya dhati

Wadi ya kawaida na Amnesty Ward zimetumika kuonyesha kuwa Cathy alikuwa na mapenzi ya dhati kwa Gatobu. Cathy anapanga kumhamisha Gatobu kutoka wadi ya kawaida hadi Amnesty Ward ili apate huduma bora za makazi na chakula na aweze kumtunza yeye mwenyewe.

Uk. 69: Aya 4

> *"Kwanza hii wadi ya kawaida nataka utoke leo hii," aliendelea. "Nataka upelekwe Amnesty Ward... Nitafanya mipango ili nije kukutunza mimi mwenyewe."*

### 4.2.1.4.2 Gatobu

#### 4.2.1.4.2.1 Mwenye mapuuza

Nafasi ya nyumbani halisi kwa kina Gatobu inadhihirisha mapuuza ya Gatobu. Yeye anapinga wazo la wazazi wake kuwa nyumbani ni Meru wala si Nairobi. Gatobu aliliona wazo hili kama lisilokuwa na msingi kwa sababu kulingana naye, haikuhalisi mtu kuishi mahali karibu maisha yake yote kisha asipatambue kama nyumbani.

Uk.74: Aya 1

> *...Nilipokua na kuanza kuwa na mawazo yangu mwenyewe, nililiona hilo wazo la "Nyumbani ni Meru" kama lisilokuwa na msingi. Itakuwaje mtu aishi Nairobi karibu maisha yake yote na bado asipatambue kama nyumbani?*

#### 4.2.1.4 Safari ya Maangamizi

##### 4.2.1.4.1 Wanakijiji

###### 4.2.1.4.1.1 Wasiowajibika

Wanakijiji hawakuwajibika kutengeneza barabara iliyoelekea kwa Mzee Majuto. Kwa muda mrefu barabara ilikuwa katika hali mbovu kwa kuwa na mashimo makubwa yaliyofanya vidimbwi wakati wa masika. Hali hii inaonyesha kutojali kwa wanakijiji kwa mazingira yao hadi pale kifo cha mmoja wao kinatokea na kuwalizimu kuitengeza barabara hiyo ili kurahisisha usafiri.

Uk. 161: Aya 2

> *... Magari manne yalionekana yameegeshwa* kando ya barabara *iingiayo kwa Mzee Majuto. Kwa muda mrefu, barabara hii ilikuwa katika hali mbovu. Ilikuwa na mashimo makubwa ambayo yalifanya vidimbwi wakati wa masika.*

##### 4.2.1.4.2 Vijana

###### 4.2.1.4.2.1 Wenye ushirikiano

Vijana wa kijiji cha mzee Majuto walishirikiana kuikarabati barabara iliyoelekea kwa Mzee Majuto kama sehemu ya maandalizi ya mazishi ya Pendo. Barabara ambayo kwa muda mrefu ilikuwa mbovu ilikarabatiwa na vijana ili kufanikisha usafiri.

Uk. 161: Aya 2

> *... Magari manne yalionekana yameegeshwa kando ya barabara iingiayo kwa mzee Majuto. Kwa muda mrefu, barabara hii ilikuwa katika hali mbovu. Ilikuwa na mashimo makubwa ambayo yalifanya*

> *vidimbwi wakati wa masika. Hata hivyo, vijana wa Kijiji hiki wakiongozwa na Kabole walikuwa wameikarabati barabara ili kufanikisha usafiri wa hususan magari…*

**4.2.1.4.3 Wanafunzi wa Chuo Kikuu**

**4.2.1.4.3.1 Watovu wa nidhamu**

Mabasi ya chuo kikuu yanatumika kuonyesha utovu wa nidhamu wa wanafunzi wa chuo kikuu. Mabasi haya yalikuwa yamejazana wanafunzi ndi! Huku wengine wao wakining'inia milangoni na madirishani bila kujali hatari ya kitendo chao.

Uk. 164: Aya 2

> …*Ubavuni yalikuwa yameandikwa kwa herufi kubwa na nzito: CHUO KIKUU CHA KWENUKWETU. Wanafunzi walikuwa wamejazana ndi! Wengine walikuwa wamening'inia milangoni na madirishani bila kujali hatari ya kitendo chao…*

**4.2.2 Hali za Kisaikolojia za Wahusika**

Kwa mujibu wa De jong (2012), hali za kisaikolojia za mhusika ni zile sifa za muda ambazo husababishwa na hali zilizopo katika wakati maalum. Hali hizi huwepo kisha zaweza kutoweka baada ya muda mfupi. Hali za kisaikolojia za wahusika zinabainika katika hadithi teule kama ifuatavyo.

#### 4.2.2.1 Vinyago vya Watalii

##### 4.2.2.1.1 Chombo

###### 4.2.2.1.1.1 Mwenye wivu

Wivu wa Chombo unadhihirika katika kibanda chake baada ya Sally ambaye ni msichana wa Kiafrika kuingia kibandani na kumwonyesha mapenzi mpenziwe mzungu Chris. Msimulizi anaeleza jinsi Chombo alivyomwonea gere Chris kwa sababu ya uhusiano wake na Sally msichana wa Kiafrika. Pia alilalamika kuwa wazungu waliwanyang'anya wasichana wao kwa kutumia dola.

Uk.11 Aya 5

> *...Alimwonea Chris wivu. "Hawa wazungu wanakuja hapa na kutumia dola kutunyang'anya wasichana wetu. Hata mimi sasa ninazo dola. Wacha tushindane," alijisemea kimoyomoyo.*

##### 4.2.2.1.2 Sally

###### 4.2.2.1.2.1 Mwenye majivuno

Sally anasema kwa majivuno kuwa yeye na Chris wanaenda *States* kufunga ndoa. Anaotea nchi ya Marekani sawa na makahaba wa jiji la Mombasa. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba amedandanyika kwa sababu Chris analikwepa mada ya kuondoka kwenda Marekani na Sally.

Uk. 15 Aya 4

> *"Ndiyo. Mimi na Chris tunakwenda States kufunga ndoa," Sally alisema kwa sauti iliyojaa fahari...*

#### 4.2.2.1.2.2 Mwepesi wa kushawishika

Ile furaha ya Sally kuwa wataondoka kwenda Marekani kufunga ndoa na Chris inaonyesha jinsi Sally anavyoshawishika kwa haraka. Anamwambia Chombo jambo hili kwa fahari. Hata hivyo, mwenzake Chris haichangii mada hii bali anaikwepa.

Uk. 15 Aya 5

> *Chris alikwepa mada ya kuondoka kwenda Marekani na Sally. Hili liliimarisha imani ya Chombo kwamba Sally kadanganywa.*

### 4.2.2.2 Mioyo ya Chuma

#### 4.2.2.2.1 Kaikai

#### 4.2.2.2.1.1 Mwenye wasiwasi

Kioo kilichokuwa juu ya meza ndogo kando ya kitanda cha Kaikai kinachangia kuonyesha hali ya kisaikolojia ya Kaikai. Kupitia kwa kioo hiki Kaikai anabainika kama mtu mwenye wasiwasi kwa sababu anajitazama kwenye kioo ili kutafuta dalili za uzimwi ndani yake. Hili linatokea baada ya kujishuku kuwa mnyama au zimwi, mkewe Milka aliposhtuka na kuzirai baada ya Kaikai kushuka kitandani.

Uk.39 Aya 2

> *…Kulikuwa na meza ndogo kando ya kitanda. Juu yake kulikuwa na kioo. Kaikai alikichukua na kujiangalia. Alijikodolea macho kutafuta dalili za uzimwi.*

### 4.2.2.3 Kurudi Nyumbani

#### 4.2.2.3.1 Gatobu

##### 4.2.2.3.1.1 Mwenye mapenzi

Cathy alipoenda kumtembelea Gatobu hospitalini, Gatobu alimwangalia akiwa kitandani akapata hisia ya ajabu. Hisia hii ilikuwa ikimjia kila alipomwona Cathy, ilipita mwilini mwake kama mkondo wa umeme. Hisia hii ilikuwa na nguvu sana kwani ilimtetemesha mwili mzima hata ikamlazimu kufunga macho ili kuipisha.

Uk. 64: Aya 1

> *…Nikiwa bado nimelala chali kitandani, nilipindua kichwa changu kwa shida kumwangalia. Nyuso zetu zilipokutana, ile hisia ya ajabu ambayo daima ilinijia kila nilipomtazama usoni, ilipita mwilini mwangu kama mkondo wa umeme…*

##### 4.2.2.3.1.2 Mwenye uchungu

Kupitia kwa njia ya changarawe ambayo Gatobu alisafirishiwa akipelekwa thieta, hali yake ya uchungu inabainika. Njia hii inamsababishia uchungu mwingi kwani kila mara kitanda kilipotikisika kwa sababu ya changarawe, alihisi uchungu mwingi mwili mzima uliosambaa kutoka mguu uliokuwa umevunjika.

Uk. 65: Aya 4

> *…Mwendo wote, nilikuwa nikitoa mlio wa maumivu kila kitanda kilipotikisika. Njia ilikuwa ya changarawe, na hivyo kilisukasuka sana. Si uchungu huo uliosambaa kutoka mguu wa kushoto uliovunjika hadi mwili mzima.*

**4.2.2.3.1.3 Mwenye msimamo**

Jiji la Nairobi linatumika kuonyesha msimamo alioushikilia Gatobu akilini mwake. Alikuwa ameamua kwamba nyumbani kwake ni Nairobi. Wakati huo alishikilia msimamo huu na hakuwa na nia ya kumshawishi yeyote kukubaliana naye. Hata hivyo, msimamo wake ulibadilishwa baadaye na matukio yaliyofuata maishani mwake yakiwemo ugonjwa na kifo cha mamake mpenzi.

Uk. 74: Aya 2

> *Bila kujali mawazo ya watu wengine, nilikuwa nimeamua kwamba kwangu mimi, nyumbani ni Nairobi. Sikuwa na lengo la kumshawishi yeyote akubaliane name…*

**4.2.2.3.2 Cathy**

**4.2.2.3.2.1 Mwenye masikitiko**

Cathy alipoingia wadini alikolazwa Gatobu alionyesha masikitiko kwa kuwa Gatobu alikuwa amepatwa na janga lililosababisha alazwe hospitalini. Alisikitika kwamba hayo yalimpata.

Uk. 64: Aya 1

> *Cathy alikuja kuniona hospitalini siku ya pili. Alipoingia kwenye wadi, alikuta nikiandaliwa kupelekwa kwenye chumba cha kupasuliwa.*
>
> *"Maskini Gatobu! Yalikupata kwa nini haya?" Alisikitika.*

#### 4.2.2.4 Mihuri ya Majanga

##### 4.2.2.4.1 Obando

###### 4.2.2.4.1.1 Mwoga

Kupitia kwa kijipango kilichokuwa katika mojawapo ya vichuguu, woga wa Obando unabainika. Obando alijificha kwenye kijipango kwa kuogopa kushambuliwa na jinyama lililovamia kijiji cha Wagimbi.

Uk. 117: Aya 2

> *Wakati huu wote Obando alikuwa akiyatazama haya yote katika kijipango kilichokuwa katika mojawapo ya vichuguu…*

###### 4.2.2.4.1.2 Jasiri

Akiwa amejificha kijipangoni alipokuwa akitazamia matukio bondeni, Obando alimkumbuka Sihaha na kuona jinyama lililokuwa likimfuata mwanamume mwingine ili kumshambulia. Alijijasirisha na kuruka mzima mzima huku akiulenga mkuki wake kwa jinyama na kulifuma tumboni barabara.

Uk. 117: Aya 2

> *Obando aliruka mzima mzima akaulenga mkuki wake. Haukukosea. Ulifuma nyangarika lile sehemu ya tumbo. Nusu ya mkuki ilizama tumboni. Wanaume waliokuwa vichuguuni na mitini walishangilia…*

### 4.3 Hitimisho

Sura hii ilionyesha dhima ya nafasi na mahali katika ujeuzi wa maudhui na wahusika. Ilionyesha maudhui mbalimbali yaliyojitokeza katika hadithi pamoja na sifa za wahusika zilizobainishwa kupitia cha nafasi na mahali.

Sura ifuatayo itashughulikia muhtasari wa matokeo ya utafiti pamoja na mapendekezo ya utafiti.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia kwa kifupi matokeo ya utafiti ambao ulichunguza kipengele cha nafasi na mahali katika hadithi fupi ya Kiswahili. Utafiti wetu ulielekezwa na nadharia ya naratolojia na ulilenga kubainisha vipengele vya nafasi na mahali, jinsi nafasi na mahali huwasilishwa na dhima ya nafasi na mahali katika ujenzi wa maudhui na wahusika katika hadithi fupi teule za diwani ya Kurudi *Nyumbani na Hadithi Nyingine*.

## 5.1 Muhtasari wa matokeo ya utafiti

Sura ya kwanza ilishughulikia vipengee vya kimsingi vya uchunguzi wetu. Ilishughulikia usuli wa mada ambao ulieleza historia ya hadithi fupi pamoja na kuifafanua dhana ya nafasi na mahali. Suala la utafiti liliwekwa wazi katika sehemu hii. Vilevile, malengo na maswali ya utafiti yalibainishwa pamoja na kupambanua sababu za kuchagua mada yetu. Upeo na mipaka ya utafiti wetu ilibainishwa pia. Isitoshe, sehemu hii ilionyesha baadhi ya tafiti zilizoshughulikia mada zinazohusiana na mada yetu ya utafiti. Nadharia iliyoongoza utafiti ilibainishwa pamoja na kufafanua mihimili ya nadharia iliyotumika katika utafiti wetu. Hatimaye sura hii ilifafanua mbinu za utafiti zilizotumika katika uchunguzi wetu.

Sura ya pili ilibainisha vipengele vya nafasi na mahali katika hadithi teule za diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* kama zinavyoelezwa na De

jong (2012). Ilifafanua nafasi ya hadithi kama jumla ya mazingira ambamo matukio ya hadithi hutukia katika hadithi ya fasihi. Aidha ilifafanua dhana ya nafasi ya msimulizi ambayo hubainisha anakotoka msimulizi wa hadithi fulani. Fremu kama mojawapo ya vipengele vya nafasi ilielezwa kuwa ni mahali pa kufikirika ambapo hutokea mawazoni mwa msimulizi au mhusika bila kuwa mahali halisi pa matukio ya hadithi. Hatimaye, vielezo vilifafanuliwa kwa kutoa maelezo ya kina kuhusu vitu, mahali, watu na matukio ya hadithi.

Sura ya tatu ilionyesha jinsi kipengele cha nafasi na mahali kinavyowasilishwa kwa msomaji au msimuliwa wa hadithi fupi. Uwasilishaji huu huonyesha uhusishaji kama mojawapo ya mbinu za uwasilishaji. Mtafiti alibainisha kwamba uhusishaji una jinsi tatu ambazo ni kupitia jicho la msimulizi, jicho la kivuli ambaye si msimulizi wala mhusika lakini ni mtu asiyebainika wazi. Uwasilishaji pia hufanyika kupitia kwa jicho la mhusika kwa mbinu kama vile kutazamia dirishani, kuingia mahali kama nyumba, kutembea mahali kama mjini, kutazama chombo na kumweleza mhusika mwingine kukihusu na kupitia kwa mhusika anapokitengeza kitu fulani. Mtazamo au mahali pa msimamo ni mbinu nyingine ya uwasilishaji iliyoshughulikiwa. Mtafiti alibainisha mtazamo wa kipanorama unaojumuisha kipanorama kando na kipanorama igizi, mtazamo wa kimandhari huku akibainisha kimandhari hamaji na kimandhari tuli na mtazamo karibu. Sehemu nyingine ya uwasilishaji iliyoangaliwa ni sifa za uafafanuzi katika vielezo. Mtafiti alieleza sifa za: Kuangazwa, za sauti, za harufu, na za mguso. Mwishowe,

alishughulikia maumbo ya vielezo ambayo ni vielezo virefu, vifupi, vya kimhutasari, vya kiufundi na vya kihistoria.

Sura ya nne ilibainisha dhima ya nafasi na mahali katika ujenzi wa maudhui na wahusika wa hadithi fupi. Sehemu ya maudhui ilionyesha jinsi nafasi na mahali hujenga maudhui huku ikiwa maudhui au kwa kumulika maudhui ambayo tayari yanashughulikiwa katika hadithi. Zaidi ya hayo, mtafiti alionyesha dhima ya nafasi na mahali katika ujenzi wa wahusika kwa kubainisha sifa za kudumu za wahusika na hali za kisaikolojia za wahusika.

## 5.2 Changamoto katika utafiti

Uchunguzi wetu ulipatwa na changamoto ya ukosefu wa istilahi za Kiswahili za kurejelea baadhi ya dhana za lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kijerumani tulizozipata katika usomaji wetu. Marejeleo mengi ya kazi yetu yalikuwa ya lugha ya Kiingereza ambayo pia yalikuwa na baadhi ya makala ya lugha ya Kijerumani ambayo yalihitaji kutafsiriwa kwa Kiswahili. Changamoto hii iliongeza gharama ya utafiti wetu kwa kuwa wakati mwingine tulihitajika kulipia huduma za kutafsiri. Hata ivyo, tulijaribu kadri ya uwezo wetu kufanya tafsiri hizi na kudumisha maana asilia.

Changamoto nyingine ilikuwa mwingiliano wa kimaana wa dhana za Kiswahili ambao ungepotosha maana iliyokusudiwa. Muda wetu wa utafiti uliongezeka kwa kuwa ilitubidi kurudi baadhi ya sehemu za kazi hii ili kuondoa utata uliotokea. Ili kusulushisha tatizo hili tulitumia tafsiri sisisi na wakati mwingine utafsiri wa kiuamilifu.

Uhaba wa vitabu vya marejeleo yaliyohusiana na mada yetu ya utafiti ilikuwa pia ni changamoto. Vitabu vichache mno vilipatikana maktabani na vilishughulikia mada yetu ya utafiti kwa ufinyu mno. Changamoto hii ilipandisha gharama ya utafiti kwa kuwa tulilazimika kununua baadhi ya vitabu. Tuliikabili changamoto hii kwa kutafuta na kununua vitabu mtandaoni.

Utafiti wetu pia ulikumbwa na changamoto ya wakati. Majukumu mengi ya kikazi yalitatiza utafiti na hata ilikuwa vigumu kupata ruhusa ya kufanya utafiti. Hili lilifanya utafit wetu kuchukua muda mrefu zaidi ya tulivyokadiria. Hata hivyo, tulijizatiti na kuikamilisha kazi.

## 5.3 Mchango wa utafiti

Utafiti wetu ulifafanua kipengele cha nafasi na mahali kwa kukitolea maelezo ya kina na kuonyesha aina zake ili kieleweke barabara kwa wasomi, watunzi na wahakiki wa kazi za fasihi. Kipengele ambacho hapo awali kilieleweka kama mazingira ya matukio ya hadithi kilielezwa zaidi kwa kufafanua dhima zake ambazo ni zaidi ya kuipa hadithi uwanja wa matukio. Uchunguzi huu ulibainisha kwamba kipengele cha nafasi na mahali kina dhima ya kujenga maudhui na wahusika wa hadithi. Kazi hii itawafaa sana waandishi wa hadithi fupi pamoja na wasomi na watafiti wa baadaye wa fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu pia ulichangia kuuendeleza utanzu wa hadithi fupi kwa kuufanyia utafiti. Isitoshe, utafiti huu ulikieleza kipengee cha nafasi na mahali na kukifanya kieleweke zaidi.

### 5.4 Mapendekezo

Uchunguzi wetu ulijikita katika kubainisha vipengee vya nafasi na mahali katika simulizi, kuonyesha jinsi kipengele cha nafasi na mahali kinavyowasilishwa katika hadithi na kuonyesha dhima ya nafasi na mahali katika ujenzi wa maudhui na wahusika wa hadithi. Hata hivyo, kuna vipengele vingine vya nafasi na mahali ambavyo havikushughulikiwa vinavyoweza kufanyiwa utafiti. Vipengele hivi ni kama vile dhima ya nafasi na mahali katika uashiriaji ili kubainisha kinachosimuliwa na nafasi na mahali fulani katika kazi ya fasihi. Vilevile, utafiti kuhusu dhima ya vielezo katika ujenzi wa ploti unaweza kufanyika. Isitoshe, kipengele cha nafasi na uhuishaji chaweza kutafitiwa kwa kuwa baadhi ya waandishi wana mazoea ya kuvipa vitu vya kimaumbile visivyo na uhai hisia, uhai, miondoko na maumbo ya kibanadamu. Vilevile, utafiti wetu ulichunguza utanzu wa hadithi fupi, hivyo tafiti zaidi zaweza kufanywa kwa kutafiti tanzu nyinginezo za fasihi.

### 5.5 Hitimisho

Sura hii ndiyo iliyotamatisha utafiti wetu. Ilishughulikia muhtsari wa matokeo ya utafiti changamoto katika utafiti, mchango wa utafiti pamoja na mapendekezo ya utafiti.

## MAREJELEO

Arege, T. (2012). *Narration in Swahili Narrative Poetry: An Analysis of Utenzi wa Rasi'Lghuli* (Doctoral dissertation, University of Nairobi, Kenya).

Bachelard, G. (1994). *The Poetics of Space.* Boston: Beacon Press.

Bal, M (1997). *Narratology: Introduction to the Theory of Narrative 2rd edition.* Canada, University of Toronto press.

Bal, M (2009). *Narratology An introduction to Theory of Narrative 3rd edition*. Toronto: University of Toronto press.

Bryman, A. (2016). *Social research methods* (5th ed.). Oxford University Press.

Canter, D. (1977). *The psychology of space*. London: Architectural Press.

Chatman, S. (1978). *Story and Discourse. Narrative Structure in Fiction and Film. London*: Cornell University Press.

Chemtai, M.J. (2016). *Mtindo katika Hadithi Fupi ya Kisasa ya Kiswahili.* Tasnifu ya uzamili chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Creswell. J.W. (2012). *Education research: planning, conducting, evaluating, quantitative and qualitative research.* Pearson education Inc.

De Jong. (2012). *Space in Ancient Greek Literature*. Boston: Leiden.

Dennerlein, K. (2009). Narratologie des Raumes. Berlin: de Gruyter.

Fludernik, M. (1996). *Towards a natural Narratology*: London: Routledge.

Fludernik, M. (2009). *An Introduction to Narratology*. London: Routledge.

Friedman, S.S. (1993). "*Spatialization: A Strategy for Reading Narrative*." *Narrative* 1: 12–23. — (1998). *Mappings: Feminism and the Cultural Geographies of Encounter.* Princeton: Princeton University Press.

Gieryn, F. (2000). *A Space for Place in Sociology*. *Annual review of Sociology,* 26, 463-469.

Harvey, D. (1993). “*From space to place and back again*.” *Mapping the Futures: Local Cultures, Global Change*. Ed. Jon Bird et al. London: Routledge.

Heath, S. (1986). *Narrative space. Ph. Rosen (ed). Narrative Apparatus, ideology. A film theory Reader*. Colombia University Press.

Herman, D. (2001). *Handbook of Narrative Analysis*. Nebraska. University of Nebraska press.

Herman, D. (2007). *The Cambridge Companion to Narrative*. Cambridge. Cambridge University Press.

Hussein, S.S. (2018). *Uchanganuzi wa Maudhui ya Siasa katika Hadithi Mbili: Kikaza ya Oduori na Uteuzi wa Moyoni ya Rayya Timammy.*Tasnifu ya uzamili. (Haijachapishwa).

Jahn, M. (2005). *Narratology: A Guide to the Theory of Narrative*. English Department: University of Cologne.

Kaui, T.M. (2015). *Tathmini ya Usimilisho wa Riwaya na Hadithi Fupi kwa Wanafunzi wa Sekondari Nchini Kenya*. Tasnifu ya uzamifu Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kothari, R.C. (2014). *Research methodology methods and techniques* (3rd ed.) New Delhi. New Age International (P) ltd.

Kyalo, M.J. (2012). *Mandhari katika Hadithi Fupi: Ulinganishi wa Diwani ya Pendo la Heba na Hadithi Nyingine na Mizungu ya Manabii na Hadithi Nyingine.* Tasnifu ya uzamili chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Lutwack, L. (1984). *The Role of Place in Literature*. Syracuse university press.

Massey, D. (1994). *Space, Place and Gender*: University of Minnesota press.

Mbatia, M. (2007). *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Focus Publishers

Mbuthia, E.M (2003*). A Stylistic and Thematic Analysis of Kiswahili Short Stories*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mbuthia, E.M na IribeMwangi, P.I. (2014) *An Analysis of Stylistic Trends in Published Kiswahili Short Story Genre*. *Education and Practice* 5 (8).

Misoi, D. (2022). *Dhima ya Usimulizi katika Uwasilishaji wa Nyimbo za Taarab*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili*: *Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi.* Nairobi. East African Educational Publishers.

Monster, L. (2009). *Taking Place. An Introductionto the Concept of Place and Its Literary Potential in Edda, 4-2009.* Oslo: Universitetsfolaget.

Mugenda, O., and Mugenda, A. (2003). *Reasearch Methods Quantitave and Qualitative Approaches.* Nairobi. Act Press.

Mugenda. O.M na Mugenda. A. M (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi.Acts Press.

Ntiba, O.G. (2011). *Taathira ya Dhamira kwa Mtindo katika Hadithi Fupi Teule za Kiswahili.* Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Nzong'a, P.S. (2020). *Mgao Mpya wa Kazi za Wanaume katika Hadithi Fupi za Kiswahili.* Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Ohly, R. (1977). Problems of Literary Genre in Swahili*: Kiswahili Journal of the Institute of Kiswahili Research*. *47*(1).

Phelan, J. & Rabinowitz, P.J. (2005). *A Companion to Narrative Theory*. Oxford. Blackwell Publishing Limited.

Piatti, B. et al. (2009). *Mapping Literature: Towards a Geography of Fiction.* In Cartwright et al., (Eds.): *Cartography and Art.* Berlin Heidelberg, Springer 2009, 179-194.

Relph, E. (1976). *The Placelessness of Place*. Pion.

Rollin, J.D (1983). *A History of Swahili Prose*, *part1*.Netherlands. Leiden.

Ronen, R. (1986). "*Space in Fiction*." *Poetics Today*. Munich. Ludicium Verlag.

Rowle, G.D. (1983). Place and Personal Identity in Old Age: Observation from Appalachia. *Journal of Environmental Psychology*, *3*, (299-313).

Ryan, M. [(2009) 2014]. *"Space*" (rev.22apr.2014). *The Living Handwork of Narratology*. Ed. Peter Huhn et al. Accessed 21 Feb 2015. Http://www.Ihn.Uni-hamburg.de/article/space.

Ryan, M.L. (2010). Space in Huhn, P (eds). *The Living Handbook of Narratology*. Humburg. Humburg University Press.

Stanzel, F.K. (1984). A Theory of Narrative. Goedsche, G., Translated. Cambridge: Cambridge University Press.

Steele, F. (1981). *The Sense of Place*. Boston. CBI publishing.

Tuan, Y.F. (1977). *Space and Place: The Perspective of Experience.* University of Minnesota press.

Tuan, Y.F. (1980). Rootedness versus Sense of Place. *Landscape*, *24* (3-8).

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Msingi na vipengele vyake*. Nairobi. Phoenix Publishers.

Wegner, P.E. (2002). *Introducing Criticism in 21st Century*. Edinburg. Edinburgh University Press.

Westphal, B. (2011). *Geocriticism: Real and Fictional Spaces*. Ontario: Palgrave.

Zoran, G. (1984). Towards a Theory of Space in Narrative. Poetics Today 5, 2: 309-335.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho I: Idhini ya Kufanya Utafiti

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 810901 Ext. 4150

Internal Memo

FROM: Executive Dean, Graduate School

DATE: 28th September, 2023

TO: Njoroge Florence Wahu
C/o Kiswahili & African Languages Dept.

REF: C50/CE/29153/2015

SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH PROJECT PROPOSAL

This is to inform you that Graduate School Board at its meeting of 13th September, 2023 approved your Research Project Proposal for the M.A Degree Entitled, "Nafasi Mahali katika Hadithi Fupi ya Kiswahili."

You may now proceed with your Data Collection, Subject to Clearance with Director General, National Commission for Science, Technology and Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed supervision tracking and progress report forms per semester. The forms are available at the university's website under Graduate School webpage downloads.

Also, please ensure that you publish article(s) from your project before submitting it to Graduate School for examination as per the Commission for University Education and Kenyatta University guidelines.

Thank you.

ELIJAH MUTUA
FOR: EXECUTIVE DEAN, GRADUATE SCHOOL

c.c. Chairman, Kiswahili and African Languages Department

Supervisors:

1. Dr. Jessee Murithi
   C/o Department of Kiswahili & African Languages
   Kenyatta University

## Kiambatisho II: Cheti Cha NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 265060 — Date of Issue: 20/November/2024

### RESEARCH LICENSE



This is to Certify that Ms.. FLORENCE NJOROGE WAHU of Kenyatta University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Nairobi on the topic: NAFASI NA MAHALI KATIKA HADITHI FUPI YA KISWAHILI for the period ending : 20/November/2025.

License No: NACOSTI/P/24/414194

265060

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE,TECHNOLOGY &
INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document,
Scan the QR Code using QR scanner application.

See overleaf for conditions

National Commission for Science, Technology and Innovation -